Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page A

# MAS’ALA YA KIFIQHI

**Kimeandikwa na:**
Sayyid Sharafuddin al-Musawi

**Kimetarjumiwa na:**
Shafi Mohamed Nina

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page B

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 512 - 87 - 4**

Kimeandikwa na:
**Sayyid Sharafud-Din Al-Musawi**

**Kimehaririwa na:**
**Sheikh Abdilahi Nassir**

Kimetarjumiwa na:
**Shafi Mohamed Nina**

Kimepangwa katika Kompyuta na:
**Ukhti Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Octoba, 2010
**Nakala: 1000**

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info

**Kwa kushirikiana na:**
Al-Mustafa International University,
S.L.P. - 3616
Dar es Salaam.
Tanzania
Barua pepe: Tanzania@miu.ac.ir
na:Info@miu.ac.ir
Tovuti: www.miu.ac.ir

# YALIYOMO

Kukusanya Swala..................................................................................2
Je, Bismillahi ni Aya katika Qur'an na je husomwa katika Swala?............................................................................................17
Hoja za wenye kutukhalifu katika Mas'ala haya............................26
Kusoma katika Swala.....................................................................31
Takbira ya kuhirimia Swala...........................................................43
Msafiri kupunguza Swala na kutokufunga Saumu Sharia ya kupunguza Swala..........................................................................45
Sheria ya kutokufunga safari...........................................................47
Hukumu ya kupunguza Swala (Qasr)............................................48
Hoja za Shafii na yeyote asiyeona ni lazima kupunguza Swala.....52
Hukumu ya kutokufunga Saumu.....................................................54
Umbali wa safari ya Swala kupunguzwa na Saumu kutofungwa...58
Ndoa ya Mut'a................................................................................ 61
Itifaki ya umma juu ya usharia wake..............................................63
Ushauri wake kwa Nususi za Hadithi.............................................65
Wenye kusema kuwa imefutwa: hoja zao na kuzifakari................ 66
Hadithi zinamfichua Khalifa...........................................................69
Kupaka miguu au kuiosha katika udhu ..........................................76
Hoja ya Imamiya.............................................................................77
Uchunguzi wa Hadithi za kuosha................................................ 83
Uchunguzi juu ya kutoa kwao hoja hapa kwa Istihisani...............86

Uzinduzi..........................................................................................88
Mpaka katika fundo mbili.............................................................. 90
Kupaka maji juu ya khofu na soks, ................................................92
Kupaka maji juu ya kilemba........................................................ 101
Je, kupaka kichwa kuna mpaka?...................................................104

**Khilafu katika Mas'ala sita:**

Kupaka maji masikio...................................................................105
Je, Inajuzu kuosha kichwa baada ya kupaka?................................106
Mpangilio wa udhu...................................................................... 106
Kutungamanisha katika Udhu...................................................... 108
Kutia nia.........................................................................................109

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page E

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho, *Masaa'ilu 'l-Fiqhiyyah*, kilichoandikwa na mwanachuoni mashuhuri wa Kiislamu, Marehemu Sayyid Abdulhusain Sharafuddin al-Musawi. Sisi tumekiita, *Masiala ya Kifikihi*.

Kitabu hiki huelezea hitilafu zilizopo baina ya Shia na Sunni kuhusu masiala (mas'ala) ya kifikihi na matendo mengine ya kiibada. Wafuasi wa madhehebu hizi wamekuwa wakishutumiana na kila upande ukiona upande wa mwenzake kuwa umepotoka. Sheria zote za Kislamu ziwe za matendo ya kiibada au za kimaisha chimbuko lake ni kutoka kwenye Qur'ani na Sunna, na madhehebu zote za Kiislamu zinakubaliana na kaida hii.

Hivyo, mwanachuoni huyu mkubwa wa Kiislamu anajaribu kuyachambua masiala haya ya kifikihi (kifqhi) ambayo madhehebu hizi hutofautiana kwa kutoa dalili na hoja kutoka kwenye Qur'ani na Sunna na pia matukio ya kihistoria kwa kutumia hoja za kielimu na ujuzi alionao.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Shafi Mohamed Nina kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni changamoto kubwa kwa wasomaji wetu.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**

# UTANGULIZI

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu***

***Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu***

Kitabu kilichopo mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha kiarabu kinachoitwa ***Masaailul Fiqhiyya*** kilichoandikwa na Sayyid Abdul-Husein Sharafud-Din Al-Musawi wa Lebanon. Katika kitabu hiki amechambua mas’ala mbalimbali ambayo madhehebu ya Kisunni na ya Kishia wametofautiana. Katika kitabu hiki ameyaeleza mas’ala hayo kielimu na kiufundi sana, akiwa ni Mshia, na kuheshimu upande wa pili huku akionyesha misingi ya tofauti hizo pamoja na hoja zao, na kuzichambua kwa misingi ya kielimu ili kila mwenye kutaka kujua achague lililo sawa katika tofauti hizo.

Sayyid Abdul-Husein Sharafud-Din alizaliwa Kadhimia, Iraq mwaka 1290 A.H / 1872 A.D. Alizaliwa na wazazi wawili ambao nasaba yao inarudi mpaka kwa Bwana Mtume (s.a.w.w). Alisoma kwa wanazuoni wakubwa waliokuweko Samorraa na Najaf, Iraq. Sayyid Sharafuddin alisoma mpaka akafikia daraja ya *Ijtihad*. Alipofikia umri wa miaka 32 (mwaka 1322 A.H) alirudi Jabal-Aamil (kusini mwa Lebanon) ambako ndiko walikotoka wazazi wake. Sharafuddin, pamoja na kuwa yeye alikuwa mwanachuoni mkubwa, pia alikuwa mwandishi wa vitabu vilivyosifiwa kwa upana wa maelezo, uchambuzi wa ndani, uaminifu wa kunukuu na usahihi wa fikra na ubainifu. Miongoni mwa vitabu vyake ni hiki ulichonacho, *Almuraajaat*, *Annas wal-ijtihaad* na vinginevyo. Baadhi ya vitabu vyake vilipotea maktaba yake ilipochomwa moto na Wafaransa walipokuwa wakimtafuta kwa kosa la kupinga ukoloni wao Lebanon. Vitabu vilivyopotea ni takriban vitabu 19, na vilivyobaki ni zaidi ya vitabu 9 pamoja na makala mbalimbali. Vitabu vyake vingi vilikuwa vinachambua tofauti za

kimadhehebi kwa lengo la kutaka Waislamu wajuane tofauti zao, na wawe pamoja katika yale yanayowaunganisha ili waweze kuulinda Uislamu wakiwa ni nguvu moja.

Sayyid Sharafud-Din aliaga dunia mwaka 1377 A.H / 1957 A.D.

*Wamaa Tawfiiqii Illaa Billaahi*

**Lamu, Kenya**
**Shafi Mohamed Nina**
**11 Dhulqaada, 1423**
**14 Januari, 2003**


بسم الله الرحمن الرحيم

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 2



# KUKUSANYA SWALA MBILI

Hakuna tofauti kati ya madhehebi yote ya Kiislamu juu ya kuruhusiwa kukusanya swala ya adhuhuri pamoja na ya alasiri, na kuziswali zote katika wakati wa adhuhuri siku ya Arafa kwa mahujaji na inayojulikana kwa istilahi yao kama *'Jam-ut taqdim'*.

Pia hakuna tofauti kati yao juu ya kuruhusiwa kukusanya swala ya magharibi na ya isha wakaziswali pamoja katika wakati wa isha**[1]** wanapokuwa Muzdalifa, na hii hujulikana kwa istilahi yao kama *'Jam-ut ta'akhiir'*.**[2]**

Bali hakuna tofauti kwa Waislamu wote kwamba kukusanya swala hizo ni sunna ya Mtume (s.a.w.w). Isipokuwa wametofautiana juu ya kuruhusiwa kukusanya swala mbili mbili hizo (adhuhuri pamoja na alasiri, na magharibi pamoja na isha) katika siku zingine za kawaida zisizokuwa za Arafa na Muzdalifa.

Tofauti hiyo iko katika kuruhusiwa kukusanya swala mbili mbili hizo na kuziswali katika wakati mmojawapo, ima kwa kutanguliza kama wanavyokusanya Arafa, au kwa kuakhirisha kama wanavyofanya Muzdalifa.

---

1 Kuafikiana huku kwa Waislamu wote juu ya kufaa kukusanya swala Arafa na Muzdalifa ni kwa mahujaji peke yake. Ama kwa wasiokuwa mahujaji kuna tofauti na khilafu.

2 Yaitwa hivyo kwa sababu ya kuakhirisha swala ya magharibi kwa kuitoa kutoka katika wakati wake makhsusi na kuiswali pamoja na swala ya isha katika wakati shirikishi na isha. Na kule kukusanya wanapokuwa Arafa kumeitwa jam-ut taqdim kwa sababu ya kuitoa swala ya alasiri kutoka katika wakati wake makhsusi na kuiswali pamoja na adhuhuri katika wakati shirikishi na adhuhuri.

Maimamu wa Ahlul-bayt (a.s), wao wamesema wazi kwamba yafaa kufanya hivyo bila sababu yoyote, isipokuwa kuziswali mbalimbali ni bora; na Shia (wafuasi) wao wamewafuata hivyo hivyo kila sehemu na kila zama walizoko. Kwa sababu hiyo utawaona wao mara nyingi wanakusanya swala ya adhuhuri pamoja na ya alasiri, na magharibi pamoja na ya isha sawa wawe safarini au mjini kwao, wawe na udhuru au wasiwe nao; na kutanguliza (*jam-ut taqdim*) au kuakhirisha (*jam-ut ta’akhir*) katika ruhusa hiyo kwao ni sawa.

Ama madhehebu ya Hanafi; wao wanazuia kukusanya swala kwa vyovyote vile, isipokuwa Arafa na Muzdalifa, pamoja na kuwa kuna Hadith sahihi za kuruhusu hivyo, hususan katika safari; na Hadith hizo ziko wazi lakini wao wameawili (wametafsiri) kwamba kukusanya huko ni kwa sura tu! utajua ubatili wa tafsiri hiyo baadaye inshaallah.

Ama madhehebu ya Shaafi, Maalik na Hambal wao wameruhusu kukusanya swala katika safari japo kuna tofauti baina yao kuhusu nyudhuru zingine kama mvua, matope, maradhi na hofu. Vile vile wametofautiana katika masharti ya safari yenye kuruhusiwa kukusanya swala.[3]

Dalili zetu ambazo tunazitegemea kumwabudia Mwenyezi Mungu katika mas-ala haya na mengineyo ni Hadith zetu sahihi zilizopokewa kwa maimamu wetu (a.s.). Huenda tukawatolea hoja watu wa madhehebu mengine kwa Hadith zao sahihi kufuatana na uwazi wa haya tunayoyasema; na yatutosha sisi zile Hadith zilizopokewa na mashekhe wawili

3 Katika wao kuna aliyeshurutisha safari iwe ni ya ibada, kama vile ya Hajj, Umra, Vita vitakatifu na mfano wake, na isiyokuwa ya ibada hairuhusiwi. Miongoni mwao kuna aliyeshurutisha uhalali wa safari; ama safari ya maasia haifai. Pia miongoni mwao kuna aliyeshurutisha aina fulani ya mwendo (safari), na kuna ambaye hakushurutisha kitu chochote. Yaani safari yoyote itakayokuwa, na kwa sifa yoyote, anaruhusiwa kukusanya. Ukitaka ufafanuzi zaidi utapata kwenye vitabu vyao vya fiqihi.

(Bukhari na Muslim) katika sahihi zao. Hapa tunakuletea zile alizozipokea Muslim katika mlango wa kukusanya swala mbili mjini (bila safari) aliposema: Ametuhadithia Yahya ibn Yahya kwa kusema: Nimesoma kwa Malik kutoka kwa Abii Zubeir kutoka kwa Said ibn Jubeir kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema: “Aliswali Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) adhuhuri na alasiri kwa kukusanya pamoja, na magharibi na isha kwa kukusanya pamoja[4] si kwa sababu ya hofu wala safari.”

Anasema (Muslim) ametuhadithia ibn Abii Shaibah, ametuhadithia Sufiyan ibn Uyainah kutoka kwa Amru ibn Dinar kutoka kwa Abi Shaathaa Jabir ibn Zeid kutoka kwa Ibn Abbas amesema: “Niliswali pamoja na Mtume (s.a.w.w) nane kwa pamoja na saba kwa pamoja, akasema Amru ibn Dinar: niliuliza eh Aba Shathaa, nadhani aliakhirisha adhuhuri na akaswali kwa haraka alasiri na akaakhirisha magharibi na akaswali kwa haraka isha?”

Akasema “na mimi nadhani ni hivyo”[5] **mwisho wa kunukuu**.

**Nasema:** Hawafuati isipokuwa ni dhana tu; na hakika ya dhana haitoshelezi chochote katika haki.

---

4 Nadhani unajua kwamba neno kukusanya swala mbili (*Jam-u Bainas Swalaatain*), kwa istilahi yao, ni kuziswali zote mbili katika wakati mmojawapo, kwa kutanguliza au kuakhirisha. Hivi ndivyo walivyokusudia waliotangulia na waliofuatia kutoka zama za maswahaba mpaka siku hii ya leo, na hapa ndipo kwenye ugomvi kama ulivyosikia hapo juu.

5 Hadth hii ameipokea Ahmad ibn Hambal kutokana na Hadith ya Ibn Abbas iliyoko uk. 221 wa Juzu ya kwanza ya *Al-Musnad* yake; na katika ukurasa huo huo ameitoa kwa njia nyingine kutoka kwa Ibn Abbas akasema: Mtume (s.a.w.w) aliswali (rakaa) saba na nane akiwa Madina wala hakuwa safarini.

Anasema (Muslim): “Ametuhadithia Abu Rabii Az-Zahraani, ametuhadithia Hammaad ibn Zaid kutoka kwa Amru ibn Dinar kutoka kwa Jabir ibn Zaid kutoka kwa Ibn Abbas kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ameswali akiwa Madina saba na nane yaani adhuhuri pamoja na alasiri, na magharibi pamoja na isha.”[6]

Akasema (Muslim): “Amenihadithia Abu Rabii Az-Zahraani ametuhadithia Hammaad kutoka kwa Zubeir ibn Al-Khariit kutoka kwa Abdallah ibn Shaqiq kuwa amesema: Siku moja Ibn Abbas alitutolea hotuba baada ya swala ya alasiri mpaka jua likazama na nyota zikadhihiri. Watu wakawa wanasema swala! Swala! Akasema (mpokezi): Kisha akaja mtu mmoja miongoni mwa Banii Tamim, ambaye sio mzushi, akasema swala! Swala!, Ibn Abbas akamjibu kwa kusema: Je unanifundisha Sunna (za Mtume) ewe usiye na mama wee! Kisha akasema: Mimi nimemwona Mtume (s.a.w.w) akikusanya adhuhuri pamoja na alasiri, na magharibi pamoja na isha. Abdallah ibn Shaqiq akasema: Jambo hilo likanikera moyoni mwangu na kunitia shaka. Nikamwendea Abu Huraira nikamuuliza. Yeye akasadikisha maneno ya Ibn Abbas.[7]

Akasema (Muslim): “Ametuhadithia Ibn Abii Umar ametuhadithia Wakii’ ametuhadithia Imran ibn Hadiir kutoka kwa Abdallah ibn Shaqiq Al-Uqailiy kwamba amesema: Mtu mmoja alimwambia Ibn Abbas, “Swalaa!” Ibn Abbas akanyamaza. Akamwambia tena; akanyamaza. Akamwambia tena mara ya tatu; hapo Ibn Abbas akamwambia: “We! Usiye na mama we! Je unataka kunifundisha mimi swala? Sisi tulikuwa tukiswali swala mbili kwa pamoja katika zama za Mtume (s.a.w.w).

---

6 Hii, katika istilahi ya Balagha, inaitwa: (*lafu wa nashru ghairu murattab*). Na hii inafaa. Kama angesema nane na saba ingelikuwa (*mrattab*).

7 Miongoni mwa udhalilifu wa dunia mbele ya Mwenyezi Mungu na dharau za watu hawa kuwadharau Ahlul-Bayt ni kumtilia shaka Ibn Abbas mpaka wamuulize Abuu Huraira. Laiti wangeitumia Hadith hii baada ya Abuu Huraira kuisadikisha! Vile vile Ahmad Ibn Hambal ameitoa Hadith hii kutoka kwa Ibn Abbas katika *Musnad* yake Juz. 1, uk. 251.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 6



**Nasema:** Vile vile An-Nasaai, kwa njia ya Amru ibn Harmi kutoka kwa Abii Sha’thaa, anasema kwamba Ibn Abbas, akiwa Basra, aliswali adhuhuri pamoja na alasiri na wala hakufanya kitu chochote baina ya swala mbili hizo. Alifanya hivyo kwa sababu ya shughuli. Imam An-Nasaai ameirufaisha Hadith hii mpaka kwa Mtume (s.a.w.w).[8]

Akasema (Muslim): Ametuhadithia Ahmad ibn Yunus na Awn ibn Sallaam wote kutoka kwa Zuhair, amesema Ibn Yunus: ametuhadithia Zuhair, ametuhadithia Abuu Zubair kutoka kwa Said Ibn Jubair kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) aliswali adhuhuri na alasiri zote kwa pamoja akiwa Madina, hakuwa na hofu wala safari.”[9]

Amesema Abuu Zubair: Nikamuuliza Said: Kwa nini Mtume alifanya hivyo? (Said) akasema: Nilimuuliza Ibn Abbas kama ulivyoniuliza, akanijibu: Alitaka asimtie katika taabu mtu yeyote katika umma wake.

Akasema (Muslim): Na ametuhadithia Abu Bakr Ibn Abu Shaibah na Abu Karib wote wawili wamesema: Ametuhadithia Abu Muawiya ametuhadithia Abu Karib na Abu Said Al-Ashaj wote wawili wamesema, ametuhadithia Waqii na Abu Muawiya wote wawili kutoka kwa Al-Aamash kutoka kwa Habib Ibn Abi-Thabit kutoka kwa Said ibn Jubeir kutoka kwa Ibn Abbas, anasema: Mtume (s.a.w.w) alikusanya adhuhuri pamoja na alasiri na magharibi pamoja isha akiwa Madina; si kwa sababu ya hofu wala mvua.

Akasema (Muslim): Na katika Hadith ya Wakii’ amesema: Nilimuuliza Ibn Abbas kwa nini (Mtume) alifanya hivyo (alikusanya swala)? Akajibu: Ili asiwape taabu umma wake. Na katika Hadith ya Abii Muawiya, Ibn Abbas

8 Kama alivyoinakili Hadith hii Az-Zarqaani katika mlango wa kukusanya swala mbili katika kitabu chake, Sherehe ya *Muwattaa* uk. 263, Juzuu ya Kwanza .

9 Hadith hii ni miongoni mwa Hadith alizozitaja Imam Malik katika mlango wa kukusanya swala mbili, katika kitabu chake *Al-Muwattaa*, na vile vile Imam Ahmad katika *Musnad* yake kutoka kwa Ibn Abbas.

aliulizwa: Mtume alikusudia nini kwa kufanya hivyo? Akajibu: Alikusudia kuwaondolea taabu umma wake.

Akasema (Muslim): Ametuhadithia Yahya ibn Habib Al-Haarithi, ametuhadithia Khalid ibn Al-Harth, ametuhadithia Qurrat ibn Khalid ametuhadithia Abuu Az-Zubair, ametuhadithia Said Ibn Jubair, ametuhadithia Ibn Abbas: “Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alikusanya swala alipokwenda Vita vya Tabuk, akakusanya adhuhuri pamoja na alasiri, na magharibi pamoja na isha. Said akasema: Nikamuuliza Ibn Abbas nini kilimfanya afanye hivyo? Akajibu: Alitaka kuwaondolea taabu umma wake.”

Akasema (Muslim): Ametuhadithia Yahya ibn Habiib, ametuhadithia Khaalid ibn Al-Harth, ametuhadithia Qurrat ibn Khaalid, ametuhadithia Abuu Zubair, ametuhadithia Aamir ibn Waailah Abuu Tufail, ametuhadithia Muaadh ibn Jabal amesema: Mtume wa Mwezi Mungu (s.a.w.w), katika Vita vya Tabuk, alikusanya swala ya adhuhuri pamoja na alasiri, na magharibi pamoja na isha. Akasema (Aamir): Nikamuuliza kwa nini alifanya hivyo? Akajibu (Muaadh): Alitaka kuwaondolea taabu umma wake. (Mwisho wa kunukuu kutoka kwa *Sahihi Muslim*).

**Nasema:** Hadith hizi sahihi zinasema waziwazi kwamba sababu ya kuwekwa sheria ya kukusanya swala si jambo lingine ila ni kuwapa nafasi umma (Waislamu) bila sharti lolote, na ili wasitiwe kwenye shida ya kuziswali pweke pweke. Hivi ni kuwaonea huruma wenye shughuli nyingi; na hawa ndio watu wengi (katika umma wa Kiislamu).

Na hizi Hadith mbili za mwisho (ile ya Muaadh na iliyo kabla yake) hazihusiki na safari peke yake, kwani sababu ya kukusanya swala katika Hadith hizo haina fungamano na safari kama safari, wala maradhi, wala mvua, wala matope, wala hofu kama udhuru, bali hiyo ni miongoni mwa zile hukumu zenye kuenea japokuwa sababu yake ya kuwekwa hukumu hiyo ni kitu au sehemu maalumu. Kwa hiyo hukumu hiyo haiwezi kuhusishwa na sehemu hiyo peke yake, bali itaingia katika kila sehemu ambapo

inakubalika kukusanya. Kwa sababu hiyo, utamwona Imam Muslim hakuziweka Hadith hizo mbili katika mlango wa kukusanya swala ukiwa safarini, kwa kuwa Hadith hizo hazihusiki na safari peke yake, bali ameziweka katika mlango wa kukusanya swala ukiwa mjini kwako ili ziwe ni zenye kujulisha kwa neno la kukata, kuwa inajuzu kukusanya swala bila ya kuhusika na sababu ya safari peke yake au sababu nyingine. Na haya yote ni kutokana na kufahamu kwake (Imam Muslim), elimu yake na usafi wake wa moyo.

Na Hadith zake hizi zilizo sahihi - katika maudhui haya - tulizozitaja na ambazo hatukuzitaja, zote ni sahihi kwa masharti ya Bukhari, kwani watu wote waliopokea Hadith hizi wote wametegemewa kwa hoja na Bukhari katika *Sahihi* yake. Sasa ni nini kilichomfanya Bukhari asizipokee hizo zote katika *Sahihi* yake? Na ni nini kilichomfanya achukue kitu kidogo tu katika hizo? Na ni kwa nini hakuziwekea katika kitabu chake mlango maalumu wa kukusanya swala kwa mtu akiwa mjini kwake, wala mlango wa kukusanya swala safarini, pamoja na kuwa kuna Hadith nyingi sahihi, tena kwa masharti yake yeye mwenyewe, ambazo zazungumzia kukusanya swala, na ilhali maimamu wote kwa ujumla wamejawazisha kukusanya swala? Na ni kwa nini alichagua Hadith za kukusanya swala zile ambazo zinajulisha kufaa kukusanya kwa mbali (haziko wazi katika jambo hilo)? Na ni kwa nini aliziweka katika mlango ambao zaweza zisijulikane kuwa zajulisha kukusanya swala? Mimi namshuku na namwogopea kuwa yeye yuko pamoja na wale wenye kupotoa neno na kulitoa katika maana yake, au ni katika wale wenye kuficha haki na hali ya kuwa wanaijua.

Hapa tunakuletea zile alizozichagua katika maudhui haya na kuziweka katika maudhui mengine, pale aliposema katika Mlango wa 'Kuakhirisha Swala ya Adhuhuri Mpaka Wakati wa Alasiri,' katika kitabu (mlango) cha

Nyakati za Swala katika *Sahihi* yake:[10] Ametuhadithia Abuu Nu'umani; amesema: Ametuhadithia Hammaad ibn Zaid kutoka kwa Amru ibn Diinaar kutoka kwa Jabir ibn Zaid kutoka kwa Ibn Abbas kwamba Mtume (s.a.w.w) aliswali Madina saba na nane, adhuhuri pamoja na alasiri na magharibi pamoja na isha. Akasema Ayub: Huenda ulikuwa ni usiku wenye mvua. Akajibu: Huenda.
**Nasema:** Hakuna wanachokifuata isipokuwa ni dhana tu!!

Na ameandika Hadith katika Mlango wa 'Wakati wa Magharibi' kutoka kwa Adam. Amesema: Ametuhadithia Shuu'bah; amesema: Ametuhadithia Amru ibn Diinaar; amesema: Nimemsikia Jabir ibn Zaid kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema: Mtume (s.a.w.w) aliswali saba kwa kukusanya, na aliswali nane kwa kukusanya.

Na anasema (Bukhari) katika 'Mlango wa Kutaja Isha na Atamata': Kutoka kwa Ibn Umar, Abii Ayub na Ibn Abbas kwamba: Mtume (s.a.w.w) aliswali magharibi na isha pamoja (alizikusanya) katika wakati mmojawapo.

10 Sheikh Al-Answaari alipofika katika mlango huu katika sherehe yake *Tuhfatul-Baari* alisema: Mnasaba wa Hadith hii ilikuwa inatakikana iwe katika Mlango wa 'Kukusanya Swala ya Adhuhuri Pamoja na Alasiri na Kukusanya Swala ya Magharibi Pamoja na Isha', kwani kufuatana na vile alivyoeleza kwamba ni kutumia 'majazi' na ni upungufu ..., akaendelea kusema: Na kuawili (kutafsiri) kwa kusema kuwa yeye (Mtume) alimaliza swala ya kwanza na wakati wa swala ya pili ukaingia, na akaiswali baada tu ya ile ya kwanza, hivyo ni kinyume cha dhahiri ya maneno ya Mtume. – (Mwisho wa kunukuu kutoka mwisho wa uk. wa 292 juz. 2 ya sherehe yake). Na amesema Alqastwalaan katika uk. 293 wa Juz. 2 ya sherehe ya *Irshaadus Sari:* Na hii tafsiri yake kuwa Mtume alikusanya kwa sura tu, kwa maana ya kuwa yeye aliakhirisha adhuhuri mpaka mwisho wa wakati wake, na akaswali swala ya alasiri katika mwanzo wa wakati wake; tafsiri hii ni dhaifu kwa sababu inahalifu dhahiri ya Hadith. hivi ndivyo walivyosema wanazuoni wengi wa Kisunni, hususan wale waliosherehesha *Sahih Bukhari* kama utakavyosikia, Mwenyezi Mungu akipenda.

Hizi Hadith chache, katika zile nyingi ambazo ni sahihi zinazozungumzia kukusanya swala, zatosha kuwa ni dalili na uthibitisho wa haya tunayoyasema kama ilivyo wazi, na zinatiliwa nguvu na Hadith iliyopokewa na Ibn Mas'ud aliposema: Mtume (s.a.w.w) alikusanya swala (Madina) baina ya adhuhuri na alasiri, na baina ya magharibi na isha. Akaulizwa: Kwa nini umefanya hivyo? Akajibu: Nimefanya hivyo ili umma wangu wasipate taabu. Hadith hii ameitoa Twabran.[11]

Imepokewa kutoka kwa Abdallah ibn Umar[12] alipoulizwa: Kwa nini Mtume (s.a.w.w) alikusanya adhuhuri pamoja na alasiri, na magharibi pamoja na isha, hali ya kuwa yuko mjini kwake na wala hakuwa msafiri? Yeye (Ibn Umar) alijibu kwa kusema: "Alifanya hivyo ili asiwape taabu umma wake."

Kwa ujumla wanazuoni wa jamhuri (*ahlus-sunna*) wote - wanaoruhusu na wasioruhusu - wamejumuika na kukubali kuwa Hadith hii ni sahihi. Pia wanakubali kwamba Hadith hizi zinazungumzia haya tunayoyasema, yaani inafaa kukusanya swala bila sababu yoyote. Rudia kitabu chochote unachokitaka miongoni mwa vitabu vilivyosherehesha Hadith hizo, haya yote utayaona wazi.[13] Ndiyo! Wamezitafsiri ili zilingane na madhehebu yao;

11 Kama ilivyo katika sherehe ya *Muwatta* ya Zarqaani katika uk. 263.wa Juz.1. Amesema: "Kule kutaka kwa Mtume kuwaondolea taabu umma wake, neno hili linakataa kutafsiriwa kwamba ni kukusanya kwa sura tu, kwani kukusanya huku kwa sura tu hakuepukani na taabu…"

12 Katika Hadith ambayo utaipata katika uk. 242 wa Juz. ya 4 ya '*Kanzul-Ummaal'* nayo ni Hadith Na. 5078 aliyoitegemeza kwa Abdallah ibn Umar.

13 Yakutosha sherehe ya Nawawii ya *Sahihi Muslim*, Zarqaani katika kusherehe *Muwattaa* ya Imam Malik, Asqalaani, Qastwalaani na Zakaria Al-Answaari katika sherehe zao za *Sahihi Bukhari* na wengine waliosherehe kitabu chochote cha Hadith ambacho kina Hadith ya Ibn Abbas ya kukusanya swala mbili, na wameisahihisha Hadith hiyo kwa kila njia zake ambazo tumezinukuu kutoka kwa Sahihi Muslim na Bukhari, na wamesema dhahiri ya Hadith hizo ni kujuzu kukusanya swala mjini kwa sababu tu ya kujikinga na taabu; na sijui ni nini kilichowafanya waziache hizo? Huenda hilo likawa ni bahati nzuri kwa Ahlul-Bayt kutoka kwao.

lakini katika tafsiri zao hizo, walikuwa wametatizika katika upofu, na wametahayari katika kiza kikubwa. Yakutosha kile alichokinukuu An-Nawawii katika kusherehesha hizi Hadith katika sherehe yake ya *Sahihi Muslim* aliposema, (baada ya kukubali kwamba dhahiri yake ni kukusanya swala mjini): "Wanazuoni katika Hadith hizi wana *taawiilaat* (maoni) mbalimbali na madhehebu tofauti. Kati yao kuna aliyeawili kuwa ni kukusanya kwa ajili ya udhuru wa mvua."

Akasema: Na hili ni jambo mashuhuri kwa wanazuoni wakubwa wa zamani (waliotangulia).[14]

Akasema: Rai hiyo (ya kukusanya kwa ajili ya mvua) ni dhaifu kufuatana na riwaya (Hadith) ya pili ya Ibn Abbas iliyosema: "Bila hofu wala mvua."[15]

Akasema: Miongoni mwao kuna waliotafsiri kwamba, siku hiyo kulikuwa na mawingu, na Mtume akaswali adhuhuri; na baada ya kuswali, mawingu yakaondoka, na ikaonekana kuwa wakati wa alasiri umekwishaingia, akaiswali katika wakati huo.[16]

Akasema: Na (rai) hii pia ni batili kwa sababu, tuchukulie kwamba alifanya hivyo katika swala ya adhuhuri na alasiri, lakini hakuna uwezekano wa tafsiri hiyo katika kukusanya swala ya magharibi na isha.

Akasema: Na miongoni mwao kuna waliotafsiri kwamba Mtume aliakhirisha swala ya kwanza mpaka mwisho wa wakati wake, akaiswali. Na alipomaliza tu, wakati wa swala ya pili ukaingia na akaiswali katika wakati wake. Kwa hiyo ikawa kukusanya kwake ni kwa sura (picha) tu, (lakini

14 Kama Imam Malik, Imam Shafi na wanazuoni wengine wa Madina.

15 Kwa sababu rai hiyo iko mbali sana na tamko la Hadith, wala hakuna dalili yoyote au fuo (*qariina*) la kuonyesha madai hayo.

16 Huko ni kukisia kwa mafungu na kutupa kwa mbali bila ya kuwa na uhakika!!

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 12



uhakika wake ni kuswali kila swala kwa wakati wake).[17]

Akasema: Na rai hii pia ni dhaifu, au ni batili, kwa sababu inakhalifu dhahiri ya Hadith hizo tena kukhalifu ambako hakutarajiwi.

Akasema: Ibn Abbas alifanya hivyo alipokuwa akihutubia watu na wakampigia kelele 'Swala! Swala!' Na yeye asiwajali, bali akawatolea hoja kwa Hadith hiyo ili kuwathibitishia usawa wa kitendo cha kuakhirisha swala ya magharibi mpaka wakati wa isha, na hatimaye akazikusanya zote katika wakati wa isha. Na Abuu Hurairah alipoulizwa, aliunga mkono bila ya kupinga. Haya yote yako wazi katika kubatilisha tafsiri hizo.

**Nasema:** Ibn Abdulbar, Al-Khatwabi na wengineo wameijibu rai hii (ya kukusanya swala kwa sura tu) kwamba: Kukusanya swala ni ruhusa. Na lau kungekuwa ni kwa sura tu, basi taabu na dhiki yake ingekuwa ni kubwa zaidi kuliko kuswali kila swala katika wakati wake wa kawaida, kwa sababu mwanzo wa wakati na mwisho wake ni kitu ambacho wengi wa watu wajuzi hawakijui licha ya watu wa kawaida. (Wakasema): Miongoni mwa dalili (hoja) ya kwamba kukusanya swala ni ruhusa ni lile neno la Ibn Abbas aliposema: "Alitaka (Mtume) asiwape taabu umma wake." (Wakasema): Vile vile dhahiri ya Hadith za kukusanya swala mbili yajulisha kwamba ni kuzitekeleza zote mbili katika mojawapo ya nyakati mbili; ima ni kuiswali swala ya pili pamoja na swala ya kwanza katika wakati wa swala ya kwanza, au kuiakhirisha swala ya kwanza mpaka wakati wa swala ya pili na kuziswali pamoja katika wakati huo wa swala ya pili. (Wakaendelea): Na hili ndilo linalofahamika kutokana na tamko la kukusanya (*jam-u*) katika Hadith zote za kukusanya swala. Na hapa ndio mahala penye khilafu na ugomvi.

[17] Huenda ukawa unajua kuwa Abuu Hanifa na wafuasi wake wamezitafsiri Hadith za kukusanya swala mjini na safarini kuwa ni kukusanya kwa sura tu, na wamesema kuwa haifai kabisa kukusanya swala. Na hii ni rai ngeni sana na ni kinyume kabisa. Sisi yatutosha kuwajadili na kuwafanyia uchunguzi walivyojadiliwa na wanavyuoni wengi kama utakavyosikia maneno yao hapo juu.

An-Nawawii amesema: Miongoni mwao wametafsiri kwamba ni kukusanya kwa ajili ya udhuru wa maradhi au udhuru mwingine. (Akasema): Na hii ndiyo kauli ya Imam Ahmad ibn Hambal na Kadhi Husein, miongoni mwa wafuasi wetu. Na rai hii ameichagua Al-Khataabi, Al-Mutawalli na Ar-Ruuyaani katika wafuasi wetu, na hii ni rai teule katika kuawili (kutafsiri) dhahiri ya Hadith hizi.

**Nasema:** Hakuna uwazi wowote katika Hadith hizi wala hakuna hoja yoyote juu ya tafsiri hii waliyoitafsiri. Na kudai hivyo ni kujihukumia tu kama alivyokiri Qastwalaani katika sherehe yake ya *Sahihi Bukhari*[18]

Baadhi ya wanazuoni waliofuatia baadaye wamesema: Yasemekana kwamba kukusanya swala kwa Mtume (s.a.w.w) kulikuwa ni kwa ajili ya maradhi; na hili ametilia nguvu An-Nawawii. Lakini rai hiyo inahitaji uchunguzi zaidi kwa sababu, lau angelikusanya kwa ajili ya maradhi, basi Mtume asingeswali pamoja na wasiokuwa wagonjwa, bali angeswali pamoja na wagonjwa peke yao tu. Lakini dhahiri ya Hadith inaonyesha kwamba Mtume alikusanya yeye pamoja na maswahaba wake; na hivi ndivyo alivyosema wazi Ibn Abbas katika Hadith iliyothubutu kutoka kwake.[19] **Mwisho wa kunukuu.**

18 Rudia sherehe yake Irshaadi Saari Mlango wa Kuakhirisha swala ya adhuhuri mpaka wakati wa alasiri, utapata katika uk. 293 wa Juz. 2; na hapa namnukuu "wameichukulia - yaani Hadith ya Ibn Abbas ya kukusanya mjini - baadhi yao kuwa ni kukusanya kwa ajili ya maradhi, na amelitilia nguvu An-Nawawii lakini wakamwambia kuwa hilo linakhalifu dhahiri ya Hadith, na kufungamanisha (na maradhi) ni kuchagua bila sababu na ni kuhusisha bila chenye kuhusisha." Mwisho wa kunukuu.

19 Rudia uk. 263 wa Juz. 1 ya sherehe ya Zarqaani ya *Muwatta* ya Maalik katika mlango wa ‘Kukusanya Swala Mbili.’

**Nasema:** Kulipokosekana tafsiri za Hadith hizi sahihi za kukusanya swala zenye kukubalika mbele ya wanazuoni, baadhi ya wanazuoni wa jamhuri (*ahlis sunna*) wameafiki rai yetu katika mas-ala haya bila kukusudia. An-Nawawii amewataja baadhi yao baada ya kutaja zile tafsiri potofu ulizozisikia; akasema: "Kuna kundi la maimamu limekwenda (kwa rai) ya kuruhusu kukusanya swala mjini pakiwa na haja ya kufanya hivyo, lakini wasifanye ni ada yao. Hii ndiyo kauli ya Ibn Siiriin na Ash-hab miongoni mwa wafuasi wa Maalik; na ametoa hikaya Al-Khattaabi kutoka kwa Al-Qaffaal Ash-Shaashi Al-Kabiir miongoni mwa wafuasi wa Shaafi; na kutoka kwa Abii Is-haaq Al-Maruuzi kutoka kwa wengi katika wanazuoni wa Hadith. Rai hii pia ameichagua Ibn Al-Mundhir (akasema) dhahiri ya kauli ya Ibn Abbas: "Alitaka (Mtume) kuwaondolea taabu umma wake," inatilia nguvu kwani Ibn Abbas hakutaja maradhi kuwa ni sababu wala kitu kingine chochote, na Mwenyezi Mungu ndie mjuzi." Haya ndiyo maneno yake.[20] Na hivi hivi wamesema wazi wengi wa wanazuoni wao.[21]

Huenda wahakiki wa Kisunni wa siku hizi wakawa wana rai kama yetu (kuruhusu kukusanya swala bila udhuru) kama walivyozungumza nami wengi wao, isipokuwa hawana ushujaa wa kueneza jambo hilo kwa watu wao. Pia inawezekana ikawa kinachowazuia kufanya hivyo ni *ihtiyat* (kutoka shakani) kwani kutokukusanya swala ni jambo lisilokuwa na upin-

20 Katika uk. 455 wa Juz. 4 ya sherehe ya ya *Sahihi Muslim* iliyochapishwa pembezoni mwa sherehe mbili za *Sahihi Bukhari; Irshaadus Saari* na *Tuhfatul Baari*. Wala hakufichiki kumili kwa An-Nawawii kwenye rai hiyo kutokana na mwisho wa maneno yake, kwani ametilia nguvu kwa neno la Ibn Abbas, na akaongeza maneno yake akisema: "Ibn Abbas hakutoa sababu ya maradhi wala sababu nyingine." Kwa sababu hiyo, yakawa maneno yake ya mwisho yanapinga tafsiri yake ya mwanzo.

21 Kama Zarqaani katika sherehi yake ya Muwattaa na wengineo waliosherehe Hadith ya Ibn Abbas kuhusu kukusanya swala mbili kati ya wale waliosherehe vitabu vya Hadith, kama vile Al-Asqalaani, Al-Qastwalaani na wengineo.

zani wala hilafu, nalo ndilo lililo bora kuliko kukusanya. Lakini wamesahau kwamba kutokukusanya kumewafanya watu wengi wenye shughuli nyingi kuacha swala, kama tunavyoona kwa macho yetu. Kwa hiyo kuzikusanya swala kuko karibu sana na kuhifadhi utekelezaji wake. Kwa maana hii lililo *ihtiyat* sana ni wanazuoni kufutu kuruhusu kukusanya swala kwa watu wote ili wawafanyie wepesi wala wasiwafanyie uzito, kwani Mwenyezi Mungu anawapendelea nyinyi wepesi, hawapendelei uzito. Pia Mwenyezi Mungu hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini. Tena dalili na hoja za kuruhusiwa kukusanya swala bila sababu zipo *alhamdu lillah,* tena Hadith sahihi zilizo wazi kama ulivyosikia. Wala sio Hadith peke yake, bali hata kitabu cha Mwenyezi Mungu kilichokamilika na chenye kubaini. Hebu sikilizeni kwa vizuri niwasomee kutoka kwenye *muhkamaat* (aya zilizo nyepesi kufahamu) tuone kwamba nyakati za swala za faradhi ni tatu peke yake: Wakati wa faradhi mbili zenye kushirikiana katika wakati huo, nazo ni adhuhuri na alasiri; wakati wa faradhi mbili, magharibi na isha, hushirikiana katika wakati huo; na wakati wa swala ya asubuhi (alfajiri). Nyamazeni msikize Qur'ani ya Mwenyezi Mungu katika aya ya 78 ya *Surat Banii Israail* inayosema: **"Simamisha swala jua linapopinduka (baada ya mchana kati) mpaka giza la usiku (kuingia usiku) na Qur'ani (swala) ya alfajiri. Hakika Qur'ani ya alfajiri ni yenye kushuhudiwa."**

Amesema Imam Ar-Raazi katika maelezo ya aya hii iliyoko katika *Surat Banii Israail* katika tafsiri yake inayoitwa *At-Tafsiirul Kabiir* (uk. 428 wa Juz. 6), na hapa namnuku: "Tukitafsiri *alghasaq* kuwa ni kudhihiri mwanzo wa kiza, basi itakuwa ni mwanzo wa magharibi,[22] na kwa maana hii zitakuwa nyakati za swala zilizotajwa katika aya hii ni tatu: wakati wa kupinduka jua, wakati wa mwanzo wa magharibi na wakati wa alfajiri." Akasema: "Tafsiri hii inapelekea kuwa kupinduka jua ni wakati wa

22 Imam Ar-Raazi amenukuu maana hii, kuhusu aya hii, katika tafsiri yake kutoka kwa Ibn Abbas, Atwaai na Nadhiir ibn Shamil; na Imam At-Tabrasi katika *Majmail Bayaan* ameinukuu kutoka kwa Ibn Abbas na Qataada.

adhuhuri na alasiri, kwa hiyo wakati huu utakuwa ni wakati wa swala mbili kwa kushirikiana. Vile vile mwanzo wa magharibi utakuwa ni wakati wa swala ya magharibi na isha kwa kushirikiana."

Akasema: "Na hii inapelekea kuruhusiwa kukusanya swala ya adhuhuri pamoja na alasiri, na magharibi pamoja na isha[23] bila masharti yoyote.

Akasema: "Isipokuwa kuna dalili inajulisha kwamba kukusanya swala kwa mtu aliye mjini kwao bila udhuru haijuzu. Kwa hiyo kujuzu kukusanya swala ni lazima kuwe ni kwa sababu ya udhuru wa safari au mvua au kitu kingine."

**Ninasema:** Tumeyachunguza kwa makini na kutia maanani haya aliyoyadai kwamba kuna dalili (hoja) ya kwamba kukusanya swala mjini bila udhuru haifai, lakini hatukupata chochote wala athari yoyote (*na Mwenyezi Mungu anashuhudia*). Ndiyo, Mtume (s.a.w.w) alikuwa akikusanya wakati akiwa na udhuru. Vile vile alikuwa akikusanya wakati hana udhuru wowote, ili tu asiwape taabu umma wake. Wala hakuna upinzani kwamba kutokukusanya ni bora kuliko kukusanya, na ndio maana Mtume (s.a.w.w) alikuwa akilitanguliza hilo isipokuwa akiwa na udhuru; na hii ni kawaida ya Mtume kutanguliza lililo bora, kama ilivyo katika mambo ya suna zote *(rehema na amani ziwe juu Yake)*.

23 Ama tukitafsiri *alghasaq* kuwa ni kiza kizito, itakuwa ni nusu ya usiku, kama ilivyopokewa kutoka kwa Imam Swaadiq (a.s). Basi wakati wa faradhi nne (adhuhuri, alasiri, magharibi na isha) ni kutoka adhuhuri mpaka katikati ya usiku, yaani adhuhuri na alasiri zinashirikiana kutoka kupinduka jua mpaka magharibi, isipokuwa adhuhuri hutangulizwa kabla ya alasiri, na magharibi na isha zinashirikiana kutoka kuzama kwa jua mpaka nusu ya usiku, isipokuwa magharibi huswaliwa kabla ya isha. Ama faradhi ya asubuhi Mwenyezi Mungu ameipwekesha pale aliposema: **"Na Qur'ani ya alfajiri? Hakika Qur'ani ya alfajiri ni yenye kushuhudiwa."**

## JE, BISMILLAHI NI AYA KATIKA QUR'ANI? NA JE HUSOMWA KATIKA SWALA?

Zimetofautiana rai za wanazuoni wa Kiislamu katika mas'ala haya.

Maalik na Al-Auzai wamesema *Bismillah* siyo katika Qur'ani, na wameizuia kabisa kuisoma katika swala za faradhi, sawa iwe mwanzo wa Surat Alhamdu au mwanzo wa sura baada ya Alhamdu, iwe ni kusoma kwa sauti au kwa siri, lakini wamejawazisha kuisoma katika swala za suna.[24]

Ama Abu-Hanifa, Thauri na wafuasi wao wameisoma mwanzo wa Surat Alhamdu lakini wamelazimisha kuisoma kwa siri hata kama ni katika swala za kusomwa kwa sauti, hii inamaanisha kuwa wao wanaafikiana na Maalik na Al-Auzai, na inajulisha hivyo kwani hatujui ni kwanini wamelazimisha kuisoma kwa siri katika swala za kusoma kwa sauti, isipokuwa siyo katika mama wa kitabu (Alhamdu).

Lakini Shaafi ameisoma kwa sauti katika swala zenye kusomwa kwa sauti, na ameisoma kwa siri katika swala zenye kusomwa kwa siri, na ameihesabu ni katika Surat Fatiha. Vile vile hii ndiyo kauli ya Ahmad ibn Hambal, Abi Thaur na Abi Ubaid. Japo kuna tofauti ya maneno yaliyonukuliwa kutoka kwa Shaafi kuihusu *bismillahi* kwamba, je, ni aya katika kila sura isipokuwa Surat Baraat, au siyo aya isipokuwa katika Surat Alhamdu peke yake? Rai zote mbili zimenukuliwa kutoka kwake. Lakini wahakiki miongoni mwa wafuasi wake wameafikiana kwamba *bismillahi*

24 Ibn Rushdi ameyanukuu haya yote kutoka kwa Maalik katika *Bidayatul Mujtahid* uk. 96 Juz. 1 na Ar-Razi anasema katika tafsiri yake *Al-Kabir* uk. 100 Juz. 1 kuhusu bismillah: Amesema Maalik na Al-Auzai kwamba hiyo siyo katika Qur'ani isipokuwa katika Surat An-Namli, wala usiisome katika swala si kwa sauti wala kwa siri isipokuwa katika swala za usiku za mwezi wa Ramadhani.

ni Qur’ani (aya) katika sura zote isipokuwa katika Surat Baraat,[25] na wameawili rai zote mbili zilizopokewa kutoka kwa Imam wao Shaafi.[26]

Ama sisi (Mashia), kwa kuwafuata maimam wa uongofu wa Ahlul-Bayt tumeafikiana kwamba *bismillah* ni aya iliyotimia katika aya saba za *sab’ul mathani* (Alhamdu), na ni aya katika kila sura ya Qur’ani Tukufu isipokuwa Surat Baraat, na mwenye kuacha kuisoma kwa makusudi swala yake ni batili, sawa sawa swala hiyo iwe ni ya faradhi au ni ya suna. Pia ni wajibu kuisoma kwa sauti katika swala zenye kusomwa kwa sauti. Vile vile ni suna kuisoma kwa sauti katika swala zenye kusomwa kwa siri,[27] na ni baadhi ya aya katika Surat an-Naml. Maneno ya maimam wetu katika haya yote yamejaa tele na ni *mutawatir* kimaana na yako wazi kukataza kukhalifu hayo, kama ilivyo katika kauli ya Imam Abi-Abdillah As-Swadiq (a.s)[28] aliposema: “Wananini hao? Wamefanya kusudi katika aya tukufu ya kitabu cha Mwenyezi Mungu wakidai ni bidaa (kuzua) kuidhihirisha, nayo ni *bismillahir rahmanir rahim*.” Hoja yetu katika njia ya jamhuri (ahlu sunna) ni sahihi zao, nazo ni nyingi:

---

25 Kuafikiana huku na taawili (tafsiri) hii ya Imam wao imenukuliwa na kundi la wanazuoni wao, miongoni mwao ni Ar-Razi akizungumzia bismillah katika tafsiri yake *Al-Kabir* uk. 104 Juz. 1.

26 Katika tafsiri hiyo wamesema: Hakuna khitilafu katika asili ya mas-ala haya, isipokuwa wametofautiana katika kunukuu kutoka kwake kwamba ni aya iliotimia katika kila sura au ni sehemu ya aya katika kila sura.

27 Imam Ar-Razi alipokuwa akielezea *bismillah* katika tafsiri yake Al-Kabir ana hoja nyingi za kuisoma kwa sauti katika swala na amenakili katika hoja ya tatu kwamba: “Madhehebi ya Ali (r.a) yalikuwa ni kusoma *bismillahir Rahmanir Rahim* kwa sauti katika swala zote.” Kisha akasema (Ar-Razi): “Hakika hoja hii ina nguvu katika nafsi yangu na imejengeka sana akilini mwangu wala haitoondoka kabisa.

28 At-Twabrasi amenakili kutoka kwake alipozungumzia *bismillahi* katika Juz. 1ya *Majmail Bayan.*

**Ya kwanza**: Hadith iliothubutu kutoka kwa Ibn Juraij kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Said Ibn Jubeir, kutoka kwa Ibn Abbas, katika neno lake Mwenyezi Mungu: **“Hakika tumekupa (aya) saba (za alhamdu) zinazosomwa mara kwa mara...” (15:87)**, akasema ni ufunguo wa Kitabu (Surat Alhamdu) nayo ni: *Bismi llahir Rahmanir Rahim Alhamdu lillahi rabil alamina* ... Akasoma sura yote. Akasema Ibn Jaraij: Nikamuuliza baba yangu: Je, Said amekupa habari kutoka kwa Ibn Abbas kwamba yeye amesema kuwa *Bismi llahir Rahmanir Rahim* ni aya? Akajibu: Ndiyo. Hadith hii ameitoa Al-Hakiim katika *Mustadrak*, pia Dhahabi katika *Talkhis* yake na wote wawili wamesema wazi kwamba *isnadi* ya Hadith hii ni *sahihi*.[29]

**Ya pili**: Hadith iliyo sahihi kutoka kwa Ibn Abbas pia amesema: “Hakika Jibril alipokuwa akija kwa Mtume (s.a.w.w) na akasoma *Bismi llahir Rahmanir Rahim* alikuwa akijua kwamba hii ni sura.”[30]

**Ya tatu**: Pia Hadith iliyo sahihi kutoka kwa Ibn Abbas amesema: “Mtume alikuwa hajui mwisho wa sura mpaka ishuke *Bismi llahir Rahmanir Rahim.”*[31]

**Ya nne**: Hadith iliyo sahihi kutoka kwake pia, amesema: “Waislamu walikuwa hawajui kumalizika kwa sura mpaka ishuke *Bismi llahir Rahmanir Rahim*, na ikishuka *Bismi llahir Rahmanir Rahim* walikijua

29 Rudia tafsiri ya Surat Fatiha katika kitabu cha tafsiri katika *Mustadrak* ya Al-Haakim Juz. 2 na Talkhis yake ya Dhahabi uk. 257 Juz. 2 utapata wote wawili wameeleza kwamba Hadith hii ni sahihi

30 Al-Haakim ameitaja Hadith hii katika kitabu Swalat katika *Mustadrak* yake uk. 231 Juz. 1 na akasema: Isnadi ya Hadith hii ni sahihi lakini wote wawili (Bukhari na Muslim) hawakuitoa

31. Al-Haakim ameitaja katika kitabu Swalat katika *Mustadrak* yake. Pia Dhahabi ameitia katika *At-Talkhisi* yake na wote wawili wakasema wazi kwamba Hadith hii ni sahihi kwa masharti ya masheikh wawili (Bukhari na Muslim) rudia uk. 231 Juz. 1 ya *Mustadrak* na At-Talkhisi yake zilizopingwa chapa pamoja.

kwamba sura iliyotangulia imekoma."[32]

**Ya tano**: Hadith iliyo sahihi kutoka kwa Ummu Salma amesema: "Mtume alikuwa akisoma: *Bismi llahir Rahmanir Rahim Alhmdu lillahi rabil alamin...*" mpaka mwisho wake akiikata herufi baada ya herufi."[33]

Pia kutoka kwa Ummu Salama, amesema kutokana na njia nyingine: Hakika Mtume (s.a.w.w) alisoma katika swala: *Bismi llahir Rahmanir Rahim* na akahesabu kuwa ni aya, *Alhamdu lillahi rabil alamin* aya ya pili, *Arrahmanir Rahim* aya ya tatu, *Maaliki yaumid dini* aya ya nne, *Iyyaka naa'budu waiyyaka nastain* akafunga vidole vitano... Mpaka mwisho wa Hadith.[34]

**Ya sita**: Hadith iliyo sahihi kutoka kwa Naiim Al-Majmar, amesema: Nilikuwa nyuma ya Abu Hurairah (kwenye swala) akasoma: *Bismillahir Rahmanir Rahim...* kisha akaendelea na Ummul Kitab (Surat Alhamdu) mpaka akafika *waladhdhaa'liin* akasema: *Aamiin* na watu wakasema: *Aamiin*[35] na walipotoa salamu akasema: Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake kuwa, hakika swala hii yangu inafanana sana

32 Al-Haakim ameitaja katika *Mustadrak* uk. 232, Juz. 1 kisha akasema: Hadith hii ni sahihi kwa sharti za masheikh wawili, pia Dhahabi ameisahihisha kwa sharti zao na akaitaja katika At-Talkhis

33 Al-Haakim ameitaja Hadith hii katika *Mustadrak* na Dhahabi katika At-Talkhis na wakasema wazi kuwa ni sahihi kwa sharti za masheikh wawili. Rudia *Mustadrak* na *At-Talkhis* yake uk. 232, Juz. 1.

34 Al-Haakim ameitaja Hadith hii kutoka kwa Ummu Salama baada ya Hadith iliyotangulia akitoa ushahidi wa hayo.

35 Siyo katika madhehebi yetu kutamka Aamiin mwisho wa Alhamdu katika swala si kwa anayeswali pweke wala imam wala maamuma, kwa sababu siyo chochote katika swala wala katika Qur'ani na huku ni kuafikiana kwa kauli moja, wala haikupokewa athari yoyote ya Hadith kwa njia yetu, kinyume na Ahli-Sunna, hiyo ni utangao wao kwani wamepokea Hadith zilizosahihi kwa sharti zao zenye kutaja jambo hilo na Hadith hii ya Abu Huraira ni miongoni mwa Hadith hizo, tena Aamiin ni miongoni mwa suna za swala katika madhehebi yao.

na swala ya Mtume (s.a.w.w).[36] Na kutokana na Abu Huraira amesema: Mtume (s.a.w.w) alikuwa akisoma kwa sauti (katika swala) *bismillahir Rahmanir Rahim.*[37]

**Ya saba**: Hadith iliyo sahihi kutoka kwa Anas ibn Maalik amesema: Siku moja Muawiya aliswali Madina akasoma kwa sauti na akasoma *Bismillahir Rahmanir Rahim* mwanzo wa *Alhamdu* na akaacha katika mwanzo wa sura baada ya *Alhamdu* mpaka akamaliza kisomo hicho. Alipotoa salamu waliomsikia miongoni mwa muhajiriina na answar walimwita kutoka kila upande huku wakimwambia: "Ewe Muawiya, je umeiba swala au umesahau?" Na aliposwali baada ya swala hiyo alisoma *bismillahir Rahmanir Rahim* mwanzo wa sura baada ya *Ummul Kitab (alhamdu*)... mpaka mwisho wa Hadith. Al-Haakim ameitaja Hadith hii katika *Mustadrak* na ameisahihisha kwa sharti za Muslim,[38] na wengi miongoni mwa maimamu wa Hadith wameitaja, kama Imam Shaafi katika *musnad*

36 Al-Haakim ameitaja Hadith hii katika *Mustadrak* baada tu ya Hadith mbili za Ummu Salama, na Dhahabi ameitaja katika *At-Talkhis* yake na wote wawili wamesema wazi kuwa Hadith hii ni sahihi kwa sharti za masheikh wawili.

37 Al-Haakim ameitaja Hadith hii baada ya Hadith iliyotangulia akitoa ushahidi (kuwa *bismillah* ni aya katika Alhamdu), na Al-Bayhaqi katika *Asunanil-Kabiir* kama ilivyo katika uk. 105 Juz. 1 ya tafsiri ya Ar-Razi.

38 Dhahabi ameitaja Hadith hii katika *At-Talkhis* na akaisahihisha kwa sharti za Muslim, pia yeye na Al-Haakim wameifanya kuwa ni sababu na ni kipingamizi cha Hadith ya Qatada kutoka kwa Anas aliposema: Nimeswali nyuma ya Mtume (s.a.w.w), Abu Bakr, Umar na Uthman sikumsikia hata mmoja wao akisoma bismillahir Rahmanir Rahim, pia Hadith hii ni batili kama tutakavyofungua wazi karibuni Mwenyezi Mungu akipenda, na Al-Haakim ameitia Hadithi hii na iliyo baada yake ili kuyadangamanisha haya na kuwa ni ushahidi wa kuyabatilisha.

yake,[39] na akatia maelezo ambayo ni muhimu tuyataje hapa:[40] "Hakika Muawiya alikuwa sultani mkubwa sana mwenye nguvu na ukali sana, lau kule kusoma kwa sauti kusingekuwa ni jambo lililozoeleka kwa maswahaba wote muhajirina na answar wasingethubutu kumkataza kwa jahara namna hiyo kwa sababu ya kuacha kusoma *bismillah*... mpaka mwisho.

Na sisi tuna maelezo yetu kuhusu Hadith hii ili nipate kumzindua kila mtafiti, nasema: Kila mwenye kutia maanani katika Hadith hii ataipata kuwa ni hoja (dalili) kwa madhehebi yetu, pia ni dalili ya kutojuzu kusoma kipande cha sura katika swala baada ya Surat Alhamdu kwani muhajirina na answar wasingeweza kumpinga Muawiya isipokuwa ni kulingana na madhehebi yetu katika mas-ala haya mawili.

**Ya nane**: Pia ni Hadith iliyo sahihi kutoka kwa Anas kwa njia nyingine amesema: Nimemsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) akisoma kwa sauti katika swala *bismillahir Rahmanir Rahim*.[41]

**Ya tisa**: Hadith iliyo sahihi kutoka kwa Muhammad ibn As-Siri Al-Asqalaani amesema: Nimeswali nyuma ya Al-Mu'utamir ibn Suleiman swala za alfajiri na magharibi zisizohesabika na alikuwa akisoma kwa jahara *bismillahir Rahmanir Rahim* kabla ya ufunguo wa kitabu (Alhamdu) na baada yake, alikiisoma kwa ajili ya sura (inayosomwa baada ya Alhamdu). Na nimemsikia Al-Mu'utamir akisema: Sikuacha kufuata swala ya baba yangu, na alisema baba yangu: Sikuacha kuwa ni mwenye kufuata swala ya Anas ibn Maalik, na alimesema Anas: Sikuacha kuwa ni mwenye kufuata swala ya Mtume (s.a.w.w).[42]

39 Rudia *Musnad* yake uk. 13.

40 Katika aliyoyanakili Ar-Razi katika hoja ya nne miongoni mwa hoja zake za kusoma kwa sauti bismillah Uk. 105 Juz. 1 ya tafsiri yake *Al-Kabir*.

41 Al-Haakim na Dhahabi wameitaja Hadith hii katika Mlango wa Kusoma kwa sauti bismillahir Rahmanir Rahim katika vitabu vyao na wakasema: Wapokezi wa Hadith hii mpaka wa mwisho wao ni wakweli, na wameifanya Hadith hii ni kipingamizi cha Hadith ya Qatadah kutoka kwa Anas.

**Ninasema:** Nimependezwa na Hadith hii na nyingine kwamba wao walikuwa wakisoma sura kamili baada ya mama wa Qur'ani (Alhamdu) kuanzia kwenye *bismillah* yake mpaka mwisho wa sura, kama yalivyo madhehebi yetu, Hadith nyingi zinajulisha hivyo.[43]

Kutokana na Qatadah amesema: Anas ibn Maalik aliulizwa: Kilikuwa vipi kisomo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Akajibu: Kilikuwa ni cha madda (kuvuta), kisha akasoma (Anas): *bismillahir Rahmanir Rahim* akavuta *Rahman* na akavuta *Rahim*.

Na kutokana na Hamid At-Twawil kutoka kwa Anas ibn Maalik amesema: Nimeswali nyuma ya Mtume (s.a.w.w), Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali wote walikuwa wakisoma *bismillahir Rahmanir Rahim* kwa jahara.

Hadith hizi zote na zilizo kabla yake amezitaja Imam wa wanazuoni wa Hadith Abu Abdillah Muhammad ibn Abdillah Al-Haakim An-Naisaburi katika *Mustadrak* yake kisha akasema baada ya Hadith ya mwisho katika hizo, na hapa namnukuu: "Hakika nimetaja Hadith hii ili iwe ni ushahidi wa yaliyotangulia, kwani katika hizi Hadith tulizozitaja kuna mgongano wa Hadith ya Qatada iliyopokewa na maimam wetu kutoka kwake, na tamko ni kutoka kwa Anas amesema: "Nimeswali nyuma ya Mtume (s.a.w.w.) Abu Bakr, Umar na Uthman sikumsikia yeyote katika wao akisoma *Bismillahir Rahmanir Rahim*", (kisha Al-Haakim akasema): Katika

42 Hadith hii Al-Hakim ameitaja katika *Mustadrak* na Dhahabi katika *At-Talkhis* na wote wawili wamesema wazi kuwa wapokezi wa Hadith hii mpaka mwisho ni wakweli na wameifanya (Hadith hii) kuwa ni sababu ya kuipinga Hadith ya Qatada kutoka kwa Anas iliobatili.

43 Kwani kutokana na Ibn Umar kwamba yeye alikuwa haachi *Bismillahir Rahmanir Rahim* mwanzo wa Surat Alhamdu pia mwanzo wa sura baada ya Alhamdu, na Imam Shaafi ameitoa Hadith hii katika *Musnad* yake uk. 13.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 24



mlango huu kumebaki Hadith iliyopokewa kutoka kwa Amirul muuminina Uthman, Ali, Twalha ibn Ubaidillah, Jaabir ibn Abdillah, Abdallah ibn Umar, Al-Hakam ibn A'mir At-Thamali, An-Nuuman ibn Bashir, Samratu ibn Jundubi, Buraidatu al-Aslami na Aisha binti Swidiq (r.a.), Hadith zote hizi kwangu zimethubutu kupokewa katika mlango huu lakini nimeziacha ili kufupisha, na nimetaja chache tu zenye kufungamana na mlango huu. Vile vile nimetaja katika mlango huu kuwa maswahaba, tabiina na waliowafuatia (r.a.) walikuwa wakisoma kwa jahara *Bismillahir Rahmanir Rahim*." **Mwisho wa kunukuu**.[44]

**Nasema:** Ar Razi ametaja katika tafsiri yake *Al-Kabir*[45] kwamba Al-Baihaqi amepokea Hadith ya kusoma kwa jahara *Bismillahir Rahmanir Rahin* katika Sunan yake kutoka kwa Umar ibn Khattab, Ibn Abbas, Ibn Umar na Ibn Zubair, kisha Ar-Razi akasema na hapa namnukuu: Hakika Ali ibn Abi Twalib (r.a) alikuwa akisoma kwa jahara *Bismillah*, hili limethubutu kwa *tawaturi* (kwa wingi) na mwenye kumfuata Ali ibn Abi Twalib katika dini yake, hakika ameongoka. Akaendelea: Na dalili (hoja) yake ni maneno ya Mtume (s.a.w.w); "Ewe Mwenyezi Mungu izungushe haki pamoja na Ali popote azungukapo."

Yatutosha kuwa ni hoja kwamba *Bismillah* ni aya ya Qur'ani katika ufunguzi wa sura zote isipokuwa Surat Baraat kwamba maswahaba wote, waliokuja baada ya maswahaba, waliowafuatia wao na waliofuatia kila zama katika umma huu tangu ilipoandikwa Qur'ani mpaka leo hii wote wameafikiana kwa vitendo kuiandika *Bismillah* mwanzo wa kila sura isipokuwa Surat Baraat, wameiandika kama walivyoandika aya zingine bila ya kuitofautisha, ilihali wote wameafikiana kutokuandika kitu chochote kisichokuwa Qur'ani mpaka wakipambanue kwa uwazi (kwamba siyo Qur'ani), hii ni bidii yao ili Qur'ani isichanganyikane na kitu kingine.

44 Rudia Uk. 234, Juz. 1 ya *Mustadrak*.

45 Katika hoja ya tano miongoni mwa hoja zake za kusoma Bismillah kwa sauti Uk. 105 Juz. 1.

Je huoni walivyopambanua Qur’ani na majina ya sura, alama za juzu, hizbi, robo, khumsi na ushuri zake, wakaziweka nje ya sura kwa namna ambavyo itajulikana kwamba ziko nje ya Qur’ani ili kufanya *ihtiyat* ya kuihifadhi.

Huenda unajua kwamba ni mara chache sana umma (wa Kiislamu) kuafikiana wote bila kukhalifu hata mtu mmoja kama walivyoafikiana katika jambo hili, hii peke yake ni hoja kuwa *Bismillahir Rahmanir Rahim* ni aya yenye kujitegemea katika kila mwanzo wa sura zote, kwani *salaf* (waliotangulia) na *khalaf* (waliofuatia) wameiweka mwanzo wa kila sura, *alhamdu lillah* kwa usawa huo.

Vile vile miongoni mwa Hadith mashuhuri zilizopokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) ni neno lake: “Jambo lolote muhimu ambalo halikuanzwa kwa *Bismillahr Rahmanir Rahim* halidumu, hukatika.”[46] Na “Jambo lolote muhimu ambalo halikuanza kwa *Bismillah* halidumu na ni lenye kukatika kwa haraka.”[47]

Inavyojulikana, Qur’ani ni bora kuliko wahyi wowote ule aliouteremsha Mwenyezi Mungu kwa Mitume Wake, hakika kila sura katika Qur’ani ni jambo lenye umuhimu na utukufu, kwani Mwenyezi Mungu alibiria (aliwataka wafanye) viumbe na wakashindwa kuleta mfano wake. Je Qur’ani itakuwa ni jambo lenye kukatika? Utakatifu ni wa Mwenyezi Mungu. Utakatifu ni wa Qur’ani Yake yenye hikima na utukufu ni wa sura za Qur’ani kwa kuepukana na hilo (kukatika) tena utukufu wa juu.

---

46 Ameitaja Hadith hii kwa tamko hili Sheikhe Abdul-Kaadir Ar-Rahawi katika Arobaini yake kwa isnadi mpaka kwa Abu Huraira. Ameipokea As-Suyuti katika herufi *alkaf katika Jaamius Saghir* Uk. 91 Juz. 2 na ameipokea Al-Mutaqil Hindi Uk. 193 Juz. 1 katika *Kanzul-Umaal* Hadith ya 2497.

47 Imam Ar-Razi ameitaja kwa tamko hili katika kuzungumzia Bismillah Juz. 1 ya tafsiri yake.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 26



Swala ni njia ya kufaulu na kuokoka, pia ni bora ya amali zote kama kunavyonadiwa katika adhana juu ya minara na mimbari. Hili linajulikana kwa watu wote wa vijijini na mijini, wala haipimwi na kulinganishwa na kitu chochote baada ya kumwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, Vitabu Vyake, Mitume Wake na Siku ya mwisho. Kwa hivyo, je inajuzu kwa Mwenyezi Mungu aweke sharia (katika swala) kitu ambacho ni chenye kukatika? Jambo hilo hathubutu kulisema mtu mwema wala muovu. Lakini maimam wema: Maalik Auzai na Abu Hanifa (r.a.) wamesahau hayo yote.

Kila (mwanachuoni) *mujtahid* anapotafiti kwa dalili (hoja) za kisharia ni mwenye kupewa udhuru na ni mwenye kulipwa mema akipata au akikosa.

## HOJA ZA WENYE KUTUKHALIFU KATIKA MAS’ALA HAYA

Wenye kutukhalifu katika mas’ala haya wametoa hoja nyingi:

**Ya kwanza**: Lau ingekuwa ni aya katika *Surat Al-Fatiha*, ingelazimika kuirudiarudia Ar-Rahmanir Rahiim, na lau ingekuwa ni sehemu ya kila sura ingelazimika kuirudiarudia katika Qur’ani mara mia moja na kumi na tatu.

**Jawabu lake**: Hali hiyo (ya kuirudiarudia) inaweza kulazimika kwa sababu ya umuhimu wa baadhi ya mambo makubwa ili kuyatilia nguvu na kuyatia maanani, na katika kitabu chenye hekima (Qur’ani) kuna mifano mingi sana; inakutosha *Suratu Ar-Rahman, Al Mursalat* na *Al Kafirun*. Na je, ni jambo gani lililo muhimu sana duniani na Akhera ambalo linatakikana kutiliwa nguvu sana na linastahiki kutiliwa maanani sana kama *Bismillahir Rahmanir Rahim*? Kwani, mitume hawakutumilizwa wala malaika hawakuteremshwa wala viumbe vya mbinguni ila ni kwa *Bismillahir Rahmanir Rahim* na uongofu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 27



Wala hazikusimama mbingu na ardhi na vilivyomo (katika mbingu na ardhi) ila ni kwa *Bismillahir Rahmanir Rahim.*[48]

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱذۡكُرُواْ نِعۡمَتَ ٱللَّهِ عَلَيۡكُمۡۚ هَلۡ مِنۡ خَٰلِقٍ غَيۡرُ ٱللَّهِ يَرۡزُقُكُم مِّنَ
ٱلسَّمَآءِ وَٱلۡأَرۡضِۚ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَۖ فَأَنَّىٰ تُؤۡفَكُونَ ﴿٣﴾ ﴾

**“Enyi watu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, je, yuko muumba mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu anayekupeni riziki kutoka mbinguni na aridhini? Hakuna Mungu ila yeye tu, basi ni wapi mnakopinduliwa?” *(Surat Faatir* aya ya 3)**

**Ya pili**: Hadith *marfuu* iliyopokewa kwa Abu Huraira kwamba: Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Nimeigawanya swala nusu mbili, kati yangu na mja wangu. Anaposema mja *Alhamdu lillahi rabil alamin* anasema Mwenyezi Mungu: Mja wangu amenihimidi. Akisema mja: *Ar-Rahmanir Rahim* anasema Mwenyezi Mungu: Amenisifu mja wangu. Akisema: *Maalik yaumiddini* anasema Mwenyezi Mungu: Mja Wangu amenitukuza. Akisema: *Iyyaaka naabudu waiyyaaka nastai’in*, anasema Mwenyezi Mungu: Hili ni kati yangu na mja Wangu…

48 Muumini hufungua kazi zake zote kwa *Bismillahir Rahmanir Rahim*. Akila au akinywa, akisimama au akiketi, akiingia au akitoka, akipokea au akitoa, akisoma au akiandika, akitoa imla au akihutubu au akichinja, husema *Bismillahir Rahmanir Rahim.* Mkunga akipokea mtoto anapozaliwa husema *Bismillah*, mtu akikaribia kufa husema *Bismillah*, akiingizwa kaburini husemwa *Bismillah*, akisimama kutoka kaburini kwake atasema *Bismillah* na akihudhuria (Siku ya Kiyama) atasema *Bismillah* kwani siku hiyo hakuna mahali pa amani wala makimbilio isipo kuwa ni kwa Mwenyezi Mungu. (Mwenyezi Mungu atuthubutishe kwa kauli thabiti katika maisha ya hapa duniani na ya akhera).

Na namna ya kuifanya Hadith hii kuwa ni hoja ni kwamba *Bismillahir Rahmanir Rahim* haikutajwa katika aya za *Surat Fatiha.* Lau ingekuwa ni aya angeitaja.

**Jawabu lake**: Hadith hii inapingana na Hadith ya Ibn Abbas ambayo ni *Marfuu*. Na katika Hadith hiyo Mwenyezi Mungu amesema: Nimeigawanya swala kati yangu na mja Wangu. Mja akisema: *Bismillahir Rahmanir Rahim* Mwenyezi Mungu anasema: Mja Wangu ameniomba... mpaka mwisho wa Hadith,[49] nayo ni ndefu. Ushahidi wetu katika Hadith hii ni kwamba imekusanya *Bismillah*, kwa hiyo inapingana na Hadith ya Abu Hurairah.

Pia yeye Abuu Hurairah, amepokea Hadith kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) kwamba alikisoma kwa sauti *Bismillahir Rahmanir Rahim* katika swala na yeye (Abuu Hurairah) alikisoma kwa jahara *Bismillah*, na akasema: Hakika swala yangu inafanana sana na swala ya Bwana Mtume (s.a.w.w).

Umeishazisoma hadithi zake mbili kuhusu jambo hilo.[50]

**Ya tatu**: Hadith iliyopokewa kutoka kwa A’isha: “Hakika Mtume alikuwa akifungua swala kwa *takbiir* na kusoma *Alhamdu lillahi rabil alamin*.”

Hadith hii sio hoja kwao, kwani yeye (A’isha) alitumia *Alhamdu lillahi rabil alamin* kuwa ni jina la sura hiyo kama unavyo sema: “Nimesoma *kul-huwallahu ahad*, fulani amesoma: *Innaa fatahnaa laka fat-han mubiinaa,”* na mfano wake. Kwa hiyo maana ya Hadith hii ni kwamba Mtume (s.a.w.w) alikuwa akifungua swala kwa *takbiir* na kusoma sura hii ambayo mwanzo wake ni *Bismillahir Rahmanir Rahim*.[51]

49 Al-Mutaqi Al Hindi ameinakili alipozungumzia *Bismillah* uk. 320 Juz. 1, katika *Kanzul ummaal* kutoka katika *Shu’bil-Iman* ya Al-Baihaqii.

50 Rudia Hadith ya sita na iliyo baada yake katika hoja zetu.

51 Huu ni mukhtasari wa yale aliyoyasema Imam Shaafi katika kuwajibu wale waliotoa hoja kwa Hadith hii

**Ya nne**: Hadith ya Ibn Mughaffal aliposema: Baba yangu alinisikia nikisoma *Bismillahir Rahmanir Rahim.* Akasema: Ewe kijana changu, jiepushe na kuzua, kwani mimi nimeswali pamoja na Mtume (s.a.w.w), Abu Bakr, Umar na Uthman sikumsikia yeyote kati yao akiisoma.[52]

**Jawabu lake:** Maimam wa *jarhi wata’diil* (Elimu ya uchambuzi wa wapokezi wa Hadith) hawamjui Ibn Mughaffal. Kwa hiyo Hadith zake hazina thamani kwao. Ibn Rushdi ameitoa Hadith hii alipozungumzia *Bismillah* katika kitabu chake *Bidayatul Mujtahid* [53] na akaiangusha (Hadith hiyo) kwa maneno aliyoyanakili kutoka kwa Abii Umar ibn Abdilbar ambaye ameeleza wazi kwamba Ibn Mughaffal ni mtu asiyejulikana.

**Ya tano:** Hadith ya Shuu’bah kutoka kwa Qatada kutoka kwa Anas ibn Maalik[54] amesema: Nimeswali pamoja na Mtume (s.a.w.w), Abu Bakr, Umar na Uthman wala sikusikia mmoja wao akisoma *Bismillahir Rahmanir Rahim*. Na mfano wa Hadith hii ni Hadith ya Hamiid At-Twawil kutoka kwa Anas[55] amesema: Nilisimama (katika swala) nyuma ya Abu Bakr, Umar na Uthman; wote walikuwa hawasomi *Bismillahir Rahmanir Rahim*.

52 Hivi hivi ameitoa Imam Ar-Razii Hadith hii ya Ibn Mughaffal katika hoja za wenye kukhalifu katika mas-ala haya uk. 106 Juz. 1 ya tafsiri yake. kisha akasema: Anas na Ibn Mughaffal wamehusisha kutokusoma *Bismillahir Rahmanir Rahim* kwa makhalifa watatu tu wala hawakumtaja Ali, na hii inajulisha kwamba Ali alikuwa akisoma *Bismillahir Rahmanir Rahim* kwa jahara.

53 Uk. 97, Juz. 1.

54 Muslim katika *Sahih* yake ameitoa Hadith hii kwa njia mbili kutoka kwa Shuu’bah kutoka kwa Anas katika Mlango wa hoja za wenye kupinga kusoma *Bismillah* kwa sauti.

55 Kufuatana na Hadith aliyoitoa Maalik katika mlango wa Al-a’maal (vitendo) katika kisomo, katika kitabu chake *Al Muwattaa*.

**Jawabu lake:** Wewe umesikia katika hoja zetu kwa Hadith iliyosahihi kutoka kwa Anas ambayo inapingana na hizi Hadith mbili, zingatia tuliyoyatanguliza. Na Imam Ar-Razi ameitia Hadith hii ya Anas katika hoja za wenye kumkhalifu, kisha akasema: Jawabu lake ni kwa njia nyingi: **Ya kwanza**: Amesema Sheikh Abu-Hamid Al-Asfaraini: Zimepokewa riwaya sita kutoka kwa Anas katika mlango huu. Madhehebu ya Hanafi wamepokea kutoka kwake riwaya tatu: (Ya kwanza): Nimeswali nyuma ya Mtume (s.a.w.w) Abu Bakr, Umar na Uthman walikuwa wakifungua swala kwa *Alhamdulillah rabil alamiin*. (Ya pili) wao walikuwa hawataji *bismillahir Rahmanir Rahim*. (Ya tatu) sikumsikia hata mmoja kati yao akisoma *bismillahir Rahmanir Rahim.* Hizi riwaya tatu zinaafikiana na kauli ya madhehebu ya Hanafi.

Akasema (Abu Hamid): Na tatu zingine zinazopingana na hizi. (Ya kwanza): Hadith yake kwamba Muawiya aliacha *Bismillahir Rahmanir Rahim* katika swala. Muhajirina na Answari wakampinga. Na hii inajulisha kwamba kusoma *bismillah* kwa jahara lilikuwa ni jambo lililokuwa limeenea kwao na lisilokuwa na tofauti kati yao. Akasema: (Y**a pili**) Abu Qalaba amepokea kutoka kwa Anas kwamba Mtume (s.a.w.w), Abu Bakr, Umar walikuwa wakisoma kwa jahara *Bismillahir Rahmanir Rahim.*[56] Akasema: (Y**a tatu**) aliulizwa kuhusu kusoma *Bismillahir Rahmanir Rahim* ni kwa jahara au kwa siri? Akajibu: Sijui mas-ala haya. Akasema (Abu Hamid): Kwa sababu hii inabainika kwamba riwaya kutoka kwa Anas katika mas'ala haya zimegongana sana na ni zenye kupingana. Kwa hiyo ni lazima turudi kwenye dalili nyingine zisizokuwa hizi.

Akasema Imam Ar-Razi: Vile vile kuna tuhuma zingine kwamba Ali (a.s.) alikuwa akisoma kwa jahara sana *Bismillah*, na dola iliposhikwa na Banii

56 Katika hoja zetu tumeitia Hadith ya Hamid At-Twawil kutoka kwa Anas aliposema: Niliswali nyuma ya Mtume (s.a.w.w), Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali wote walikuwa wakisoma *Bismillahir Rahmanir Rahim* kwa sauti.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 31



Umayah walifanya bidii sana kuzuia kuisoma kwa jahara ili kupoteza athari za Ali (a.s).[57] Akasema (Ar-Razi): Huenda Anas aliwaogopa (Banii Umayah); kwa sababu hii ndiyo maneno yake yakawa yanagongana.

Akasema (Ar-Razi): Sisi, kwa vyovyote tunapokuwa na shaka katika jambo hatui nayo (shaka hiyo) kunapotokea mgongano baina ya neno la mtu mfano wa Anas na Ibn Mughaffal na kauli ya Ali ibn Abi Twalib (a.s) ambaye alibaki Kwake (Mtume) umri wake wote, kwani kushikamana na kauli ya Ali ni bora.

Akasema: Hili ni jawabu la kukata katika mas-ala haya... mpaka akasema: Na mwenye kumchagua Ali (a.s) kuwa ndio Imam wa dini yake, basi bila shaka atakuwa ameshika mashiko yenye nguvu katika dini yake na nafsi yake... mpaka mwisho wa maneno yake.[58]

**Nasema:** Shukurani kubwa ni za Mwenyezi Mungu ambaye ametuongoza katika (neema) hizi, na hatukuwa ni wenye kuongoka kama asingetuongoza Mwenyezi Mungu.

## KUSOMA KATIKA SWALA

Wanazuoni wa fiqhi wametofautiana juu ya kusoma katika swala, Abu Bakr Al-Aswam, Ismail ibn Aliyah, Sufiyan ibn Uyainah na Husein ibn Swaleh wamesema kwamba kusoma sio wajibu katika swala yoyote bali ni sunna tu.

57 Hii ndio sera yao kumfanyia Amiril Muuminin na watoto wake katika sheria za Mwenyezi Mungu mpaka haki ikachanganyika na batili. Hapana hila wala nguvu isipokuwa ni kwa Mwenyezi Mungu Aliye wa Juu na Aliye Mtukufu.

58 Mrudie (Ar-Razi) uk. 106 na mwisho wa uk. 107 wa Juz. 1 katika tafsiri yake *Al-Kabiir*.

Hii ni rai iliyokiuka; ni kutoka nje ya dalili na ni kuvunja *ijmaa* (kongamano) ya umma. Wao wametoa hoja kwa riwaya aliyoipokea Abuu Salma na Muhammad ibn Ali kutoka kwa Umar ibn Khatwab kwamba aliswali Magharibi bila kusoma chochote katika swala hiyo, na akaulizwa kuhusu jambo hilo, akasema: Je rukuu na sijda zilikuwa vipi? Wakamjibu: Zilikuwa nzuri. Akasema: Basi hakuna tatizo lolote.

**Jawabu**: Hii ni rai yake (Umar) kwa sababu kitendo hiki hakukitegemeza kwa Mtume na huenda yeye ni miongoni mwa wenye kuona kuwa kutosoma katika swala kwa kusahau hakubatilishi swala. Na Mwenyezi Mungu ni mjuzi zaidi

Hasan Al Basri na wengineo wamesema kwamba kusoma ni faradhi katika rakaa moja tu katika swala. Pia rai hii ni kama iliyotangulia katika kukiuka na kuvunja *ijmaa* (kongamano) ya Waislamu.

Wao wametoa hoja kwa neno la Mtume (s.a.w.w): “Hakuna swala ila ni kwa *Suratul Fatiha*,” kwa kushika hoja kuwa *istithnai* (kuvua) baada ya kukanusha ni kuthibitisha, na kukipatikana kusoma *Surat Fatiha* japo ni mara moja tu inalazimika kusema kuwa swala hiyo ni sahihi kwa hukumu ya *istithnai*.

**Jawabu**: Hadith hii - inavyofahamika - haiangalii hali ya swala inapokuwa pamoja na *Surat Fatiha* - na wakati huo - haihukumu katika hali hiyo ya swala kwa kuikubali au kuikanusha, bali (Hadith hii) inaielezea swala pindi inapokuwa haina *Surat Fatiha* na inaihukumu swala hiyo - wakati huo - kuwa sio swala. Hii ni kama neno la Mtume (s.a.w.w): “Hapana swala yoyote isipokuwa ni kwa twahara.” Hii ni kuonyesha umuhimu wa *Surat Fatiha* kuwa ni sehemu katika swala na umuhimu wa twahara kuwa ni sharti yake. Mifano ya maneno haya katika mazungumzo ni mengi sana. Je, huoni lau mtu atasema kuwa hakuna *sikinjabin* isipokuwa ni kwa siki, kwa mfano. Hakuna yeyote atakayefahamu kutokana na maneno haya, kwamba kiasi chochote cha siki - japo ni tone moja au chini yake - kuwa kinatosha au hakitoshi, bali kinacho fahamika ni kwamba *sikinjabin* ni

mchanganyiko maalum, na siki ni miongoni mwa viungo vyake muhimu, kiasi ambacho ikikosekana siki basi hakuna *sikinjabin*.

Pia *istidlali* (hoja) yao kwa Hadith hii ingelitimia, kama walivyodai, ingekuwa ni hoja ya kutokulazimu kitu chochote katika vitendo vya swala au visomo pindi tu kukipatikana kusoma *Surat Fatiha*, kama ilivyo wazi kwa mwenye kuzingatia.

Imam Abuu Hanifa na wafuasi wake wamesema: Kusoma *Surat Fatiha* khaswa sio lazima katika swala yoyote ile, bali lililo lazima katika swala ni kusoma chochote katika Qur'ani. Kwa hiyo Abuu Hanifa anatosheka na kusoma aya moja yoyote katika Qur'ani japo aya hiyo ni neno moja tu, kwa mfano *mud-hamataan* (za kijani kibichi) lakini wafuasi wake wawili Abuu Yusuf na Muhammad ibn Hasan Al-Shaibani wametosheka kwa kusoma aya tatu fupi; kwa mfano: *thumma nadhara, thumma a'basa wabasara, thumma adbara wastakbara* (Kisha akatazama, Kisha akakunja kipaji na akanuna, Kisha akaipa kisogo haki na akatakabari) au aya moja inayolingana na aya tatu fupi au zaidi ya aya tatu. Na kwa rai hii ndivyo wanavyofanya wafuasi wa madhehebu ya Hanafi.**[59]**

Abuu Hanifa amejawizisha kutarjumi kinachosomwa katika swala kwa lugha yoyote isiyokuwa ya kiarabu, hata kama ni kwa mwenye kujua Kiarabu vizuri;**[60]** na akatosheka kusema - badala ya *Surat Fatiha* na sura nyingine - kwa kusema: *doblak sabzi* tarjumi ya *mud-hamatan* kwa

59 Rudia fiqihi yao, na inakutosha *Ghunyat Mutamallil Kabiir* na *As-Swaghiir*. Hivi ni vitabu vilivyoenea kama vitabu vyao vinavyotumiwa na watu wote.

60 Hili ni jambo *mutawaatir* (lililoenea) kutoka kwake. Miongoni mwa walionakili kutoka kwake ni Fakhru-Din Ar-Razi mwanzo wa uk. 108 Juz. 1 katika tafsiri yake *Al-Kabiir*. Kisha akasema: "Jua kwamba madhehebu ya Abuu Hanifa katika mas-ala haya yako mbali sana (na ukweli). Kwa sababu hii, Alfaqihi Abuu Laith As-Samarqandi na Alkadhi Abuu Zaid Addabusi wamesema wazi (kwamba) rai hii iachwe.

Kifursi. Lakini wafuasi wake wawili wamejawizisha kutarjumi kwa mwenye kushindwa kusoma kwa Kiarabu sio kwa anayeweza. Na madhehebu ya Hanafi yanaendana na rai hii. Kwao kisomo ni faradhi katika rakaa mbili za mwanzo za kila swala yenye rakaa mbili kama vile swala ya Ijumaa, Alfajiri na Adhuhuri, Alasiri na Isha za msafiri. Ama swala zisizokuwa za rakaa mbilimbili - kama swala ya Magharibi, Isha, Adhuhuri na Alasiri za mtu ambaye yuko mjini kwake - basi ni faradhi kwake kusoma katika rakaa mbili zozote katika swala. Mwenye kuswali atachagua; akitaka atasoma katika rakaa mbili za mwanzo au mbili za mwisho au ya kwanza na ya tatu au ya kwanza na ya nne au ya pili na ya tatu au ya pili na ya nne. Kwa mfano, akisoma katika mbili za mwanzo basi katika mbili za mwisho yeye mwenyewe atachagua, akitaka atasoma au ataleta tasbihi au atanyamaza kiasi cha muda wa kuleta tasbihi. Haya ndiyo madhehebu yao, na yaliyoenea katika fiqhi yao.

Wametoa hoja ya kutosheka kusoma chochote katika swala kwa Hadith ya Abuu Hurairah iliyoko katika *Sahihi Bukhari* na *Sahihi Muslim* **[61]** aliposema: Mtume (s.a.w.w) aliingia msikitini, na baada yake akaingia mtu mmoja akaswali, kisha akaja akamsalimia Mtume. Baada ya kumjibu salamu akamwambia: Rudia kuswali kwani hukuswali. Akarudia na akaswali kama alivyoswali mara ya kwanza. Kisha akaja kwa Mtume akamtolea salamu. Mtume akamwambia, *wa alaikum salam* rudia kuswali kwani hukuswali.... Akafanya hivyo hivyo mara tatu, kisha yule mtu akasema: Naapa kwa aliyekutuma kwa haki. Siwezi kuswali vizuri zaidi ya hivi. Basi nifundishe. Mtume (s.a.w.w) akasema: Pindi unaposimama kuswali, piga

---

61 Vilevile wametoa hoja kwa Hadith iliyopokewa na Muslim katika Sahihi yake kutoka kwa Abuu Hurairah amesema: Mtume (s.a.w.w) amesema: "Hakuna swala isipokuwa ni kwa kusoma" kwani ametaja kusoma bila ya kutaja kinachosomwa. Haya ni madai yao.

**Jawabu**: Lau Hadith hii ingekuwa sahihi ingelazimu kuitafsiri kwa Hadith ya Mtume aliposema hakuna swala kwa yule ambaye hakusoma Surat Fatiha. Hapana shaka kwamba maneno ambayo ni mutlaq (ya kukata) hutafsiriwa kwa ambayo ni muqayad (yenye sharti). Hii ni kwa ijmaa na kwa neno moja.

*takbir*. Kisha soma kinacho *tayasar* kwako (kuwia wepesi) katika Qur'ani. Kisha rukuu mpaka utulie katika rukuu. Kisha inuka mpaka unyooke kwa kusimama. Kisha usujudu mpaka utulie katika sijda. Kisha inuka mpaka utulie kwa kuketi. Kisha fanya hivi hivi katika swala yako yote.

Sehemu muhimu katika maneno ya Mtume ni "*kisha soma kinacho kuwia wepesi katika Qur'ani*" kwa dhahiri ya madai yao.

**Jawabu**: Kwa hakika Abuu Huraira ni katika watu ambao Hadith zao hatuzipi uzito wowote, kama tulivyobainisha kwa upana na tukasimamisha hoja za kukata, za kiakili na za kunakili, katika kitabu maalum tulichokipwekesha kwa ajili yake. Mwenye kutaka uchunguzi wa uhakika ni akirudie kitabu hicho.

Tena Hadith yake hii huenda ikawa haijuzu kuwa imetoka kwa Mtume (s.a.w.w) kwa sababu tukio hilo limetuka wakati ambapo ni lazima kubainishwa. Na tumeiangalia kwa mazingatio tukaipata haiko katika kubainisha, na hilo halilingani na tabia za mitume (a.s) kwa Hadith hii kutokuwa na mambo mengi ambayo umma umeafikiana kuwa ni lazima katika swala: kama nia, kukaa tashahudi ya mwisho, kupanga nguzo za swala, kusoma tashahudi ya mwisho, kumswalia Bwana Mtume (s.a.w.w), kutoa salamu na nguzo zingine. Pia Mtume kumwacha yule mtu kurudiarudia kuswali mara tatu swala batili ni jambo lisilolingana na tabia ya Mtume (s.a.w.w). Na huenda ni jambo lisilofaa kwake (s.a.w.w).

Pia Abii Daudi amekitoa kisa hiki katika *Sunan* yake katika Mlango wa Swala ya Mtu Asiyenyoosha Mgongo Wake Katika Rukuu na Sijda, kwa *isnadi* (wapokezi) mpaka kwa Rafaa'h ibn Rafi'i[62] Al-Answari, naye ni

62 Alihudhuria Vita vya Badr, Uhud na vita vingine pamoja na Mtume (s.a.w.w), na alikuwa pamoja na ndugu zake wawili katika Badr nao ni Khalaad na Maalik ambao ni watoto wa Rafi'i. Na huyu Rafaa'h alihudhuria Vita vya Jamal na Swifiin pamoja na Amirul muuminin (Ali) na alikuwa ni mtiifu wake mkubwa wa kumnusuru kwa maneno na vitendo; yote haya yanajulikana kutoka katika tarjuma (maelezo) yake yaliyoelezwa katika *Al-Iswaba* na vitabu vingine vilivyoeleza hali za maswahaba.

miongoni mwa watu wa Badr, na katika Hadith hiyo anasema: Mtume alimwambia mtu ambaye alikuwa haswali vizuri swala yake: Unaposimama kuswali na ukaelekea kibla, piga *takbir*, kisha soma *alhamdu* na chochote unachotaka kusoma (katika Qur’ani).

Vile vile Ahmad ibn Hambal na Ibn Habaan wametoa kisa hiki kwa *isnadi* yao mpaka kwa Rafaa’h ibn Rafi’i, na katika kisa hicho imesemwa kwamba hakika Mtume (s.a.w.w) alisema kumwambia yule mtu mwenye kuharibu swala yake: ‘Kisha soma *Alhamdu*, na kisha soma chochote unachotaka (katika Qur’ani)... Mpaka mwisho wa Hadith.[63]

Miongoni mwa mambo mashuhuri ni kwamba Abuu Hurairah ni katika wale ambao hawawezi kulinganishwa na Rafaa’h, si kwa maneno wala kwa kazi. Kwa hiyo bila shaka Hadith yake (Rafaa’h) hutangulizwa juu ya Hadith ya Abuu Hurairah pindi zinapopingana. Kwa sababu hii utampata Al-Qastwalaani katika *Fat-hul Bari* ameawili yale yaliyokuwemo katika Hadith ya Abuu Hurairah kwa kuyachukua yaliyokuja katika Hadith ya Rafaa’h. Mwenye kufuatilia maneno ya *salaf* (waliotangulia) na *khalaf* (waliofuatia) kuhusu yaliyomo katika Hadith ya Abuu Hurairah aliposema: Soma kinachokuwia wepesi katika Qur’ani. Wote (isipokuwa madhehebu ya Hanaf) utawapata baadhi yao wameipinga na kuifanya hii ni Hadith dhaifu,[64] na wengine wameawili maneno yake.[65] Ukitaka angalia maneno

63 Haya utayapata mwisho wa mlango wa ‘Lazima ya Imamu na Maamuma Kusoma Katika Swala Yote’ uk. 441 Juz. 2 ya *Irshaad Saari fi Sahihil Bukhari* alipokuwa akisherehe Hadith hii ya Abuu Hurairah, akinukuu kutoka kwa Abii Daud, Ahmad na Ibn Habaan.

64 Kama baadhi ya Mu’tazila na Shia

65 Kama wanazuoni wa jamhuri (sunni) wasiokuwa wa Kihanafi.

yao kuhusu Hadith hii ya Abuu Huraira katika sherehe zote za sahihi mbili (*Bukhari* na *Muslim*).[66]

Vile vile Abuu Huraira mwenyewe ameipinga hii Hadith yake kwa Hadith yake nyingine iliyo sahihi kutoka kwake. Amesema: Nimemsikia Mtume (s.a.w.w) akisema: “Swala ambayo haikusomwa *Alhamdu* ndani yake, haitoshelezi.”[67] Na amesema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) aliniamrisha nitoke na ninadi Madina kwamba hakuna swala isipokuwa ni kwa kusoma japo *Surat Fatiha* na zaidi.[68]

Na amesema: Nimemsikia Mtume (s.a.w.w) akisema: Mwenye kuswali swala ambayo haikusomwa Alhamdu ndani yake basi swala hiyo ni pun-

66 Imam An-Nawawi amesema kuhusu Hadith hii ya Abuu Hurairah katika sherehe ya *Muslim* katika Mlango wa Lazima ya Kusoma Fatihatil Kitab (alhamdu): Ama neno lake (Abuu Hurairah) “Soma kinacho kuwia wepesi katika Qur’ani” maana yake ni Surat Fatiha kwa sababu ndiyo nyepesi, au kile kilicho zaidi ya Surat Fatiha kwa wepesi au kwa mwenye kushindwa kusoma Surat Fatiha. **Mwisho wa kunukuu**.

Amesema Imam Al-Sindi alipokuwa akitia taaliki (maelezo) Hadith hii ya Abuu Hurairah katika *Sahihi Bukhari*, na hapa namnukuu: “Neno lake (Mtume) soma kinacho kuwia wepesi, kana kwamba amemwambia hilo kulingana na kuwa kilicho chepesi namna hiyo ni Fatiha. (Akasema) kwamba imepokewa katika baadhi ya riwaya kuwa (Mtume) alimuainishia Fatiha. **Mwisho wa kunukuu**.

67 Abu Bakr ibn Khuzeima ameitaja katika *Sahih* yake kwa sanadi iliyo sahihi. Pia Abuu Hatim ibn Habaan ameipokea. Na Imam An-Nawawi ameinakili kutoka kwa wote wawili na akasema wazi katika Mlango wa Lazima ya Kusoma Fatiha katika sherehe yake ya *Sahih Muslim* kuwa ni sahihi.

68 Abuu Daud ameitaja Hadith hii katika *Sunan* yake katika Mlango wa Kuacha Kusoma Katika Swala, na huko ametaja Hadith nyingine kutoka kwa Abuu Hurairah kwa njia nyingine akasema: Mtume aliniamrisha ninadi kuwa: Hapana swala isipokuwa ni kwa kusoma Surat Fatiha na zaidi.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 38



gufu, swala hiyo ni pungufu, swala hiyo ni pungufu.[69]

Jambo lililobaki ni tujiulize: Kwa nini wanafiqhi wa madhehebu ya Hanafi wameshika dhahiri ya kauli ya Hadith ya Abuu Hurairah iliyosema "soma kinacho kuwia wepesi katika Qur'ani" bila ya kuchukua nususi zilizo wazi kwamba ni lazima kujituliza katika kusimama, kukaa, kurukuu na kusujudu. Na zile walizozichukua zinapingana na nususi zilizo wazi na zinazokhalifu jamhuri ya Waislamu (umoja wa waislamu), pia zile ambazo hawakuzichukua zimetiliwa nguvu na Hadith sahihi na ndizo zilizochukuliwa na jamhuri.

Madhehebu ya Hanafi huenda wametoa hoja katika kutilia nguvu rai yao katika mas'ala haya kwa neno la Mwenyezi Mungu: "Someni kinachowawia wepesi katika Qur'ani."

**Jawabu**: Aya hii haizungumzii kabisa haya tuliyonayo ya kusoma katika swala. Bali fuo lake linashuhudilia haya katika *Surat Al-Muzamil*. Mwenye kutaka airudie na azingatie yale yaliyosemwa na wafasiri katika kutafsiri aya hiyo, uhakika utamfunukia wazi.

Madhehebu ya Hanafi wametoa hoja ya kujuzu kutarjumi Qur'ani inayosomwa katika swala kwa lugha yoyote isiyokuwa ya Kiarabu kwa hoja nyingi:

**Ya kwanza:** Ibn Mas'ud aliwasomea baadhi ya Waajemi "*Inna shajarataz zaquumi twaamal athiimi*." Yule mwajemi akawa anasoma: "*Twaamal yatiim*" Akasema (Ibn Mas'ud) kumwambia yule mwajemi sema: "*Twaamal faajir*." Kisha akasema: "Sio makosa katika Qur'ani mtu kusoma *alhakim* mahala pa *al-alim*, bali makosa ni mtu kuweka aya ya rahma mahala pa aya ya adhabu.'"

69 Abuu Daud ameitaja katika mlango uliotangulia hapo juu na Muslim ameitaja katika *Sahih* yake katika Mlango wa Lazima ya Kusoma Surat Fatiha Katika Kila Rakaa kutoka kwa Abuu Hurairah kwa njia nyingine.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 39



**Jawabu:** Hadith hii iko mbali na haya tuliyonayo; hakuna dalili yoyote katika haya. Tena lau maneno haya yangekuwa sahihi basi itakuwa ni rai ya Ibn Mas'ud, inamfaa yeye mwenyewe wala haiwi ni hoja (dalili).

**Ya pili:** Ni neno la Mwenyezi Mungu:

﴿ وَإِنَّهُۥ لَفِى زُبُرِ ٱلْأَوَّلِينَ ﴿١٩٦﴾ ﴾

**"Na haya (yaliyomo katika Qur'ani) yamo katika vitabu vya kale (walivyoteremshiwa mitume wa zamani)" (26:196).**

Pia neno lake:

﴿ إِنَّ هَٰذَا لَفِى ٱلصُّحُفِ ٱلْأُولَىٰ ﴿١٨﴾ صُحُفِ إِبْرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ ﴿١٩﴾ ﴾

**"Hakika haya (yaliyomo katika Qur'ani) yamo katika vitabu vilivyotangulia, vitabu vya Ibrahim na Musa." (87:18-19).**

Namna ya kutoa dalili kwa aya hizi ni kwamba umma (wa Kiislamu) wameafikiana kuwa Qur'ani haikuja kwa matamshi ya Kiarabu katika vitabu vilivyotangulia wala katika Suhufi za Ibrahim na Musa, bali (Qur'ani) ilikuwepo katika hivyo vitabu kwa maana yake na kwa matamko ya Kiebrania na Kisiryan.

**Jawabu:** Hoja hii ni kama iliyotangulia katika kutokujulisha haya madai. Bali iko mbali, mbali sana.

**Ya tatu:** Mwenyezi Mungu amesema: **"(Sema, ewe Muhammad) nimefunuliwa hii Qur'ani ili nikuonyeni kwayo."** Wasiokuwa Waarabu hawafahamu matamko ya Kiarabu mpaka waelezwe maana yake kwa lugha zao, na hayo maonyo huwa kwa lugha hizo.

**Jawabu:** Hii inafaa kuwa ni dalili ya kujuzu kuitafsiri Qur'ani kwa lugha zao (wasiokuwa Waarabu) ili wachukue hukumu, adabu, maamrisho na

makatazo yake (Qur’ani); na hili ni jambo moja. Ama kuzungumza kilugha katika swala ambayo ameamrishwa kusoma Qur’ani ndani yake, hilo ni jambo lingine. Ni Mwarabu gani au asiyekuwa Mwaarabu gani ambaye akiambiwa kusoma *Surat Fatiha* hafahamu kuwa ni kuisoma kama ilivyoandikwa katika misahafu? Na ni nani mwenye utamu (wa kuelewa) hakubali kuepusha neno la kusoma *Surat Fatiha* na kusoma Qur’ani kwa lugha ya kiajemi au lugha nyingine yoyote isiyokuwa ya Kiarabu iwe ya Magharibi au ya Mashariki?

Imam Ar-Razi katika kuzipinga hizi hoja - alipokuwa akinukuu kutoka kwa madhehebu ya Hanafi - ana maneno, yarudie. Mimi namshuku Imam Abuu Hanifa kuwa ameleta mgongano mkubwa sana katika huku kutoa kwake dalili katika kuchimbua (kutafuta) hukumu, na hii ni kwa kuwa yeye anategemea sana *qiyas* (kufananisha mambo) na *istihsani* (kuhukumu kulingana na yanayompendeza) katika kuchimbua hukumu za sheria. Kwa namna hii alikuja huyu mtu kana kwamba yeye alipendezwa kwamba wasiokuwa Waarabu watarjumi kisomo chao katika swala kwa lugha zao, kwa sababu aliliona hilo liko karibu sana na fahamu zao kukifahamu kisomo na kunatarajiwa sana kuwa watanyenyekea zaidi katika kisomo. Hapa kana kwamba yeye alifanya *qiyas* (kufananisha) kisomo cha wasiokuwa Waarabu kwa lugha zao kwa (kufananisha) na kusikiliza kwao mawaidha au masomo kwa lugha zao. Hii ni nadharia ya Ataaturik katika swala, nadharia ambayo hakuichukua kutoka kwa Abuu Hanifa, bali ni vile ambavyo mawazo yake yalimtuma. Kilichomsaidia Ataaturik katika nadharia hii ni kuwa yeye alikuwa hathamini hoja (dalili) za sheria, tena alikuwa hazijui wala hakutaka kuzijua katika yanayompendeza ili atengeze nadharia yake. Lau katika dalili za sheria kungekuwa na chenye kusaidia kuonyesha kuwa yajuzu (inafaa) kutegemea *istihsani*, basi hili walililoliona lingekuwa na njia ya kukubalika. Lakini ni ukubwa ulioje wa kosa alilolifanya!

Imam Shaafi, Malik, Ahmad na wengine wamesema kuwa ni faradhi (wajibu) kusoma *Surat Fatiha* kwa lugha ya Kiarabu katika rakaa zote za swala za faradhi na za sunna. Dalili (hoja) yao ni Hadith ya Abuu Hurairah

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 41



inayozungumzia kisa cha mtu wa mashamba ambaye alikuwa hajui kuswali vizuri. Pale Mtume (s.a.w.w) alipomwambia, alipomfundisha kuswali, akamwamrisha asome, kisha akamwambia "fanya hivi hivi katika swala yako yote."[70] Umekwishajua maoni yetu kuhusu Hadith hii tuliposema kuwa sisi hatumzingatii Abuu Hurairah...

Ama Imamiya (Shia) - kwa kufuata Maimamu wa kizazi (cha Mtume) kilicho takaswa - kusoma *Surat Fatiha* kwa Kiarabu kilicho sahihi ni faradhi katika rakaa mbili za mwanzo katika kila swala za faradhi na za sunna.[71] Kwa anayeswali peke yake na kwa imam. Ama maamuma yeye kisomo

70 Imam An-Nawawi ambaye ni mfuasi wa madhehebu ya Shaafi, amesema katika kitabu chake, Sherehe ya *Sahihi Muslim* katika Mlango wa Lazima ya Kusoma Fatiha: "Jamhuri ya wanazuoni waliotangulia na waliofuatia wamesema: Ni lazima kusoma Surat Fatiha katika kila rakaa, kwa sababu Mtume (s.a.w.w) alisema kumwambia yule mtu wa mashamba ambaye alikuwa hajui kuswali vizuri: 'Fanya hivi hivi katika swala yako yote." Naseama: Huenda wewe unajua kwamba An-Nawawi, Shaafi na wangine wenye kusema kuwa ni lazima kusoma Surat Fatiha katika kila rakaa za swala hawakuizingatia Hadith ya Abuu Hurairah isipokuwa ni kutafsiri maneno yake yanayosema "Soma kinachokuwia wepesi" kwamba ina husika na Surat Fatiha.

71 Ni lazima kwetu katika rakaa mbili za mwanzo za swala tano za faradhi kusoma sura kamili baada ya Surat Fatiha kwa sababu hilo limethubutu kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) katika Hadith ya Abuu Qatad. Na Bukhari ameitaja katika *Sahihi* yake; pia wengine wameitaja. Na inajuzu kwetu kuacha sura (baada ya Surat Fatiha) katika baadhi ya hali, na huwenda ikawa ni lazima pale inapokuwa dhiki ya wakati au dharura nyingine miongoni mwa dharura. Ama swala za sunna ni lazima kusoma Surat Fatiha peke yake. Na kusema ni lazima kuisoma (Surat Fatiha) katika swala ni kusema kwa hilo ni sharti ya kuswihi (kukubaliwa) swala.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 42



chake huchukuliwa na imam wake.[72] Ama rakaa mbili za mwisho, ni faradhi katika hizo ima kusoma *Surat Fatiha* au kuleta tasbihi – kufuatana na uchaguzi wake - wala imam katika hizo rakaa mbili hamchukulii maamuma wake kisomo wala tasbihi.

Na hoja zetu katika haya yote ni nusus (Hadith) za Maimamu wetu. Wao (a.s) ndio wenzi wa Kitabu (Qur'ani) kuwa kisomo cha Mtume (s.a.w.w) katika kila rakaa mbili za mwanzo zilikuwa ni *Surat Fatiha* na sura kamili. Hili limethubutu katika *swihahi* na *masaaniid* (vitabu vya Hadith) vyote kutokana na Hadith ya Abuu Qataada Al-Harth ibn Rabi'i na wengineo.

72 Kufuatana na neno la Mtume (s.a.w.w): "Kila mwenye imam kisomo cha imam ndiyo kisomo chake." Hadith hii imepokewa na jamhuri kwa njia nyingi; utaipata katika kitabu *Al-Fiqhi alal Madhahib al-Arbaa* (fiqhi ya madhehebu manne) katika kuzungumzia kusoma Surat Fatiha. huko utapata kauli ya kumzuia maamuma kusoma iliyopokewa kutoka kwa Amiirul-Muuminiin (Ali) na Abaadila (wakina Abdallah) miongoni mwa maswahaba wakubwa themanini. Bali utapata kauli inayosema kuwa swala ni batili pindi maamuma akisoma nyuma ya imam. Haya pia yamepokewa kutoka kwa idadi kubwa nyingine ya maswahaba. Na lililo ihtiyat (kutoka shakani) kwetu, bali ndilo lenye nguvu, ni maamuma kuacha kusoma katika rakaa mbili za mwanzo za swala zenye kusomwa kwa siri; vile vile katika rakaa mbili za mwanzo zenye kusomwa kwa sauti anaposikia sauti ya imam wake japo ni kwa mnong'ono. Na huku ni kutekeleza neno la Mwenyezi Mungu: "Pindi ikisomwa Qur'ani isikilizeni na mnyamaze huenda nyinyi mtarehemiwa." (7:204). Lakini kama hasikii japo mnong'ono basi inajuzu kwa maamuma kusoma, bali ni sunna kwake kusoma.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 43



Na asili ni kwamba chochote anachokifanya (Mtume) katika swala yake huwa ni faradhi[73] kufuatana na neno lake (s.a.w.w): "Swalini kama mlivyoniona mimi nikiswali." Na kama imethubutu kutoka kwake (s.a.w.w) kuwa alikisoma *Surat Fatiha* katika rakaa mbili za mwisho, pia imethubutu kuwa alikileta dhikri (tasbihi) katika hizo rakaa mbili za mwisho. Hizo tasbihi ni kusema: *subhana llah walhamdu lillah walaa ilaha illa llahu wallahu akbar*. Hii imepokewa kutoka kwa Maimamu ambao ni kizazi chake (s.a.w.w) kilichotwaharika, na inashuhudia hayo Hadith ya Sa'd ibn Abii Waqaas iliyoko katika *Sahihi Bukhari* na vingine miongoni mwa vitabu vya Hadith pale watu wa mji wa Kufa walipolalamika kwa Umar wakasema kuwa yeye (Sa'd) hajui kuswali vizuri. Sa'd akasema: *wallahi*, nilikuwa nawaswalisha swala ya Mtume. Sikupunguza chochote, bali nilikirefusha rakaa mbili za mwanzo kwa kusoma *Surat Fatiha* na sura, na nilikifupisha rakaa mbili za mwisho; yaani alifanya haraka katika rakaa mbili za mwisho kwa kuleta tasbihi au kusoma *Surat Fatiha* peke yake (bila kuongeza), na Mwenyezi Mungu peke Yake ndiye Mjuzi.

## TAKBIRA YA KUHIRIMIA SWALA

Wameaafikiana Imamiya (Mashia) wote - kwa kufuata Maimamu wa kizazi cha Mtume kilichotakasika - kuwa takbira ya kuhirimia swala ni nguzo katika kila swala ya faradhi na ya sunna. Swala haiwezi kupatikana bila hiyo. Namna yake ni kusema: *Allahu Akbar* peke yake (haina badali). Lau mwenye kuswali akaanza swala yake kwa kumsabihi Mwenyezi Mungu, au kuleta tahlili Zake, au kusema *Allahu Kabiir* au *Allahul Akbar* au *Allahu A'dham* au mfano wa hizi, basi swala yake haiswihi (haikubaliki), licha ya kutafsiri *Allahu Akbar* kwa lugha yoyote isiyokuwa ya Kiarabu. Inatosha kuwa ni faradhi kwamba Mtume (s.a.w.w) hakuanza swala katika swala zake zote isipokuwa ni kwa kusema: *Allahu Akbar*, na

73 Kama alivyoeleza wazi Imam Al-Sindi katika kuelezea Hadith ya Sa'd iliyoko katika *Sahihi Bukhari* ambayo tumeitaja hapo juu (kwenye kitabu).

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 44



umekwishajua kabla kidogo kuwa chochote anachofanya Mtume (s.a.w.w) katika swala yake ni faradhi, na hii ni kufuatana na maneno yake aliposema: "Swalini kama mlivyoniona mimi nikiswali." Lazima ya hiyo imethubutu katika Qur'ani, Sunna (Hadith) na *Ijmaa* (kongamano) ya umma.

Mwenyezi Mungu amesema: **"Na Mola wako mtukuze."** Kuna *Ijmaa* kuwa kinachokusudiwa hapa ni lazima ya takbira ya kuhirimia kwa sababu tamko lake linaamrisha, na maana ya kuamrisha ni lazima, na isiyokuwa takbira siyo lazima kwa *Ijmaa*. Na Mtume (s.a.w.w) amesema: "Ufunguo wa swala ni kujitwaharisha, kuhirimia kwake ni takbira na kufunguka (kutoka) kwake ni salaam. Hadith hii imepokewa na Abuu Daud katika *Sunan* yake.

Madhehebu ya Hanafi wamesema kuwa kuhirimia siyo nguzo katika swala, bali kuhirimia kumeungana na kusimama ambako ndiyo nguzo Kwa sababu hiyo ni lazima wakati wa kuhirimia kuelekea Kibla, kujisitiri na kuwa na twahara; na lazima hiyo siyo kwa ajili ya kuhirimia, bali ni kwa sababu kuhirimia kumeungana na nguzo (kusimama). Na wanasema: siyo sharti katika kutumia lugha ya Kiarabu katika kuhirimia, inatosha kuitafsiri kwa lugha yoyote aitakayo mwenye kuswali – sawa iwe anaimudu lugha ya Kiarabu au haimudu - kwao swala inakubalika kusema, kwa mfano, *khuda-buzrug* (Mwenyezi Mungu ni Mkubwa kwa lugha ya Kiajemi) badala ya *Allahu Akbar*.

Wamesema kuhirimia inafaa hata kwa kuleta *tasbihi* au tahlili au kwa jina lolote katika majina ya Mwenyezi Mungu bila ya kuzidisha chochote, mfano aanze swala kwa kusema *Allahu* au *Ar-Rahman* au mfano wake miongoni mwa majina matukufu ya Mwenyezi Mungu bila ya kuzidisha chochote; lakini ni karaha. Haya ndio madhehebu yao wala hawakutofautiana katika kauli hiyo; hoja yao ni *istihsan* (kupendezwa) kama ulivyosikia. Na majibu yake hapa ni yale yale kule. Na Mwenyezi Mungu ndiyo mwenye kuafikisha la usawa.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 45



# MSAFIRI KUPUNGUZA SWALA NA KUTOKU-FUNGA SAUMU SHARIA YA KUPUNGUZA SWALA

Swala za rakaa nne hupunguzwa safarini na kuwa rakaa mbili, ni sawa katika safari hiyo kuwe na hofu au amani. Hii ni *Ijmaa* (kongamano) ya umma kwa kauli moja. Mwenyezi Mungu amesema: “Na mnaposafiri katika ardhi si makosa kwenu kupunguza swala iwapo mtaogopa fitina za wale waliokufuru.”

Amepokewa Ya’ala ibn Umayah, amesema nilimuuliza Umar ibn Khattab kwamba (aya inasema) “Na mnaposafiri katika ardhi si makosa kwenu kupunguza swala iwapo mtaogopa fitina za wale waliokufuru” lakini sasa watu wako kwenye amani! Akajibu (Umar): Niliona ajabu kama ulivyoona wewe, nikamuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), akasema: “Hiyo ni swadaka aliyoitoa Mwenyezi Mungu kuwapa nyinyi. Kwa hiyo ikubalini swadaka Yake.” Hadith hii ameitaja Muslim katika *Sahihi* yake.

Kutokana na Ibn Umar, katika Hadith aliyoitoa Muslim pia katika *Sahihi* yake, amesema: “Nilikuwa nikifuatana na Mtume (s.a.w.w) katika safari zake. Yeye hakuzidisha zaidi ya rakaa mbili mpaka Mwenyezi Mungu akamfisha. Nimeishi pamoja na Abu Bakr nae hakuzidisha zaidi ya rakaa mbili mpaka Mwenyezi Mungu akamfisha. Nikaishi pamoja na Umar nae hakuzidisha zaidi ya rakaa mbili mpaka Mwenyezi Mungu akamfisha. Na nikaishi pamoja na Uthmani, nae hakuzidisha zaidi ya rakaa mbili mpaka Mwenyezi Mungu akamfisha.” Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ ﴿٢١﴾ ﴾

**“Hakika mjumbe wa Mwenyezi Mungu (Mtume) kwenu ni ruwaza mwema”(33:21).**

Kutokana na Anas ibn Maalik katika Hadith iliyopokewa na Mashekhe wawili katika *Sahihi* zao amesema (Anas): Tulitoka Madina kwenda Makka pamoja na Mtume (s.a.w.w) akawa anaswali rakaa mbili mbili mpaka tukarudi Madina.

Kutokana na Ibn Abbas, katika Hadith aliyoipokea Bukhari katika *Sahihi* yake, amesema (Ibn Abbas): “Mtume (s.a.w.w) alibaki Makka siku kumi na huku akipunguza swala...” (mpaka mwisho wa Hadith).

**Nasema:** Mtume alipunguza swala na kubaki kwake Makka siku kumi na tisa kwa sababu hakuwa na nia ya kubaki Makka siku hizo zote.

Imethubutu kutoka kwa Bwana Mtume (s.a.w.w) kuwa alikuwa akiwaswalisha watu wa Makka baada ya hijra, akawa anatoa salam katika swala za rakaa nne nne mwisho wa rakaa mbili za mwanzo, tayari alikuwa ametangulia kuwaambia watu (wa Makka) watimize swala zao rakaa nne na huku akiwaeleza udhuru wake yeye na watu aliokuja nao kuwa wao ni watu wa safari.

Amepokea ibn Abii Shaibah kwa *sanad* (mfululizo wa mapokezi) yake mpaka kwa Mtume (s.a.w.w) amesema: “Wabora wa umma wangu ni wale walioshuhudilia kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni *Allah*, na hakika ya Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na wale ambao pindi wakifanya mema wanafurahi, na wakifanya maovu hutaka maghufira, na wakisafiri hupunguza swala.

Na kutokana na Anas katika Hadith aliyoipokea Muslim kwa njia mbili katika *Sahihi* yake, amesema (Anas): “Nimeswali pamoja na Mtume (s.a.w.w.) swala ya Adhuhuri tukiwa Madina rakaa nne, na nimeswali pamoja naye swala ya Alasiri tukiwa Dhul-Huleifa – safarini - rakaa mbili.

Na kuna Hadith nyingi sahihi ambazo zinasema wazi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka sheria ya kupunguza swala safarini.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 47



## SHERIA YA KUTOKUFUNGA SAFARINI

Hakuna shaka kwamba Mwenyezi Mungu ameweka sharia ya kutokufunga saumu katika mwezi wa Ramadhani kwa kila msafiri anayesafiri safari ya kupunguza swala. Kwa kiasi hiki (kilichotangulia) umma wa Kiislamu umeafikina, na Qur’ani na Hadith zinathibitisha hivyo kwa uwazi. Mwenyezi Mungu amesema:

﴿ شَهْرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِىٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلْقُرْءَانُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٍ مِّنَ ٱلْهُدَىٰ وَٱلْفُرْقَانِ
فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۖ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ
يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ ٱلْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا۟ ٱلْعِدَّةَ ﴿١٨٥﴾ ﴾

**“(Huo) ni mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika mwezi huo Qur’ani ili iwe ni uongofu kwa watu, ubainifu wa uongofu na upambanuzi. Atakayekuwa mjini kwake katika mwezi huu afunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini basi (atimize) hisabu (ya siku alizoacha kufunga) katika siku zingine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na pia (anakutakeni) mtimize hesabu hizo...” (2:185)**, mpaka mwisho.

Mtume (s.a.w.w) alipokuwa akisafiri katika mwezi wa Ramadhani alikuwa akifungua saumu yake na akawatangazia watu (kuwa yeye amefungua), na aliona kufunga safarini ni maaswia na akatilia nguvu kwa kusema: “Sio wema kufunga safarini,” na utasikia hayo yote kwa uwazi wa maneno ya Mtume (s.a.w.w).

Kumetajwa katika Hadith ya Abuu Qalabah - nayo ni katika Hadith *sahihi* - kwamba Mtume (s.a.w.w) alimwambia mtu mmoja katika kabila la Banii A’mir: “Hakika Mwenyezi Mungu amemwondoshea msafiri saumu na sehemu ya swala.”

Mwenye kuziandama Sunna (Hadith) na maneno ya wanazuoni kuhusu swala ya msafiri na saumu yake atapata *Nassi* (hoja), *fat-wa* na *Ijmaa* ya umma kwamba kupunguza swala na kutokufunga safarini ni katika mambo ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameyafanya ni sharia katika dini ya Kiislamu. Bila shaka sababu ya kufanya mojawapo (kati ya kupunguza swala na kutokufunga) ndiyo sababu ya kufanya lingine.

## HUKUMU YA KUPUNGUZA SWALA (*QASR*)

Maimamu wa Kiislamu wametofautiana katika hukumu ya kupunguza swala safarini kwa kauli mbalimbali.

Miongoni mwao kuna aliyeona kwamba kupunguza swala ni faradhi kwa msafiri wala hana hiari. Hii ni kauli ya Imamiya (Shia) kwa kufuata Maimamu wao. Na kauli hii ndiyo rai ya Abuu Hanifa na wafuasi wake, na ndiyo rai ya wanazuoni wa (mji) wa Kufa.[74]

Miongoni mwao pia kuna aliyeona kwamba kupunguza swala na kutimiza - yote mawili - ni faradhi, lakini mwenye kuswali ana hiari (ya kuchagua alitakalo) kama hiari ya kutoa kafara ya wajibu, na hii ni rai ya wafuasi wa Shaafi.

74 Madhehebi ya Hanafi wameafikiana kwamba kupunguza swala ni lazima kwa msafiri wala haijuzu kwake kuswali kamili, na akiswali kamili huzangatiwa amefanya madhambi kwa kuchelewesha kutoa salam (ya swala) katika kikao cha faradhi, yaani kikao cha kwanza. Pamoja na hayo mtu huyo kwao atakuwa ameswali swala ya sunna katika zile rakaa mbili za mwisho, kwani faradhi ni zile rakaa mbili za mwanzo tu. Kwa maana hii wao wanahukumu kubatilika swala yake pindi akiacha kikao cha kwanza katika swala hiyo kwa sababu atakuwa ameacha nguzo ya swala.

Miongoni mwao vile vile kuna aliyeona kwamba kupunguza swala ni sunna iliyokokotezwa (iliyotiliwa nguvu). Hii ni rai ya Maalik katika riwaya mashuhuri kutoka kwake.

Miongoni mwao kadhalika kuna aliyeona kuwa kupunguza swala ni ruhusa tu, lakini kutimiza ni bora. Hii ni rai ya Shaafi katika riwaya mashuhuri kutoka kwake na ndio (rai) iliyoelezwa na Asw-hab zake.

Na madhehebu ya Hambali wanasema kuwa inajuzu kupunguza swala na ndio bora kuliko kutimiza, lakini siyo karaha kutimiza.

## HOJA ZETU

Imamiya wametoa hoja ya lazima ya kupunguza swala (safarini) kwa Hadith zilizo *sahihi* kwa njia za jamhuri (ahlus-Sunna) na kwa *nusus* (dalili) zilizothubutu kutoka kwa Maimamu waongofu wa Ahlul-Bayt (a.s).

Miongoni mwa Hadith *sahihi* kutoka kwa Jamhuri, ni ile iliyotajwa na Muslim katika *Sahihi* yake katika kitabu (mlango) cha Swala ya Wasafiri na Kupunguza Swala "Kutokana na Ibn Abbas kwa njia mbili amesema: Mwenyezi Mungu amefaradhia swala kupitia katika ulimi wa Mtume wenu (mkiwa) mjini rakaa nne, na safarini rakaa mbili." Hadith hii iko wazi kwamba msafiri ameamrishwa atekeleze swala ya Adhuhuri, Alasiri na Isha rakaa mbili mbili, kama alivyoamrishwa aliye mjini kuzitekeleza rakaa nne nne. Kwa hiyo haiswihi (haikubaliki) kwa msafiri isipokuwa ziwe ni rakaa mbili mbili kama alivyofaradhiwa. Vile vile haiswihi kwa aliye mjini isipokuwa ni rakaa nne nne kama alivyofaradhiwa, kwani ibada haikubaliki mpaka itekelezwe kulingana na vile ilivyoamrishwa.

Vile vile katika *Sahihi Muslim*, kwa *isnad* (mfulilizo wa wapokezi) mpaka kwa Musa ibn Salmah Al-Hadhli amesema: Nilimuuliza Ibn Abbas: Nitaswali vipi nikiwa Makka hali nikiwa msafiri? Akasema: Rakaa mbili

ambazo ndiyo sunna ya Abil-Qasim (s.a.w.w). Ibn Abbas alitoa jawabu moja kwa moja kana kwamba ni kitu kinachofahamika kuwa ni rakaa mbili na kuwa ni kumfuata Abil-Qasim (s.a.w.w). Na hii inajulisha kwamba kupunguza swala (safarini) ni jambo lisilofichikana hata kwa watu wa kawaida.

Pia Muslim ametoa Hadith katika *Sahihi* yake kwa njia ya Al-Zuhri kutoka kwa Urwa kutoka kwa A'isha, kuwa: "Mwanzo wa kufaradhiwa swala ilifaradhiwa rakaa mbili. Ikaendelea hivyo hivyo safarini na ikatimizwa (ikaongezwa) kwa aliye mjini." Al-Zuhri akasema: Nikamuuliza Urwa, kwa nini A'isha alikuwa anatimiza swala safarini? Akajibu: Yeye ameawili (tafsiri) kama alivyoawili Uthman.

Na katika *Sahihi Muslim*, kutoka kwa A'isha kwa njia nyingine, amesema: Mwenyezi Mungu aliifaradhia swala alipoifanya faradhi ikiwa ni rakaa mbili, kisha akaitimiza (akaiongeza) kwa aliye mjini, na swala ya msafiri ikabaki palepale katika faradhi ya kwanza.

**Nasema:** Jambo lililo wazi kabisa ni kwamba haya yakiwa ni kweli basi swala hiyo haitoswihi (haitokubalika) kwa msafiri akiswali rakaa nne kwa sababu (mtu) huyo hakuamrishwa na aliyeiweka sharia (Mwenyezi Mungu) hiyo. Bali tangu mwanzo yeye ameamrishwa atekeleze rakaa mbili, na Mwenyezi Mungu akazibakisha hivyo hivyo. Na lau msafiri atazitekeleza hali ya kuwa ni rakaa nne basi atakuwa amezua, na hili ni kama mtu aliyetekeleza faradhi ya swala ya asubuhi rakaa nne, pia ni kama mtu aliyeko mjini akazitekeleza faradhi zake za rakaa nne nne, rakaa mbili mbili.

Ama *nusus* (dalili) za Maimamu wa uongofu ni Hadith iliyo *sahihi* kutoka kwa Zurara ibn A'yun na Muhammad ibn Muslim, walipomuuliza Imam Abu-Ja'far Al-Baqir (a.s) wakasema: Unasema nini kuhusu swala safarini? Iko vipi, na ina rakaa ngapi? Akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema: "Pindi mkisafiri katika ardhi hapana makosa kwenu kupunguza

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 51



swala" (4:101). Kwa hiyo kupunguza ni lazima kama ilivyo ni lazima kutimiza kwa aliye mjini." Wakasema: Tumesema kwamba Yeye (Mwenyezi Mungu) amesema "pindi mkisafiri katika ardhi hapana makosa kwenu kupunguza swala," wala hakusema punguzeni swala! Sasa ni vipi amelifanya hilo ni lazima kama alivyofanya ni lazima kutimiza?

Akasema (Imam): Je Mwenyezi Mungu hakusema kuhusu Swafaa na Marwa

﴿ فَمَنْ حَجَّ ٱلْبَيْتَ أَوِ ٱعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَن يَطَّوَّفَ بِهِمَا ۚ ﴿١٥٨﴾ ﴾

**"Mwenye kuhiji nyumba (Kaaba) au akafanya umra, hapana makosa kwake azitufu (Swafaa na Marwa)" (2:158)**.

Je, huoni kuwa hiyo twawafu ni lazima iliyofaradhiwa kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameitaja katika Kitabu Chake, na Mtume Wake aliifanya? Vile vile kupunguza swala safarini ni kitu alichokifanya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu amekitaja katika Kitabu Chake. Wakasema (Zurara na Muhammad): Tunauliza, je, mtu akiswali safarini rakaa nne arudie au asirudie? Akasema (Imam): Kama amesomewa aya ya kupunguza swala na akatafsiriwa, pamoja na hivyo akaswali rakaa nne, basi atarudia; na kama hakusomewa (aya hiyo) wala hakuijua, basi sio lazima kwake kurudia. Akaendelea kusema (a.s): Na swala safarini katika kila faradhi ni rakaa mbili isipokuwa swala ya Magharibi, kwani yenyewe ni rakaa tatu wala haipunguzwi. Mtume (s.a.w.w) ameiacha hali ya kuwa ni rakaa tatu safarini na mjini."

Imam At-Twabrasi amesema baada ya kuitaja Hadith hii: Hii inajulisha kwamba faradhi ya msafiri ni tofauti na faradhi ya aliye mjini. (Akaendelea): Hakika taifa (mashia wote) wameafikiana hivyo na wameafikiana kuwa huko siyo kupunguza (swala) kwani imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) kwamba amesema: "Faradhi ya msafiri ni rakaa mbili na wala siyo kupunguza." **Mwisho wa tuliyoyanukuu kutoka**

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 52



***Majma'a Albayan*.**

Katika (kitabu) *Al-Kashaaf* kuhusu aya hii ya kupunguza swala, amesema: "Kwa Abuu Hanifa kupunguza swala safarini ni lazima wala siyo ruhusa tu. Kwa hiyo haijuzu (hairuhusiwi) namna nyingine (isipokuwa ni kwa kupunguzwa). Akaendelea kusema: Na kutokana na Umar ibn Khattab, yeye amesema: Swala ya safari ni rakaa mbili na ni kutimiza (siyo kupunguza) kwa ulimi wa Mtume wenu.[75]

## HOJA ZA SHAFII NA YEYOTE ASIYEONA NI LAZIMA KUPUNGUZA (SWALA)

**Wametoa hoja kwa mambo mengi:**

**La kwanza:** Ni dhahiri ya neno la Mwenyezi Mungu: "Hapana makosa kwenu kupunguza swala," kwani kuondoshewa makosa maana yake ni kuondoshewa madhambi, na hii inalifanya jambo hilo kuwa ni *mubaha* (lenye kufaa, kufanya na kuacha ni sawa) wala siyo lazima.

Bila shaka jibu lake umekwisha kulijua kutokana na maneno ya Imam Abii Ja'far Al-Baqir (a.s). Kana kwamba watu wakati huo (wa Mtume) walikuwa wamezoea kutimiza swala. Kwa sababu hiyo - kama alivyoeleza Imam Zamakhshari katika (kitabu chake) *Al-Kashaaf* - walikuwa na dhana katika akili zao kwamba kupunguza swala kuna upungufu (katika thawabu), ndipo Mwenyezi Mungu akawaondoshea makosa ili nafsi zao ziwe safi katika kupunguza, na wawe na hakika nalo.

**La pili:** Uthman na A'isha walikuwa wakitimiza swala safarini.

75 Kama swala safarini ni rakaa mbili, na kuswali kwa rakaa mbili ndio ukamilifu wake wala siyo kupunguza, na yote hayo ni kwa ulimi wa Mtume wetu, kwa ushahidi wa Umar, sasa ni kwa nini isihi (ikubalike) kwa rakaa nne? Je, ibada inakubalika ikifanyika kinyume na alivyoiwekea sharia Mwenyezi Mungu Mtukufu?

**Jibu:** Wao wameawili (wametafsiri) dalili (hoja) za kupunguza swala na walikosa. Baadhi ya wanazuoni wa jamhuri wametafsiri taawili yao hii kwamba Uthman alikuwa ni *Amiril muuminina* (kiongozi wa waumini) na A'isha alikuwa ni mama yao. Kwa hiyo wao katika safari zao bado wako katika mji wao. Kwa kuzingatia kwamba wao popote wanaposafiri wako kwa watu wao, nyumba zao na miji yao. Hizi ni fikra zao za kuzua, na tunaona kwa nini ikawa ni uzushi. Kwa sababu inaonyesha kuwa Mtume (s.a.w.w) alikuwa ni mgeni katika hii dunia ya waumini, kwani haikupokewa kutoka kwake akiwa safarini isipokuwa ni kupunguza swala. Vile vile, kwa msingi huu, Abu Bakr, Umar na Ali watakuwa wageni kwao (*waumini*)!

**La tatu:** Ni Hadith ambazo ni mashuhuri alizozitaja Muslim katika *Sahihi* yake zinasema wazi kuwa maswahaba walikuwa wakisafiri pamoja na Mtume (s.a.w.w) miongoni mwao wakawa wanakusuru, na wengine wanatimiza, na miongoni mwao wakawa wanafunga (saumu) katika mwezi wa Ramadhani na wengine wakafungua, na hakuna watu waliowatia ila (aibu) wenzao (katika kufunga na kufungua).

**Jibu:** Hakuna chochote kilichothubutu katika hizi Hadith kwa njia yetu. Pia hizi Hadith zinapingana na Hadith zilizo *sahihi* ambazo zimepokewa kutoka kwa Maimamu wetu ambao wao ndio wenza wa Kitabu (Qur'ani). Vile vile zinapingana zenyewe kwa zenyewe kama anavyofahamu mwenye kuzingatia, na kama utakavyosikia karibuni Mwenyezi Mungu Mtukufu akipenda.

Hakuna mwenye shaka kwamba Hadith za mawaswii (walioachiwa wasia) katika nyumba ya Muhammad ni zenye kutangulizwa zinapopingana na zingine hususan baada ya kuwa zinatiliwa nguvu na kundi la Hadith *sahihi* za jamhuri (*Ahalus-Sunna*).

## HUKUMU YA KUTOKUFUNGA SAUMU

Wanazuoni wa fiqhi wa Kiislamu wametofautiana katika hukumu ya kutokufunga safarini. Jamhuri wameona kuwa ni ruhusa tu, na kwamba msafiri akifunga saumu yake *itaswihi* (itafaa) na itatosheleza. Wamelitolea hoja hilo kwa Hadith alizozitaja Muslim katika *Sahihi* yake.

Miongoni mwa hizo Hadith ni Hadith ile iliyopokewa kutoka kwa Abu Said Al-Khudri kuwa amesema: “Tulikwenda vitani pamoja na Mtume (s.a.w.w) baada ya kupita siku kumi na sita za mwezi wa Ramadhani. Miongoni mwetu walikuwa wamefunga, na wengine walikuwa hawakufunga. Aliyefunga hakumtia aibu ambaye aliyefungua, wala ambaye hakufunga hakumtia aibu aliyefunga.”

Pia kutoka kwake kwa njia nyingine amesema: “Tulikuwa tukisafiri pamoja na Mtume (s.a.w.w) katika mwezi wa Ramadhani, na wala hatiwi aibu mwenye kufunga kwa saumu yake na wala ambaye hakufunga kwa kutofunga kwake.”

**Jibu:** Hizi Hadith - zikijaaliwa kuwa zimeswihi - basi kwa namna yoyote ile zitakuwa zimefutwa (hukumu zake) kwa Hadith *sahihi* zilizopokewa kwa njia ya jamhuri, na Hadith zingine *sahihi* zilizopokewa kwa njia yetu kutoka kwa Maimam wa Ahalul-Bayt (a.s).

Hapa tunakutajia Hadith zilizo sahihi katika mlango huu kwa njia ambayo siyo yetu. Imepokewa kutoka kwa Jaabir ibn Abdillah kuwa amesema - kama ilivyo katika *Sahihi Muslim*: “Mtume (s.a.w.w) katika mwaka wa Fat’hi alitoka kwenda Makka katika mwezi wa Ramadhani. Alifunga mpaka akafika Kura’i al-Ghamim. Pia watu walikuwa wamefunga. Kisha akaomba chombo cha maji na akakiinua mpaka watu wakawa wakiona. Hatimae akayanywa. Baada ya hapo akaambiwa: “Kuna baadhi ya watu wamefunga.” Hapo akasema (s.a.w.w): Hao wameaswi hao wameaswi!”

Na ametaja Muslim pia kutoka kwa Jaabir. Amesema: “Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alikuwa safarini, akamuona mtu amezungukwa na watu na amewekewa kivuli. Akauliza (Mtume): Ana nini huyo? Wakajibu: Ana saumu. Hapo akasema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu: Siyo kutenda wema nyinyi kufunga safarini.”

Hakika si jambo lingine, sisi tumesema kuwa Hadith hizi zimefuta zile (walizozitolea hoja) kwa sababu zilikuja baada ya zile, na jamhuri wenyewe wamelikiri hilo. Na kinachojulisha haya ni zile Hadith zilizomo katika *Sahihi Muslim* na vitabu vingine kutoka kwa Ubaidullah ibn Abdillah ibn U’tba kutoka kwa ibn Abbas kwamba yeye (Ibn Abbas) alinipa habari kwamba Mtume (s.a.w.w) alitoka mwaka wa Fat-hi na alikuwa amefunga mpaka akafika Al-Kadid akafungua. Akasema (U’tba): Na maswahaba wa Mtume walikuwa wakifuata maamrisho Yake yaliyo mapya zaidi (na wakaacha yaliyotangulia).

Imepokewa kutoka kwa Az-Zuhri - kama ilivyo katika *Sahihi Muslim* na vitabu vingine - kwa *isnadi* (mapokezi) hii hii. Az-Zuhri amesema: “Kutokufunga (safarini) kulikuwa ndiyo kwa mwisho kati ya mambo haya mawili (kufunga na kutokufunga), na hakika linalochukuliwa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) ni lile linalokuwa la mwisho zaidi.”

Na imepokewa kutoka kwa ibn Shihab - kama ilivyo katika *Sahihi Muslim* na vitabu vingine - kwa *isnad* hii hii pia, kwamba Ibn Shihab alisema: “Walikuwa wakifuata jipya baada ya jipya katika maamrisho Yake (Mtume), na walikuwa wakiliona (jipya) ni lenye kufuta lile (la zamani).” Kwa ufupi, lau ikajaaliwa kuwa saumu za wale baadhi ya maswahaba wake safarini pamoja naye ziliswihi (zilikubalika), basi hiyo ilikuwa ni kabla ya kulazimishwa kutokufunga (safarini) na kabla ya Mtume (s.a.w.w) kusema: “Sio kutenda wema nyinyi kufunga safarini,” na pia kabla ya kusema kuwaambia wale waliyofunga: “Hao wameaswi. Hao wameaswi!”

Ama Imamiya wao wameafikiana kuwa kutofunga saumu safarini ni lazima. Na hiyo ndiyo madhehebu ya Daud ibn Ali Al-Asfahani na asw-habi zake, na hivi hivi ndivyo walivyosema maswahaba wengi kama Umar ibn Khattab, mtoto wake Abdillah, Abdallah ibn Abbas, Abdurrahman ibn A’uf, Abu Hurairah na U’rwa ibn Zubeir. Hili ni jambo *mutawatir* (lililopokewa kwa wingi) kutoka kwa Maimam wa uongofu wa kizazi kitakatifu (cha Mtume).

Imepokewa kwamba Umar ibn Khattab alimwamrisha mtu ambaye alikuwa amefunga safarini arudie saumu yake kama yalivyo madhehebu yetu na ya Daud. Na amepokea Yusuf ibn Al-Hakam amesema kuwa: “Nilimuuliza Ibn Umar kuhusu kufunga safarini, akanijibu: “Waonaje lau ukatoa swadaka kumpa mtu, kisha akakurudishia, je hukasiriki? Hiyo ni swadaka aliyoitoa Mwenyezi Mungu kuwapa nyinyi, basi msiirudishe.”

Amepokea Abdur-Rahman ibn A’uf kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: “Mwenye kufunga safarini ni kama mwenye kufungua mjini.”

Kutoka kwa ibn Abbas (amesema): kufungua saumu safarini ni lazima. Na imepokewa kutoka kwa Abuu Abdillah As-Swadiq (a.s) kuwa: “Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani safarini ni kama mwenye kufungua katika Ramadhani (na yeye yuko) mjini kwake.” Na imepokewa tena kutoka kwake (a.s): “Lau mtu atakufa na hali amefunga safarini, basi siwezi kumswalia.” Na tena (a.s) amesema: “Mwenye kusafiri, atafungua saumu na atakusuru swala isipokuwa ikiwa safari yake ni ya kumuaswi Mwenyezi Mungu Mtukufu.” Vile vile amepokea Al-Ayash kwa mapokezi yake mpaka kwa Muhammad ibn Muslim kutoka kwa Abu Abdillah As-Swadiq (a.s) kuwa: “Aya hii **{..na yule ambaye ni mgonjwa katika nyinyi au yuko safarini... (2:184)}** ilishuka sehemu inayoitwa Kurai’ Alghamim wakati wa swala ya adhuhuri. Mtume (s.a.w.w) aliomba chombo kilicho na maji akayanywa na akawaamrisha watu wafungue (saumu yao). Baadhi ya watu wakasema: “Mchana umekwisha pita kwa nini tusitimize siku yetu?”

Mtume (s.a.w.w) akawaita (kwa jina) *Aal-u’swat* (wenye kuaswi).” Wala hawakuachwa kuwa ni wenye kuitwa *Aal-u’swat* (wenye kuaswi) mpaka Mtume (s.a.w.w) akafa.

Yatutosha; kuwa neno la Mwenyezi Mungu: **“Basi atakayekuwa mjini kwake (katika huu mwezi) afunge na mwenye kuwa mgonjwa au safarini atatimiza idadi (ya siku alizo fungua) katika siku zingine Mwenyezi Mungu anawatakia nyinyi mepesi wala hawatakii mazito,”** kuwa ni hoja ya kulazimu kutofunga safarini. Na hilo ni kwa njia nyingi:

**Ya kwanza**: Amri ya lazima ya saumu katika aya hii si lingine bali imeelekezwa kwa mtu aliye mjini kwake wala siyo kwa aliye safarini. Lafudhi (tamko) yake kama unavyoiona: “Mwenye kushuhudia katika nyinyi huu mwezi - maana yake ni aliye mjini kwake katika huu mwezi - basi ni aufunge.” Kwa hiyo msafiri hakuamrishwa. Saumu yake itakuwa ni kutia katika dini kisicho kuwa katika dini kwa kulazimisha na kwa kuzua.

**Ya pili**: *Mafuhumi* (istilahi ya usuliil fiqhi) ya neno lake Mwenyezi Mungu: “Atakayekuwa mjini kwake katika huu mwezi afunge,” ni mtu ambaye hayuko mjini kwake katika huu mwezi sio lazima kwake kufunga saumu, na *mafuhumi ya sharti* (istlahi) ni hoja kama ilivyokaririwa katika usulil fiqhi. Kwa hiyo aya hii inajulisha kwamba sio lazima kufunga saumu safarini kwa *mantuqi* yake na *mafhumi* yake.

**Ya tatu**: Ni neno Lake Mwenyezi Mungu: **“…Na mwenye kuwa mgonjwa katika nyinyi au akawa safarini akamilishe idadi katika siku zingine.”** Neno *i’ddat* (kukamilisha idadi) katika aya hii linaweza kukadiriwa kwa namna mbili:

Ni juu yake kukamilisha idadi (aliyofungua) katika siku zingine. Na hii ni pindi likisomwa neno hili kwa *raf-i’*.
Na neno hili likisomwa kwa *nasbi* litakadiriwa kuwa ni afunge kukamilisha idadi katika siku zingine.

Kwa kila hali aya hii inajulisha lazima ya kufunga saumu katika siku zingine (kwa mgonjwa na msafiri). Hii inamaanisha kuwa na lazima ya kutokufunga saumu siku za safari, kwani hakuna hata mtu mmoja anayesema ni lazima kufunga saumu na tena ni lazima kulipa kadha, kwa sababu kukusanya yote mawili kunapingana na wepesi ambao unazungumziwa na aya hii.

**Ya nne:** Ni neno lake Mwenyezi Mungu: “Mwenyezi Mungu anawatakieni nyinyi wepesi wala hawatakii uzito”. Wepesi katika aya hii si jambo lingine isipokuwa ni kutokufunga saumu. Vile vile uzito katika aya hii si jambo lingine isipokuwa ni saumu. Kwa hiyo maana ya aya hii ni: Mwenyezi Mungu anataka kwenu kutokufunga saumu wala hataki kwenu kufunga.

## UMBALI WA SAFARI YA SWALA KUPUNGUZWA NA SAUMU KUTOFUNGWA

Maimamu wa Kiislamu wametofautiana katika kukadiria umbali wake. Amesema Abu Hanifa, asw-hab wake na wanazuoni wa Kufa kwamba uchache wa umbali ambao swala hupunguzwa na kutofunga saumu ni safari ya siku tatu. Na hakika ya kupunguza swala na kutofunga saumu huwa ni kwa kusafiri safari ya kutoka pembe hadi pembe.[76]

Amesema Shaafi, Maalik, Ahmad na watu wengi: swala hupunguzwa na saumu hufunguliwa katika mwezi wa Ramadhani kwa kusafiri umbali unaofikia farsakhi kumi na sita kwenda tu.[77] Na wamesema Ahlu-dhahir (wenye kuchukuwa Qur’ani kwa dhahiri yake) kuwa kupunguza swala na

76 Ibn Rushd ameyanukuu haya kutoka kwao katika kitabu chake *Bidayatul Mujtahid.*

77 Umbali huu ni sawa sawa na kilometa 80 na nusu na mita 140, ambao ni umbali wa mwendo wa usiku na mchana kwa mwendo wa ngamia aliebeba mzigo mzito na anayekwenda mwendo wa wastani. Kwao haidhuru kupungua kiasi kidogo katika kiasi hiki kama utakuwa ni upungufu mdogo kama maili moja au mbili.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 59



kutofunga saumu ni kwa kila msafiri hata kama ni safari ya karibu.

Amesema Ibn Rushdi (katika mlango wa Swala ya Msafiri katika Kitabu chake *Bidayatul Mujtahid*: "Sababu ya kukhitalifiana kwao inatokana na kutofautiana kwao katika mlango huu kufahamu maana ya safari yenye kukubalika kupunguzia swala na kutokufunga saumu. Kwani lenye kufanya safari iwe ni yenye kuathiri kupunguza swala na kutofunga saumu ni safari hiyo iwe na taabu ndani yake. Ikiwa ni hivyo, basi kupunguza swala na kutofunga saumu huwa katika safari yenye taabu. Kwa Abu-Hanifa taabu haipatikani isipokuwa ni kwa safari ya kukata marhala tatu (siku tatu), na kwa Shafi, Malik na Ahmad huwa kwa kukata farsakhi kumi na sita.

Akasema (Ibn Rushdi): Ama yule ambaye hachungi katika hilo (safari) isipokuwa ni tamko (la safari) tu kama vile Ahlu-Dhahir wao wamesema: "Mtume (s.a.w) amesema wazi kuwa Mwenyezi Mungu amemuondoshea msafiri saumu na sehemu ya swala. Mtu yeyote atakayeitwa msafiri yajuzu kwake kupunguza swala na kutofunga saumu." Akasema (Ibn Rushdi): na hilo wamelitilia nguvu kwa Hadith alizopokea Muslim kutoka kwa Umar ibn Khattab kwamba Mtume (s.a.w.w) alikuwa akipunguza swala kwa safari ya mfano wa maili kumi na saba. **Mwisho wa kunukuu.**

Kulingana na haya, Maimamu wa madhehebu manne, katika kuweka mpaka wa umbali wa safari, hawakutegemea hoja yoyote katika maneno ya Mtume au vitendo vyake, isipokuwa wao wametegemea falsafa ambayo waliiita *maanal maaquli* (maana yenye kukubalika kiakili). Na hilo ni jambo ambalo Maimamu wa Ahlul-Bayt hawaliridhii wala hawalitegemei katika kutoa hukumu za sharia.

Watu wa Makka wakati wa Mtume (s.a.w.w), Abu Bakr na Umar walipokuwa wakitoka Makka kwenda Arafa, walikuwa wakipunguza swala wakiwa Arafa, Muzdalifa na Minaa. Hili ni jambo lililothubutu, wala halina shaka.

Mashekhe wawili (Bukhari na Muslim) wamepokea katika *sahihi* zao kuwa Mtume (s.a.w.w), wakati alikitoka Makka kwenda Arafa, alikuwa akipunguza swala. Pia baada yake Abu Bakr na Umar walipunguza. Na kwamba Uthman pia alipunguza, kisha akatimiza baada ya kupita miaka sita ya Ukhalifa wake na watu wakampinga katika jambo hilo.**[78]**

Haya ndio mategemezi ya Imam Maalik aliposema kuwa kupunguza swala mahujaji wakiwa sehemu hizi ni sunna iliyotiliwa nguvu, sawa sawa wawe ni watu wa Makka au wa sehemu zingine za mbali. Rudia fiqhi ya madhehebu ya Maalik.**[79]**

---

78 Hayo yote utayapata katika mlango wa swala ukiwa Minaa, nao ni miongoni mwa milango ya kupunguza swala na ni miongoni mwa milango ya Haji katika juzu ya kwanza ya Sahihil Bukhar. Pia utayapata katika kitabu (mlango) cha swala ya wasafiri na kuipunguza kwake katika Sahihi ya Muslim. Pia utapata katika uk. 178 katika kitabu cha Profesa Twaha Hussein kinachoitwa Alfitnat Alkubra na hapa namnukuu: “Kisha waislam walioishi pamoja na Uthman walimlaumu kwa kukhalifu sunna ya Mtume (s.a.w.w) iliyojulikana sana kutoka kwake, kwa mashekhe wawili (Abu Bakr na Umar) na kwa Uthman mwenyewe katika mwanzo wa ukhalifa wake. Hayo yote ni pale alipotimiza swala akiwa Minaa na ilihali Mtume (s.a.w.w) alipunguza. Pia mashekhe wawili walipunguza na yeye Uthman alipunguza kwa miaka mingi, kweli waislamu walishtuka sana alipotimiza swala Minaa, baadhi yao wakaenda kwa wengine na baadhi yao wakalizungumza na wengine. Kisha Abdur-Rahman ibn A’uf akamkabili Uthman akamwambia: Je, wewe hukuswali hapa pamoja na Mtume rakaa mbili? Akajibu: Ndiyo. Abdulr-Rahman akamuuliza tena: Je, wewe hukuswali pamoja na Abu Bakr na Umar rakaa mbili? Uthman akajibu: Ndiyo, Abdulr-Rahman akamuuliza tena: Wewe mwenyewe hukuwaswalisha watu hapa rakaa mbili? Akajibu: Ndiyo. Akamuuliza tena: Sasa ni uzushi gani huo uliouzua? Uthman akajibu kwa kusema: Mimi nimesikia kwamba watu wa vijijini na wapumbavu wa Yemen wanasema kwamba swala ya mtu akiwa mjini kwake ni rakaa mbili. Abdulr-Rahman akamjibu: Hofu yako kwa watu wa vijijini na wapumbavu wa Yemen siyo sawa, kwani Mtume (s.a.w.w) ameswali rakaa mbili na ilihali Uislamu ulikuwa bado haujaenea. Sasa Uislamu umeenea kwa majirani wote wala haitakikani wewe uogope.”

79 An-Nawawi amenukuu kutoka kwa Maalik katika sherehe yake ya *Sahihi Muslim* katika kitabu (mlango) cha swala ya wasafiri na kuipunguza kwake.

Pia haya ndiyo mategemezi (hoja) yetu katika kupunguza swala katika safari ya umbali wa farsakhi nane sawa ziwe ni za moja kwa moja au ni za kuunga nne kwenda na nne kurudi, kama umbali ulioko kati ya Makka na Arafa, nao ndiyo umbali mchache kabisa Mtume (s.a.w.w) aliopunguzia swala. Na hii ndiyo hoja ya kukata kabisa *walhamdu lillahir Rabil a'lami-in.*

# NDOA YA MUT'A

## 1. UHAKIKA WA NDOA HII

Uhakika wa ndoa hii ni mwanamke ambaye ni muungwana kikamilifu na mwislamu au *ahlulkitab* (waliopewa Kitabu) ajioze nafsi yake, wakati ambapo hakuna kizuizi cha kisharia ya Kiislamu kumuowa mwanamke huyo kwa nasaba au sababu au kunyonya au kuolewa au eda au kizuizi kingine miongoni mwa vizuizi vya kisharia, kama vile akawa aliwahi kuolewa na mmoja wa wazazi wako (baba, babu...) hata kama alikwisha kumtaliki, au alikufa akamuacha kabla ya kumuingilia, au mfano akawa ni dada wa mke wako, au mfano mwingine.

Huyu mwanamke ajioze kwako kwa mahari maalumu, kwa muda maalumu, kwa kufunga ndoa iliyokusanya sharti zote za kisharia za kuswihi ndoa, iwe haina kizuizi chochote cha kisharia kama ulivyosikia. Huyo mwanamke aseme kukuambia wewe, baada ya kuridhiana na kuafikiana kati yenu wawili: nimejioza kwako kwa mahari kiasi kadhaa, kwa muda kadhaa (ataje idadi yake) kwa mfano siku moja au mwezi au miezi miwili au mwaka au miaka miwili au ataje muda mwingine maalumu, na wewe useme kumwambia yeye kwa haraka: Nimekubali.

Na katika ndoa hii kila mmoja, kati ya mume na mke, inajuzu kuwakilisha watu wengine kama ilivyo katika vifungo (kama vya bei, ijara n.k) vingine. Ndoa hiyo ikitimia yule mwanamke atakuwa mke wako, na wewe utakuwa

mume wake mpaka mwisho wa wakati uliopangwa katika hiyo ndoa; na kwa kukoma ule muda tu basi (yule mwanamke) atakuwa ameachika bila ya talaka, yaani kama ilivyo katika ijara.

Pia inafaa kwa mume kumuacha kabla ya kumalizika muda kwa kumpa hiba ule wakati uliobaki, lakini siyo kwa talaka. Hii ni kufuatana na *nusus* (dalili) maalumu zenye kuhukumu hivyo. Na ni lazima kwa yule mwanamke, kama atakuwa ameingiliwa,[80] kukaa eda baada ya kupewa hiba ya muda au kumalizika muda uliopangwa; na eda yake itakuwa ni tahara mbili kama atakuwa ni mwanamke mwenye kupata hedhi. Na kama hapati hedhi itakuwa ni siku arobaini na tano kama eda la suria. Hii ni kulingana na dalili (hoja) maalumu zinazohukumu hivyo. Na kama atampa hiba ule muda, au ukamalizika bila ya kumgusa, basi atakuwa hana eda kama mwanamke aliyetalikiwa kabla ya kuguswa.[81] Na wale wenye mimba katika ndoa ya mut’a, eda lao ni kuzaa ile mimba kama wenye mimba katika ndoa ya daima. Ama eda la mwanamke aliyefiwa na mume wake wa ndoa ya mut’a, eda lake ni vile vile kama eda la mwanamke aliyefiwa na mume wake katika ndoa ya daima.[82]

Mtoto wa mut’a wa kike au wa kiume ananasibishwa na baba yake wala haangaliwi vingine isipokuwa ni kama watoto wake wengine. Na mtoto huyo katika kurithi ni kama alivyotuusia Mwenyezi Mungu Mtukufu katika neno Lake: **“Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu, mwanamume apate sawa na fungu la wanawake wawili...”** Wala haku-

80Na kama hajafikia miaka ya kukata tamaa ya hedhi ya kisharia.

81 Kwani hakuna eda kwa mwanamke aliyefikia miaka ya kukata tamaa ya hedhi kama ilivyo katika talaka.

82 Ni sawa awe ameingiliwa au la, sawa awe amekata tamaa au la. Na sawa awe na mimba au hana. Na eda la mwenye mimba, akifiliwa na mume wake katika ndoa zote mbili, ni muda uliyo mrefu katika nyakati mbili, nazo ni kuzaa na kumalizika muda wa eda ambao ni miezi minne na siku kumi baada ya yeye kujua kifo cha mume wake.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 63



na tofauti kati ya watoto wako wawili; aliyezaliwa kwa ndoa hii (mut'a) na mwingine aliyezaliwa kwa ndoa ya daima. Pia hukumu zote za sharia zenye kuzungumzia watoto na wazazi zinawakusanya watoto wa mut'a na wazazi wao. Vile vile hukumu za jumla zinazozungumzia ndugu wa kike na wa kiume na watoto wao, maami, mashangazi, wajomba, makhalati na watoto wao zinaingia kama alivyosema Mwenyezi Mungu: **"...Na ndugu wa nasaba baadhi yao ni bora kuliko baadhi nyingine katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu….."**

Ndio, ndoa ya mut'a peke yake haisababishi mke na mume kurithiana, wala zamu ya kulala, wala lazima ya chakula kwa mke wa mut'a. Na inafaa kwa mume kufanya *azli* (kushusha manii nje) na huyo mwanamke. Na hiyo ni kutokana na dalili makhususi ambazo zinahusisha yale yaliyopokewa kwa ujumla katika mambo haya ya hukumu za walioolewa.

Hivi ndivyo ndoa ya mut'a vile ilivyo, na hii ndiyo mut'a ya wanawake kwa uhakika wake, na hapa ndipo mahala tulipotofautiana sisi na jamhuri (*Ahlul-sunna*).

## 2. ITIFAKI YA UMMA JUU YA USHARIA WAKE

Wameafikiana watu wa *kibla* (Waislamu) wote kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweka sheria ya ndoa hii katika dini ya Kiislamu. Kiasi hiki hakina shaka kwa yoyote katika wanazuoni wa madhehebi ya Kiislamu pamoja na tofauti zao za mitazamo, madhehebi na rai. Bali huenda hili likatiwa - kwa Ahlu-Sunna - ni katika dharura za kidini. Na kutokana na yaliyothubutu kutoka kwa Bwana wa Mitume (s.a.w.w) hakuna hata mmoja mwenye kupinga katika wanazuoni wa umma wake. Na mwenye kuzingatia yale yanayosemwa na wenye madhehebi yote ya Kiislamu katika hukumu ya ndoa hii akifuatilia fiqhi zao atajua kuwa wote wameafikiana juu ya asili ya kuwekwa sharia ya ndoa hii, isipokuwa wanadai kuwa ilifutwa kama utakavyosikia inshaallah.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 64



### 3. HOJA YA QUR'ANI JUU YA USHARIA WAKE

Yatutosha kuwa ni hoja ya usharia wake kauli ya Mwenye Mungu katika Surat An-Nisaa: **"..Basi na wale mnaostarehe (mnaowaowa) nao miongoni mwao wapeni mahari yao yaliyolazimu..." (4:24).** Kwani Maimamu wa Ahlul-Bayt na wafuasi wao wameafikiana kuwa aya hii imeshuka kuhusu ndoa hii ya mut'a. Na Ubaiya ibn Ka'bi, ibn Abbas, Said ibn Jubair na Al-Sidi walikuwa wakiisoma aya hii: "..Basi na wale mnaostarehe (mnaowaowa) nao miongoni mwao *kwa muda maalumu*..."[83] (walikuwa wakiongeza neno kwa muda maalumu). Na amesema dhahiri swahaba I'mran ibn Haswin kwamba aya hii ilishuka kuhusu mut'a, na hii ndoa haijafutwa mpaka mtu mmoja akasema kwa rai yake aliyoyataka.[84] Vile vile Mujahid amesema wazi kuwa aya hii imeshuka kuhusu mut'a katika maneno aliyoyataja Twabari katika tafsiri yake inayoitwa *Al-Kabiir*.[85]

83 Hayo yamepokewa na wanazuoni wengi wakubwa kama Twabari alipozungumzia aya hii katika Juzu ya tano ya tafsiri yake iitwayo *Al-Kabir*. Zamakhshari amekitaja kisomo hiki kama kitu kinachojulikana katika kitabu chake *Al-Kashaaf* kutoka kwa Ibn Abbas. Na amenukuliwa kadhi I'yadh kutoka kwa Al-Maziri kama ilivyo katika mwanzo wa Mlango wa Ndoa ya Mut'a katika sherehe ya *Sahihi Muslim* ya Imam An-Nawaw: Kwamba Ibn Mas'ud alisoma: "Na wale mnaowaowa miongoni mwao mpaka muda maalumu…" Na Ar-Razi ametaja katika kuitafsiri aya hii kwamba amepokewa Ubaiya ibn Ka'b kwamba alikuwa akisoma: "..na wale mnaowaowa miongoni mwao kwa muda maalumu wapeni mahari yao" na akasema: Pia hiki ndicho kisomo cha ibn Abbas. Akasema: Na umma (wa Kiislamu) haukuwapinga kisomo chao hiki. Akandelea kusema: Na hiyo ilikuwa ni ijmaa (kitu kinachojulikana) kwa umma kwamba inafaa kusoma hivi... mpaka mwisho wa maneno yake katika uk. 201 Juz. 1 ya tafsiri yake *Al-Kabir.*

84 Utaona maneno yake kuhusu jambo hili hivi karibuni.

85 Rudia uk. 9 wa juzu yake ya tano.

Na ushahidi wa haya ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alikwisha bainisha katika mwanzo wa hii sura hukumu za ndoa ya daima kwa kauli Yake: **“..Oweni mnaowapenda katika wanawake wawili au watatu au wanne…” (4:3).** Mpaka akasema: **“..na wapeni wanawake mahari yao hali ya kuwa ni hidaya (waliopewa na Mwenyezi Mungu)” (4:4).** Sasa aya hii pia ingekuwa inazungumzia ndoa ya daima basi ingesababisha kurudia mambo hayo hayo katika sura moja. Ama kama itakuwa inabainisha ndoa ya mut’a, basi itakuwa inabainisha mambo mapya, na wenye kuzingatia, ambao wameizingatia Qur’ani yenye hekma, na walijua kwamba *Surat An-Nisaa* imekusanya ndoa zote za Kiislamu. Ndoa ya daima na kumiliki suria vimebainisha kwa neno Lake Mwenyezi Mungu: **“Oweni mnaowapenda katika wanawake wawili au watatu au wane, na kama mtaogopa kuwafanyia uadilifu basi (oeni) mmoja tu, au wale waliomilikiwa na mikono yenu.”**

Na ndoa ya kumwoa suria (wa mtu mwingine) imebainisha kwa neno lake Mwenyezi Mungu: **“…Na asieweza katika nyinyi mahari ya kuowa wanawake waungwana waislamu, (basi aowe) wajakazi walio waislamu ambao mmewamiliki…” (4:25)**. Mpaka akasema: **“…Waoweni wao kwa idhini ya mabwana zao na muwape mahari yao kwa sharia…” (4:25)**. Na mut’a imebainishwa kwa aya yake hii: **“...Basi na wale mnaostarehe (mnaowaowa) miongoni mwao wapeni mahari yao…..”**

### 4. USHARIA WAKE KWA NUSUSI ZA HADITH

Zinatutosha miongoni mwa Hadith katika mlango huu, Hadith *sahihi* zilizo *mutawatir* (zalizopokewa kwa wingi) kutoka kwa Maimamu wa Kizazi Kitakatifu. Na wamepokea mashekhe wawili; Bukhari na Muslim katika kuzungumzia usharia wa ndoa hii Hadith nyingi zilizo *sahihi* kutoka kwa wote wafuatao: Salma ibn Al-Aku’i, Jabir ibn Abdullah, Abdullah ibn Mas’ud, Ibn Abbas, Abu Dhar Al-Ghafaari, Emraan ibn Haswiin, Al-Aku’i ibn Abdullah Al-Aslami na Sabra ibn Ma’bad. Na amepokea Ahmad ibn Hambal katika *Musnad* yake kutoka Hadith za hawa wote, na pia kutoka

kwa Umar na mtoto wake Abdullah.

Na amepokea Muslim katika Mlango wa Ndoa ya Mut'a katika kitabu (mlango) cha Nikaha katika juzu ya kwanza ya Sahihi yake kutoka kwa Jabir ibn Abdillah na Salma ibn Al-Aku'i wote wawili wamesema: "Alitutokea mwenye kutangza kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) na akasema: hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu amewapa idhini nyinyi mstarehe, yaani mut'a ya wanawake" *mwisho wa maneno yake*.

Na Hadith *sahihi* katika jambo hili ni nyingi sana; hazitoshi kuzitaja katika imla hii.

**5. WENYE KUSEMA KUWA IMEFUTWA: HOJA ZAO NA KUZITAFAKARI**

Wenye madhehebi manne na wengine katika wanazuoni wa jamhuri wamesema kuwa ndoa hii ilifutwa na ni haramu, na huku wakitoa hoja kwa Hadith walizozipokea mashekhe wawili katika *sahihi* zao. Hakika tumeziangalia kwa makini, kwa uhuru na bila kuelemea upande wowote tukazipata kuwa zinagongana kuhusu wakati wa kufutwa (ndoa hii) kiasi ambacho haziwezi kuaminika. Kwa mfano baadhi yake zinasema dhahiri kuwa kufutwa ilikuwa ni siku ya Khaibar; baadhi yake ilikuwa ni siku ya Fat-hi; baadhi yake ilikuwa katika Vita vya Tabuk; zingine zinasema ilikuwa katika Hijjat Alwidai (hija ya mwisho ya Mtume); zingine ilikuwa katika U'mra ya kadha; na zingine (zinasema) ilikuwa katika mwaka wa Autwaas.

Huu ni mgongano ambao utausikia kutoka kwa *Sahihi Bukhari* na *Sahihi Muslim*, kitu ambacho kinajulisha kutokufutwa (kwa ndoa hii), na kwamba uharamu na kukatazwa kwake ni mambo yaliyoletwa na Khalifa wa Pili kwa sababu ya tukio lililotokea la Amru ibn Hariith katika zama zake.

Kabla ya hapo maswahaba walikuwa wakifanya mut’a katika zama za Makhalifa wote wawili, kama walivyokuwa wakiifanya katika zama za Mtume (s.a.w.w). Utakaposikia maneno ya I’mran ibn Haswiin, Abdillah ibn Mas’ud, Abdillah ibn Umar, Abdillah ibn Abbas na Amiril muuminin utayaona wazi kwamba uharamu haukutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu wala kwa Mtume (s.a.w.w), bali ulitokana na makatazo ya Umar.

Na haiwezekani kuwepo chenye kufuta na watu hawa wasikijue na hali wao ni wale ambao utukufu wao katika elimu na daraja yao kwa Mtume, na kudumu kwao pamoja naye kunajulikana, kiasi ambacho lau kungekuwa na chenye kufuta basi baadhi yao wanaolijua hilo wangewatanabahisha, kwa kuwa hakuna aliowapinga walipokuwa wakinasibisha uharamu wa mut’a kwa Umar, tumejua kwamba wao wote wanakubali kuwa hakuna chenye kufuta kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu wala kutoka kwa Mtume (s.a.w.w).

Pia Khalifa wa Pili mwenyewe hakudai kuwa imefutwa, kama utakavyo yasikia maneno yake yaliyo wazi katika kujinasibishia yeye mwenyewe uharamu na makatazo mut’a. Lau kungekuwa na chenye kufuta kutoka kwa Mwenyezi Mungu au kutoka kwa Mtume basi angenasibisha uharamu kwa Mwenyezi Mungu au kwa Mtume, kwa sababu hilo (kunasibisha kwa Mwenyezi Mungu au kwa Mtume) ndilo lenye kufaa zaidi katika kukanya, na ni bora zaidi katika kukumbusha.

Mimi nina shaka kwamba waliokuja baada ya maswahaba waliweka Hadith za kufuta (ndoa ya mut’a) ili wapate kuiswaibisha rai ya Khalifa, kwa sababu yeye alizitafsiri dalili, akakataza na kuharamisha na huku akitishia kuadhibu aliposema: “Mut’a mbili zilikuweko katika zama za Mtume (s.a.w.w) lakini mimi naziharamisha na nitamuadhibu mwenye kuzifanya; nazo ni mut’a ya haji na mut’a ya wanawake.

Na miongoni mwa mambo ya ajabu kabisa ni madai ya baadhi ya wanazuoni waliokuja baadaye kuwa ndoa ya mut’a imefutwa kwa kauli ya

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 68



Mwenyezi Mungu isemayo: **"Na wale ambao tupu zao wamezihifadhi, isipokuwa kwa wake zao au kwa suria waliowamiliki." (23:5-6).** Kwa kudai kwamba mwanamke aliyeolewa ndoa ya mut'a siyo mke wala suria. Wakasema: Ama kwa kuwa siyo suria aliyemilikiwa hilo liko wazi. Na ama kwa kuwa siyo mke ni kwa sababu mwanamke huyo hana lazima ya chakula wala harithi wala hana zamu ya kulaliwa.

**Jibu:** Yeye ni mke wa kisharia kwa ndoa ya kisharia kama ulivyosikia. Ama kuwa hapaswi kupewa chakula, kutorithi na kutokuwa na zamu ya kulaliwa, hayo yanatokana na dalili maalumu ambazo zimehusishwa kutoka katika zile zenye kuzungumzia hukumu za wake kwa ujumla kama tulivyobainisha hapo mwanzo.

Pia aya hii ni ya Makka; ilishuka kabla ya Hijra. Na hili wote wanaliafiki. Kwa hiyo haiwezekani ikawa ni yenye kufuta halali ya mut'a iliyohalalishwa Madina baada ya Hijra, kwa kuafikiwa na wote.

Na miongoni mwa maajabu makubwa ya watu hawa wenye kulazimisha mambo ni wao kusema kwamba aya ya Surat Muuminun inafuta ndoa ya mut'a ya wanawake kwa sababu siyo mke wala siyo kumiliki suria. Sasa je, tukiwauliza wao: Kwa nini aya hiyo haifuti ndoa ya kuwaowa suria waliomilikiwa na mtu mwingine ambaye siyo yule yule muowaji, kwa sababu wao siyo wake wa ndoa wala siyo kumiliki suria? Watajibu wakati huo kuwa Surat Muuminun ni ya Makka, na ndoa ya suria waliotajwa imewekewa sharia kwa neno lake Mwenyezi Mungu katika Surat Nisaa nayo ni ya Madina aliposema:

﴿ وَمَن لَّمْ يَسْتَطِعْ مِنكُمْ طَوْلًا أَن يَنكِحَ ٱلْمُحْصَنَٰتِ ٱلْمُؤْمِنَٰتِ فَمِن مَّا مَلَكَتْ أَيْمَٰنُكُم مِّن فَتَيَٰتِكُمُ ٱلْمُؤْمِنَٰتِ ۚ ﴿٢٥﴾ ﴾

**"Na yule ambaye hawezi miongoni mwenu mahari ya (wanawake) waungwana walio waislamu basi ni waoe suria mliowamiliki" (4:25),**

na aya ya Makka haiwezi kufuta aya ya Madina, kwa sababu aya inayofutwa ni lazima itangulie (kushuka) kabla ya aya ya kufuta. Wao husema maneno haya wanasahau kwamba aya ya mut'a iliteremshwa Madina. Na pia aya yake imo katika Surat Nisaa. Bila shaka sisi tumepewa watu wasiofahamu. Na hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Yeye tutarejea.

## 6. HADITH ZINAMFICHUA KHALIFA

Muslim amepokea katika Mlango wa Mut'a ya Haji na U'mra katika *Sahihi* yake [86] kwa mfululizo wa mapokezi mpaka kwa Abi Nadhra kwamba: Ibn Abbas alikuwa akiamrisha kufanya mut'a na Ibn Zubeir akiikataza; Jaabir akaambiwa mambo hayo, na akasema kuwa mazungumzo hayo yamenifikia na akasema: "Sisi tumefanya mut'a wakati wa Mtume (s.a.w.w), lakini Umar alipokuwa khalifa[87] alisema: "Hakika Mwenyezi Mungu alikuwa akimhalalishia Mtume Wake anachokitaka na atakavyo.[88] Sasa timizeni Haji na U'mra, na acheni ndoa za hawa wanawake kwani sitoletewa mwanamume aliyeoa mwanamke kwa muda maalumu isipokuwa nitamrujumu kwa mawe."[89]

86 Katika uk. 467 Juz. 1 iliyopigwa chapa Misri mwaka 1306 A.H.

87 Yaani alipokuwa khalifa, na hili liko wazi kwa sababu ya matukio haya yafuatayo: kukataza, kuharamisha na kutahadharisha hayakuwepo kabla ya hapo.

88 Laiti mimi au mtu yeyote angejua? Je neno hili lina njia ya kufahamu kuwa mut'a ni haramu? Je unaweza kufahamu kuwa yeye alikuwa anaona kuwa hiyo ni hukumu mahsusi kwa Mtume (s.a.w.w)? Sivyo hivyo, mimi ninamuweka mbali na maana hii.

89 Rajmu ni hukumu miongoni mwa hukumu za Mwenyezi Mungu. Sharia na hiyo haiwekwi na yoyote isipokuwa Mtume. Au mwenye kuihalalilisha mut'a awe ametoa uhalali wake kutoka katika Kitabu (Qur'ani) na Hadith. Kama atakuwa amepata basi atakuwa ametoa kutoka kwenye Qur'ani na Hadith na kama atakuwa amekosa basi atakuwa amedanganyikiwa na hatopigwa hadi lau atafanya kwani, hududi (hukumu) huondoshwa na shubha (udangamanifu).

Na hii ndiyo aliyoipokea Ahmad ibn Hambal katika Hadith ya Umar katika *Musnad* yake.[90] Pia kutoka kwa Abi Nadhra, na tamko lake ni kama ifuatavyo: “Amesema Abi Nadhra: Nimemwambia Jaabir kuwa Ibn Zubeir anakataza mut’a, na Ibn Abbas anaiamrisha. Akaniambia: Haya mazungumzo yamenipitia, Sisi tumefanya mut’a wakati wa Mtume (s.a.w.w), na wakati wa Abu Bakr, lakini alipotawala Umar[91] aliwahutubia watu na akasema: “Hakika Qur’ani ni Qur’ani. Na hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu ni Mtume. Hakika zote (mut’a) mbili zilikuwako katika zama za Mtume (s.a.w.w); mojawapo ni mut’a ya Haji na nyingine ni mut’a ya wanawake.[92]

Hili liko wazi na ni fasaha kwamba makatazo (ya mut’a) yaliletwa na yeye baada ya kutawala na kuwa khalifa. Na mfano wake ni Hadith ya A’twaai iliyopokewa na Muslim katika Mlango wa Ndoa ya Mut’a katika *Sahihi* yake.[93]Amesema: “Jabir ibn Abdillah alikuja kufanya Umra, tukaenda kumuona aliposhukia. Watu wakamuuliza mambo mengi, kisha wakamtaja mut’a. Akasema: Ndiyo tumefanya mut’a katika zama za Mtume (s.a.w.w), Abu Bakr na Umar.” *Mwisho*.

Na Hadith ya Ibn Zubeir kama ilivyo katika *Sahihi Muslim* amesema: “Nilimsikia Jaabir ibn Abdillah akisema: Sisi tulikuwa tukifanya mut’a[94]

kwa teko moja la tende na unga kwa siku kadhaa katika zama za Mtume (s.a.w.w) na Abu Bakr. Kisha Umar akaikataza kwa sababu ya tukio la

90 Uk. 52 wa Juzuu yake ya kwanza.

91. Hili la uharamu wa mut'a alilolitilia nguvu Khalifa katika khotuba yake halikuweko kabla ya yeye kushika utawala.

92. Hakuna nafasi ya kuikubali hii riwaya yake kwa sababu amesema: zilikuwako wakati wa Mtume (s.a.w.w). kwa hiyo yeye kuiharamisha ni maoni yake binafsi aliyokuwa akiyaona.

93 Uk. 535 wa Juzuu yake ya kwanza.

94 Uwazi wa kauli yake: tulikuwa tukifanya mut’a, ni kwamba sera ya maswahaba ilikuwa ikiendelea hivyo na pamoja na kuwa Mtume, Abu Bakr na Umar kabla hajaikataza walikuwa wanajua.

Amru ibn Hariith.” Na katika mlango huo huo wa *Sahihi Muslim* pia, kutoka kwa Abi Nadhira amesema: “Nilikuwa kwa Jaabir akaja mtu mmoja akasema: Hakika Ibn Abbas na Ibn Zubeir wametofautiana kuhusu mut’a mbili. Jaabir akasema: Sisi tumezifanya[95] wakati wa Mtume (s.a.w.w), kisha Umar akazikataza.

Yanajulikana sana maneno ya Umar aliyoyasema, na yeye yuko juu ya mimbari, kuwa: “Zote mut’a mbili zilikuwako wakati wa Mtume (s.a.w.w) na mimi ninazikataza. Na nitamuadhibu mwenye kuzifanya.[96] (Nazo ni) mut’a ya Haji na mut’a ya wanawake.” Hata Ar-Razi ameyanukuu maneno haya kutoka kwa Umar akitoa hoja kwa maneno hayo kuwa mut’a ya wanawake ni haramu. Rudia yaliyomo katika aya yake (mut’a) katika tafsiri yake *Al-Kabir*.

Na huyu hapa Al-Kaushaji, ambaye ni mwanachuoni wa elimu ya Tawhiid katika madhehebi ya Ash’ari, na ni Imam wao katika Al-Maaquul wal-Mankuul, anasema katika mwisho wa kuchambua ni uimamu katika kitabu chake Sherehe ya *Al-Jariid* kwamba Umar alisema na huku yuko juu ya mimbari: Enyi watu! mambo matatu yalikuwako wakati wa Mtume (s.a.w.w) na mimi nawakataza, na nayaharamisha, na nitamuadhibu mwenye kuyafanya, (nayo ni) mut’a ya wanawake, mut’a ya Haji na *hayya a’la khairil amal*.” Na (Al-Kaushaji) amempa udhuru (Umar) kwamba hii ni *ijtihadi* (rai) na ni tafsiri yake. Hadith hizi na zingine katika jambo hili ni nyingi kiasi ambacho ni dhiki kuzitaja katika kitabu hiki.

Rabia’h ibn Umayah ibn Khalfi Al-Thaqafi, ambaye ni ndugu yake Swafwan, alifanya mut’a katika zama za Umar kama ilivyo Hadith iliyotajwa na Maalik katika Mlango wa Ndoa ya Mut’a katika (kitabu) *Al*-

95 Uwazi wa maneno haya tulizifanya: ni kwamba waliendelea kuzifanya mut’a zote mbili kama ilivyo wazi kwa maneno yao: “Tulizifanya” na “Tumefanya mut’a.”

96 Haufichikani uwazi wake kwamba kukataza kumetoka kwake, siyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu wala kutoka kwa Mtume (s.a.w.w).

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 72



*Muwatta*, kutoka kwa Urwa ibn Zubeir amesema: "Hakika Khaulah bint Hakim Al-Samiyah, aliingia kwa Umar na akamwambia: Rabia'h ibn Umayah amefanya mut'a na mwanamke mmoja na akashika mimba (kutokana na mut'a hiyo). Umar akatoka na huku akikokota kishali chake na akasema: Mut'a hii lau ningekuwa nimetangulia (kuikataza) basi ningerujumu," yaani lau ningetangulia kuiharamisha na kuwatahadharisha kuwarujumi wenye kuifanya kabla ya leo basi ningemrujumu Rabia'h na yule mwanamke aliyefanya naye mut'a, kwani maneno haya yalikuwa kabla ya yeye kuikataza. Maneno haya ameyataja Ibn Abdulbar, kwa kunukuliwa na Az-Zarqani katika Sherehe ya *Al-Muwatta*,[97] wala uwazi wa maneno haya haufichikani kwamba huko ni kufanya kazi isiyo yake katika hukumu ya mut'a na ni yeye ndiye aliyefanya hivyo wala hakuna mwingine.

**7. WENYE KUMPINGA UMAR**

Amiril Muuminin Ali alimpinga, katika Hadith ya Tha'labi na Twabari, walipofika katika aya ya mut'a katika tafsiri zao mbili kubwa, walipotaja kwa mapokezi mpaka kwake, kwamba yeye alisema: "Lau si Umar kukataza mut'a basi wasingezini isipokuwa watu wachache."

Na ibn Abbas alimpinga kwa kusema:[98] "Haikuwa mut'a isipokuwa ni rehema ambayo Mwenyezi Mungu amewaruhumia umma wa Muhammad. Lau si yeye - Umar - kuikataza basi wasingehitaji kuzini isipokuwa watu wachache." Hii ni kufuatana na Ibn Kathiir alivyotafsiri neno *shafii* kwa *fai* katika kitabu chake *An-Nihaya*. Ibn Abbas alikuwa akisema jahara kuwa mut'a ni halali, na katika jambo hilo ana hikaya nyingi pamoja na ibn Zubeir - mpaka katika siku za uamiri wake - na ni mambo marefu kuyata-

97 Pale alipokuwa akisherehe Hadith hii katika *Al-Muwattaa*.

98 Kama alivyo mpokea Ibn Jureij na Umar Ibn Dinar.

ja hapa.[99] Na Jaabir alimpinga, kama ulivyosikia katika Hadith yake kuhusu mambo hayo.

Pia mtoto wake Abdallah alimpinga kama ilivyothubutu kwake, kwani amepokea Imam Ahmad katika uk. 95 wa Juzu ya pili ya *Musnad* yake katika Hadith ya Abdallah ibn Umar, kwamba - alipoulizwa kuhusu mut’a ya wanawake - alisema: “Naapa! kwa Mwenyezi Mungu, sisi hatukuwa tunazini katika zama za Mtume wala hatukuwa tunafanya uchafu”, kisha akasema: “Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Hakika nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: Kabla ya siku ya Kiyama atakuweko Masihi Dajali na warongo thelathini au zaidi. Siku nyingine aliulizwa kuhusu mut’a ya wanawake akasema - kama ilivyo katika *Sahihi Tirmidhi*:[100] “Hiyo ni halali.” Akaulizwa tena: Baba yako ameikataza. Akasema: “Unaonaje kama baba yangu ameikataza na Mtume (s.a.w.w) ameifanya, je, tuache sunna na tufuate maneno ya baba yangu?!”

Pia Abdallah ibn Mas’ud alimpinga kama inavyojulikana kutoka kwake, kwani wamepokea masheikhe wawili katika *Sahihi* zao, na hapa namnukuu Bukhari:[101] Kutoka kwa Abdallah ibn Mas’ud kwamba amesema: “Tulikuwa vitani pamoja na Mtume (s.a.w.w) wala hatukuwa na chochote. Tukamwambia: Je, tujihasi? Akatukataza kufanya hivyo. Kisha akatu-ruhusu tuoe mwanamke kwa kumpa nguo kwa muda maalumu. Kisha aka-tusomea:

99 Ninakutanabahisha kwenda kuangalia yale yaliyomo katika uk. 489 wa mjala-da wa 4 wa Sherehe ya *Nahjul Balagh* ya Al-Haamidi Al-Hadidi alipokuwa akimwelezea Ibn Zubeir wakati akisherehe neno la Amir Al-muuminin (a.s): “Bado Zubeir ni katika sisi Ahlul Bayt mpaka akazaliwa mtoto wake mkorofi.”

100 Al-Allama katika Nahju Al-Swidq na Al-Shahid Al-Thani katika Mlango wa Mut’a katika *Raudhwa* yake, wote wamenukuu kutoka kwa Tirmidhi.

101 Katika uk. 2 au uk. 3 katika Mlango wa Nikaha..

﴿ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تُحَرِّمُوا۟ طَيِّبَـٰتِ مَآ أَحَلَّ ٱللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوٓا۟ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ ٱلْمُعْتَدِينَ ﴿٨٧﴾ ﴾

**“Enyi mlioamini, msiharamishe yale mazuri mliohalalishiwa na Mwenyezi Mungu, wala msiruke mipaka, hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kuruka mpaka” (5:87).**

Wewe pia unajua yaliyomo katika aya hii miongoni mwa makatazo makali kutokana na kuiharamisha, kama walivyosema wazi wale waliosherehesha *Sahihi* mbili.

Na I’mran ibn Haswiin alimpinga katika habari zilizoenea sana kutoka kwake, kwani Ar-Razi amemnukuu[102] kwamba yeye amesema: “Mwenyezi Mungu aliteremsha aya kuhusu mut’a wala hakuifuta kwa aya nyingine. Na Mtume (s.a.w.w) alituamrisha tufanye mut’a na wala hakutukataza. Kisha mtu akasema alichokitaka kwa rai yake” Ar-Razi amesema: Alimkusudia Umar.

Na Bukhari amepokea katika *Sahih* yake kutoka kwa I’mran ibn Haswiin amesema: “Aya ya mut’a ilishuka katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na tukaifanya pamoja na Mtume (s.a.w.w) wala haikushuka Qur’ani ili kuiharamisha, wala (Mtume) hakukataza mpaka akafa. Mtu mmoja akasema alichokitaka kwa rai yake.

Na Ahmad amepokea katika *Musnad* yake kutoka kwa Abi Rajai kutoka kwa I’mran ibn Haswiin kuwa amesema: “Aya ya mut’a ilishuka katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na tukaifanya pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wala haikushuka aya yoyote ya kuifuta, wala Mtume hakukataza mpaka akafa.

Maamun katika siku za ukhalifa wake, aliamrisha kutangazwe uhalali wa mut’a. Lakini wakaingia Muhammad ibn Mansur na Abul-Ainaa

102 Alipokuwa akichambua hukumu ya mut’a ya wanawake katika aya yake (mut’a) katika tafsiri yake Al-Kabir.

wakamkuta anapiga mswaki na huku akisema kwa hasira - kama alivyomnukuu Ibn Khalkan :[103] “Mut’a mbili zilikuwako wakati wa Mtume (s.a.w.w) na wakati wa Abu Bakr, na mimi ninazikataza.” Akasema: “Na wewe ni nani, - ewe mweusi kama (mdudu) - mpaka ukataze alichokifanya Mtume wa Mwenyezi Mungu na Abu Bakr.” Hapo Mohammad ibn Mansur akataka kuzungumza naye lakini Abul-Ainaa akamwashiria na akamwambia: Mtu anamzungumza Umar ibn Khattab kama anavyozungumza, sisi tutaweza kuzungumza naye?! Basi hawakuzungumza naye. Na akaingia Yahya ibn Aktham, lakini woga wake ukamwepusha na fitna. Na akaambiwa kuwa watu wanamwona kwamba kwa huku kutangaza kwake amezua kizushi kikubwa sana katika Uislamu, kinachoathiri watu wa kawaida na wale wajuzi, kwani wao hawatofautishi kati ya kutangaza uhalali wa mut’a na kutangaza uhalali wa zinaa. Hayo yaliendelea mpaka akaondosha dhamira yake ili kutetea ufalme na nafsi yake.

Na miongoni mwa watu waliopinga uharamu wa mut’a, wakaihalalisha na wakaifanya, ni Abdul-Malik ibn Abdul-Aziz ibn Juraij Abu Khalid Al-Maki, aliyezaliwa mwaka 80H alikufa mwaka 149H, na alikuwa ni katika wanachuoni wa *taabiina*, ibn Khalkan amemweleza katika kitabu chake *Wafayat*, pia ibn Sa’d amemweleza katika uk. 361 Juz. 5 katika kitabu chake *Twabaqat.* Wenye *sihahi* (vitabu vya Hadith) wamemtegemea. Pia Ibn Qaisarani amemweleza katika uk. 314 wa kitabu chake *Al-Jam’u baina rijali al-Sahihain* na Dhahabi amemtaja katika *Al-Mizani* yake na akasema kuwa yeye alioa karibu ya wanawake tisini (90) kwa ndoa ya mut’a, na yeye alikuwa anaona kuwa (ndoa hiyo) imeruhusiwa, na akasema: “Na alikuwa mwanafiqhi wa watu wa Makka katika zama zake.”

## 8. RAI YA IMAMIYA KATIKA (*NDOA YA*) MUT’A

Imamiya (Shia) wameafikiana - kwa kufuata maimamu wao kumi na mbili - kwamba bado (mut’a) ni halali, na inatosha kwao kuwa ni hoja katika (uhalali wake) yale uliyoyasikia kuhusu kuafikiana watu wa kibla kimoja

103 Katika tarjuma (kumweleza) ya Kadhi Yahya ibn Aktham

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 76



(waislamu wote) kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliiweka kuwa ni sharia katika Dini Yake iliyonyooka na akatoa idhini kwa Mtume Wake Mtukufu airuhusu, na wala haikuthubutu kunasikhiwa (kufutwa) kutoka kwa Mwenyezi Mungu wala kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) mpaka *wahyi* ukakatika kwa Mwenyezi Mungu kumkhitaria Mtume wake nyumba ya ukarimu (Akhera). Bali kutokunasikhiwa kumethubutu kwa nususi (Hadith) kutoka katika Sahihi zetu zilizo *mutawatir* kutoka kwa Maimamu wa kizazi kitakatifu. Zirudie mahala pake, kama kwenye (kitabu) *Wasail al-Shia ila ahkami al-Sharia*.

Isitoshe! katika *sihahi* (vitabu vya Hadith sahihi) za Ahlul Sunna, na vitabu vingine vya Hadith kuna *nususi* (Hadith) zinazosema wazi kwamba uhalali wake ulibakia na uliendelea mpaka katika zama za Abu Bakr na sehemu ya zama za Umar, mpaka yeye akaikataza kwa sababu ya tukio la Amru ibn Hariith. Na yanakutosha katika hayo yale machache tuliyokutajia hapa kwa haraka haraka.

﴿إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَذِكْرَىٰ لِمَن كَانَ لَهُۥ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى ٱلسَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ ٣٧﴾

**"Katika hayo kuna ukumbusho kwa mwenye akili au kutega sikio na yeye ni shahidi." (50:37).**

## KUPAKA MIGUU AU KUIOSHA KATIKA UDHU

Wametofautiana wanazuoni wa Kiislamu kuhusu namna ya kutwaharisha miguu ambayo ni miongoni mwa viungo vya udhu. Wanazuoni wa Jamhuri, wakiwemo miongoni mwao maimamu wanne, wameona kuwa ni lazima kuosha miguu tena ni faradhi *a'ini* (bila hiari). Na Daud ibn Ali na Naswirulil-Haqi, katika maimamu wa Zaidia, wao wamelazimisha kufanya yote mawili: kuosha na kupaka maji.[104] Na huenda kuna aliyesema kuwa

104 Fakhru-Dini Ar-Razi amenukuu kutoka kwao alipokuwa akizungumzia aya ya udhu katika tafsiri yake *Al-Kabir*, kana kwamba wao walichanganyikiwa, na wakawa hawajui wafanye nini, kwa sababu ya mgongano kati ya aya hii na hadithi (za kuosha miguu). Kwa sababu hiyo wakalazimisha kukusanya yote ili kutekeleza zote mbili (aya na hadithi).

ni hiari ya mtu kuchagua moja kati ya hayo mawili.[105] Ama Imamiya wao - kwa kufuata Maimamu wa kizazi kitakatifu - wamesema ni lazima kupaka, tena ni faradhi *a'ini* (bila hiari).[106]

## HOJA YA IMAMIYA

Hoja yao ni neno la Mwenyezi Mungu: **"...na mpake vichwa vyenu na miguu yenu mpaka vifundoni.." (5:6).**

Na anatutosha Imam Ar-Razi katika kubainisha namna ya kutoa hoja kwa aya hii kwa yale aliyoyasema wazi kwa urefu aliposema: "Hoja ya wenye kusema kuwa ni lazima kupaka miguu imejengwa kwa visomo viwili mashuhuri katika neno Lake Mwenyezi Mungu *Waarjulakum*," akasema: "Ibn Kathiir, Hamzah, Abu Amru na Aaswim - kutoka kwa mapokezi ya Abu Bakr - wamesoma kwa *jari* (kasri).

Na Nafi'i, ibn Aamir na Aaswim - kwa mapokezi kutoka kwa Hafsw - wamesoma kwa *nasbi*," akasema: "Tunasema, ama kusoma kwa *jari* (*arjulikum*) hiyo inasababisha kuwa miguu ni *maatufu* (inafuata kihukumu) katika kichwa; kama ilivyo ni lazima kupaka kichwa, pia ni lazima kupaka miguu." Akasema: "Je, kukiulizwa, kwa nini haifai kusema kuwa hii *kasri* (katika *arjuli*) ni *kasri a'la jiwar* (ni *kasri* ya ujirani), kama ilivyo katika maneno ya kiarabu yanayo sema *juhuru dhabi kharibi* na maneno yao *kabiru unasin fi bijadi muzmilin*? Tutasema: hii (hoja) ni batili kwa

105 Kama Al-Hasan Al-Busri na Mohamad ibn Jarir Twabari kwa walivyonukuliwa Ar-Razi na wengine, kana kwamba zote; - Qur'ani na Hadith - ni haki isiyoingiwa na batili, waliona kuwa kuosha na kupaka ni haki, na wajibu ni kimojawapo kwa kuchagua.

106 Na haya ndio madhehebi ya Ibn Abbas, Anas ibn Maalik, I'krimah, Al-Sha'abi na Imamu Abu-Ja'far Al-Baqir, kama alivyotaja Al-Razi katika tafsiri yake kwa kunukuu kutoka kwa tafsiri ya Al-Qafaal. **Ninasema:** na hivi ndivyo walivyosema Maimamu wetu wote (a.s).

sababu nyingi:

**Ya kwanza:** kutia *kasri* kwa ajili ya ujirani huhesabika ni katika makosa ambayo yanaweza kukubalika kwa sababu ya dharura ya kimashairi, na maneno ya Mwenyezi Mungu ni lazima yaepukane na makosa (kama hayo).

**Ya pili:** Ni kwamba kutia *kasri* kwa ajili ya ujirani tu hilo linawezekana panapoaminika kuwa hakuna kudangamanika kama ilivyo katika maneno (ya Kiarabu) *juhru dhabi kharibi* (shimo la mburukenge limeharibika) jambo ambalo liko wazi kwa watu wote ni kwamba kuharibika hakui ni sifa ya mburukenge bali ni sifa ya shimo, na katika aya hii hakuna amani ya kutokutangamanikiwa (ni kupaka au kuosha).

**Ya tatu:** kutia *kasri* kwa ajili ya ujirani, huwa bila ya kuweko herufi ya *atfi*, ama ikiwepo herufi ya *atfi* basi Waarabu hawajawahi kuzungumza hivyo.” Akasema: “Ama likisomwa kwa *nasbi* (*wa arjula*), pia wamesema kwamba inamaanisha kupaka (miguu) kwa sababu (Mwenyezi Mungu) aliposema: “*wamsahu biruusikum*” kwani *ruusi* hapa liko mahala pa *nasbi* na limenasibishwa na *wamsahu* kwa hiyo *ruusi* ni *maf-ulu bihi* lakini kitamko (neno hilo) *limejururishwa* na *albau* kwa hiyo *ikiatfia al-arjul* katika *ruus* inajuzu kunasibisha *arjul* kwa *kuatfia* mahali pa *ruus*[107] na inajuzu *kujururisha* kwa *kuatfia* katika tamko lililo dhihiri.” Akasema: “Na hili

[107]Na hivi ni mara nyingi katika maneno, kwani wanasema *laisa fulanu bia’limi wala a’milan* na wengine wameimba: *Mua’wiya innana basharun fasjah falasna biljibali walal hadida* na amesema Taabatwa-Shara: *hal anta baaithu dinari lihajatina au a’bda rabbi akha A’uni ibn Mihraq* kwa kunasibisha a’bda kwa sababu ya kuatfia katika mahala pa dinari.

likithubutu, tutasema: Imedhihiri kwamba, kilichotenda kazi katika *waarjulakum* inajuzu kiwe ni neno lake *wamsahu*,**[108]** na inajuzu kiwe ni neno lake *faghsilu*,**[109]** lakini vitendakazi viwili vinapopambana katika kitendwakazi neno moja, basi kukifanyisha kazi kile kilicho karibu ndio bora."**[110]** Akasema: "Kwa sababu hiyo inalazimu kwamba kitendakazi cha *nasbi* katika neno lake *waarjulakum* ni neno lake *wamsahu*." Akasema: "Kwa sababu hiyo kunakuwa kusoma *waarjulakum* kwa *nasbi* katika *lamu*, vile vile inalazimu kupaka." Akasema: "Kisha wamesema: Wala haijuzu kuyabatilisha haya kwa Hadith (zinazojulisha kuosha) kwani zote ziko katika Mlango wa Hadith *Aahadi* (hazikupokewa kwa wingi) na kufuta Qur'ani kwa Hadith ambayo ni katika *Aahadi* haifai."**[111]** **mwisho wa kumnukuu**.

Haya ni maneno yake kwa kumnukuu**[112]** na wala hakutia kitu, lakini alisema: "Hakika kuna Hadith nyingi zilizopokewa kulazimisha kuosha, na kuosha ndani yake kuna kupaka na siyo kinyume chake. Kwa hiyo kuosha, kuko karibu sana na kutoka shakani basi ni lazima tufanye hivyo."**[113]** Akasema: "Na kwa maana hii ni lazima tujue kwamba kuosha miguu

---

108 Bali hilo ni lazima, kwani haijuzu kwamba kitendakazi kiwe ni *faghsiluu* kama utakavyosikia.

109 Kwani hivyo haifai kabisa, kwa sababu inasababisha kuatfia *arjul* katika *ujuuhi*, na hilo ni jambo lisilowezekana kwa itifaki ya wataalamu wa lugha, kwa sababu haijuzu kupambanua kati ya *al-a'tif* na *al-ma'tuf alaih* (chenye kuatfia na chenye kuatfiwa) kwa neno moja licha ya jumla nzima nyingine ya maneno.

110 Hapa hakuna isipokuwa ni kitendakazi kimoja tu, nacho ni *wamsahu* kama tulivyobainisha.

111 Na hilo ni jambo ambalo halikuthubutu kabisa kwetu.

112 Yarudie katika uk. 370 Juz. 3 katika tafsiri yake Al-Kabir alipokuwa akieleza aya ya udhu katika Surat Al-Maidah.

113 Kutoka shakani (*ihtiyat*) haiwezi kupatikana mpaka kwa kufanya yote mawili; kupaka na kuosha kwa sababu yote mawili ni vitu viwili tofauti - wala haiwezekani kuvikusanya pamoja.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 80



kunasimama mahala pa kupaka…" **mpaka mwisho.**

**Nasema:** kuhusu Hadith za kuosha, utaijua rai ya Maimamu wa Ahlul-Bayt na wafuasi wao hivi karibuni Inshallah Taa'la.

Ama kauli yake kuwa ndani ya kuosha kuna kupaka, huku ni kupotosha kuliko wazi kabisa, bali hivyo ni vitu viwili tofauti kilugha. Kikawaida na hata kisheria.**[114]** Kwa hiyo kinachofahamika ni kwamba kuosha miguu hakusimami mahala pa kuipaka.

Lakina Imamu Ar-Razi alisimama (njia panda) kati ya matatizo mawili; nayo ni kuhalifu aya iliyohakimika (wazi) na kuhalifu Hadith zilizosahihi kwa maoni yake. Kwa sababu hiyo akaidanganya nafsi yake, kwa kusema kuwa ndani ya kuosha kuna kupaka. Na kwamba kuosha ni karibu sana na *ihtiyaat* (kutoka shakani) na kwamba, kunasimama mahala pa kupaka, kwani yeye alidhani kwa kufanya hivyo atakuwa amekusanya (amezitekeleza zote mbili) aya na Hadith. Na mwenye kuzingatia vizuri katika huku kujitetea kwake atampata alikuwa hajui afanye nini. Kwani lau si hii aya kuwa iko wazi katika kujulisha lazima ya kupaka asingehitajia kusema kuwa kuosha kunasimama mahala pa kupaka. Zingatia na taamali haya kwa undani.

Na kwa njia hii wamepita wanafiqhi waliobobea na wataalamu wa lugha, miongoni mwao ni mwanafiqhi mchambuzi Sheikh Ibrahim Al-Halabi alipoichambua aya hii katika Mlango wa Udhu katika kitabu chake *Ghuniyatul Mutamali fi Shereh Mughniyatil Muswalli alal Madhhabil Hanafi* amesema: "Imesomwa (aya hii) katika visomo saba kwa *nasbi* na kwa *jarri*, na iliyomashuhuri ni kwamba kusoma kwa *nasbi* ni kwa kuwa ni *ma'tufu* katika *ujuhu* na kusoma kwa *jarri* ni kwa sababu ya ujirani."

114 Kwani kuosha kumechukuliwa kwa maana yake nayo ni kuchurizisha maji japo ni machache juu ya chenye kuoshwa, na kupaka kumechukuliwa kwa maana yake nayo ni kutokuchurizisha maji na kutosheka na kupitisha mkono (wenye unyevunyevu) juu ya chenye kupakwa.

Akasema: “Na iliyo sawa ni kwamba *arjul* ni *ma’tuf* katika *ruus* kwa visomo vyote viwili; kuifanya *nasbi* ni (*ma’tuf*) katika mahali (*pa nasbi*) na kwa *jarri* ni (*ma’tuf*) katika tamko.”

Akasema: “Na hayo yote ni kwa sababu ya kutokufaa *kuatifia* katika *ujuhakum* kwa sababu kuna kipambanuzi ambacho ni sentesi tofauti kati ya chenye kuatufia na chenye kuatufiwa juu yake, nacho ni *wamsahu biruusikum*.” Akasema: “Na katika misingi ya lugha ni kusipambanuliwe kati yao kwa neno licha ya sentesi nzima.” Akasema: “Wala hatujasikia katika fasaha ya lugha; *dharabtu Zaidan wamarartu bi Bakrin wa A’mra* yaani kwa kuatfia A’mran katika Zaidan.” Akasema: “Ama kuifanya ni *jarri* kwa ujirani, hiyo huwa lakini ni kwa uchache sana katika *naa’t* (sifa) kama walivyosema baadhi ya yao: *hadha juhru dhabin kharibin* na katika *taakidi* (kukokoteza) kama alivyosema mshairi: *ya swahi balligh dhawil zaujaati kullihim, in laisa waswala idhaan halat a’ra aldhamb* kwa kutia *jarri* kwenye *kulihim* kama alivyotoa hikaya Alfarai.” Akasema: “Na ama katika *a’tfi nasaq* haiwezekani *a’tfi* (ya ujirani) kwa sababu chenye kuatfia kinazuia mjawara (ujirani).” Haya ndio maneno yake kwa kumnukuu.[115]

Na miongoni mwa waliopita njia hii ya wazi ni Abul-Hasan Imam Muhammad ibn Abdul-Hadi anayejulikana kwa jina la Al-Sindi katika hashia (maelezo) yake juu ya *Sunan ibn Majah* aliposema: - baada ya kukata kwamba dhahiri ya Qur’ani ni kupaka - “Hakika si jambo lingine kupaka ndiyo dhahiri ya Qur’ani, kwa sababu kusoma kwa *jarri* ndiyo dhahiri yake, na kukifanya kisomo kwa *nasbi* kwa *kuatfia* katika mahali (pa *nasbi*) ndiyo kukokaribu sana kuliko kuchukua kisomo cha *jarri* badala ya *nasbi*, hivi ni kama walivyosema wazi Wananahau.” Akasema: “Kwa sababu *kuatfia* kwa ujirani ni kuepuka misingi, na *kuatfia* katika mahali ndiyo kufuata misingi.” Akasema: “Pia kufanya hivyo ni kujiepusha na kipam-

115 Kirudie, uk. 16 wa *Ghiniyat Al-Mutamali* kinachojulikana kama *Halabiyun Kabir*. Pia kinapatikana katika mukhtasari yake inayojulikana kama *Halabiyun Swaghir* na vitabu vyote viwili vimepigwa chapa na ni mashuhuri.

banuzi cha sentensi mbali kati ya chenye *kuatfiwa* na chenye *kuatfiwa* juu yake. Kwa sababu hiyo, kukawa dhahiri ya Qur’ani ni kupaka.” Haya ndiyo maneno yake.[116] Lakini yeye kama mwingine, amelazimisha kuipondoa Qur’ani kwa Hadith zilizosema wazi kuosha.

Imam Zamakhshari alitoa falsafa zake katika kitabu chake *Al-Kashaf* kuhusu aya hii aliposema: “Miguu ni miongoni mwa viungo vitatu vyenye kuoshwa na huoshwa kwa kunyunyizia maji juu yake, kwa sababu hiyo kukawa kuna uwezekano sana wa kufanya *israfu* (kutumia maji kwa fujo), ambayo ni kitu kibaya kilichokatazwa, kwa hiyo (miguu) *ikaatfiwa* katika kiungo cha tatu (kichwa) chenye kupakwa na si kwa ajili kipakwe, bali ili ipatwe kutanabahishwa ule ulazima wa kutumia kwa uchache katika kunyunyizia maji juu yake.” Na akasema: “Na kumesemwa mpaka katika macho (ya miguu) yaani kumetajwa mpaka ili kuondoa dhana za wenye kuhesabu kuwa ni kiungo cha kupakwa, kwa sababu kupaka hakukuwekewa mipaka katika sharia.” **- Mwisho wa kunukuu.**

Hii ndiyo falsafa yake ya *kuatfia arjul* (miguu) katika *ruus* (vichwa) na (ndiyo falsafa yake) ya kutaja mpaka wa miguu. Hayo ni kama uonavyo, si chochote katika kutoa hukumu za kisharia katika aya ambayo iko wazi. Wala si chochote katika kuitafsiri. Wala aya haijulishi chochote katika hayo anayoyadai kuwa inajulisha, bali huko ni kujihukumia kwa kufanya bidii ili kuilinganisha aya na madhehebi yake, badala ya kutoa madhehebi kutoka katika dalili (aya), kwani ameshangaza sana katika kupiga ramli kwake huku, kiasi ambacho hakuna atakayemsikiliza isipokuwa ni kwa yule ambaye kwake kuosha miguu ni kitu kinachojulikana sana, wala hakuna shaka. Ama ikiwa ni mahala penye ugomvi (upinzani), haziwezi

116 Katika taaliki (maelezo) yake kuhusu zile (Hadith) zilizokuja kuhusu kuosha nyayo mbili uk. 88, Juz. 1 ya sherehe ya *Sunan ibn Majah*. Na wale waliosema wazi kama walivyosema wazi Ar-Razi, Al-Halabi na Al-Sindi ni wengi hatuwezi kuwadhibiti, bali wanatutosha hawa maimamu watatu. Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.

kumsaidia dalili hizi chochote, hususan pamoja na wao wamekubali kuwa Qur'ani iko wazi katika ulazima wa kupaka (miguu). Yatutosha katika hilo, yale yanayoelezwa na misingi ya lugha ya Kiarabu kwamba *atfi* ya *arjul* (miguu) iko katika *ruus* (vichwa) vyenye kupakwa na hiyo ni kwa *ijmaa* (itifaki) kwa *nassi* (dalili) na kwa *fatwa*.

## UCHUNGUZI WA HADITH ZA KUOSHA

Hadith za kuosha ziko kwenye vigawanyo viwili; kigawanyo cha kwanza ni zile ambazo hazijulishi kuosha, kama Hadith ya Abdallah ibn A'mru ibn Al-a'swi aliposema: - kama ilivyo katika Sahihi mbili: "Mtume (s.a.w.w) alikuwa nyuma yetu katika safari tuliyosafiri naye. Kisha akatukuta na wakati wa swala ya alasiri umeingia. Sisi tukawa tunapaka juu ya miguu yetu. (Mtume) akanadi: "Maangamizo makubwa ya moto yawe juu ya wenye visigino."[117]

Hadith hii kama itaswihi, basi inajulisha kupaka, kwani Mtume hakuwapinga kupaka bali aliwaacha vile vile kama unavyoona. Isipokuwa yeye aliwakataza uchafu wa visigino vyao. Wala si ajabu, kwa sababu miongoni mwao kulikuwa na watu wa vijijini wanaotembea bila viatu, wajinga na wenye kukojoa kwenye visigino vyao hususan wakiwa safarini. Kwa sababu hiyo (Mtume) akawakhofisha moto ili wasiingie katika swala pamoja na visigino hivyo vilivyo najisika.

Na miongoni mwa Hadith hizo ni zile zenye kujulisha kuosha; kama Hadith ya Himran aliyekuwa mtumwa wa Uthman ibn Affan, aliposema: "Nilimwona Uthman alikuwa amemiminia maji mikono yake kutoka kwenye chombo na akaiosha mara tatu, kisha akatia mkono wake wa kulia katika chombo kisha akasukutua, akapandisha maji puani na kuyatoa...".

117 Maneno haya - maangamizo makubwa ya moto yawe juu ya wenye visigino - pia yametajwa katika Hadith za wote akina; A'mru, A'isha na Abu Hurairah, nazo ni sahihi kwa masharti ya mashekhe wawili.

Mpaka mwisho wa Hadith.[118]

Na kumetajwa katika Hadith hiyo: "Kisha akaosha kila mguu mara tatu. Kisha akasema (Uthman): Nimemuona Mtume (s.a.w.w) akitawadha kama huu udhu wangu.

Na mfano wa Hadith hii ni Hadith ya Abdallah ibn Zaid ibn A'swim Al-Answari wakati alipoambiwa: Tawadha mbele yetu udhu wa Mtume (s.a.w.w). Akaomba chombo (cha maji), akayatia kidogo katika mikono yake..." Hadith ikaendelea.[119] Na mwisho wake ikasema: "Kisha akaosha miguu yake mpaka katika fundo mbili." Kisha akasema (Abdallah): Hivi hivi ndivyo ulivyokuwa udhu wa Mtume (s.a.w.w)." Kuna na Hadith zingine zilizokuja kwa maana hii.

Katika Hadith hizi kuna uchunguzi kwa njia nyingi:
**Ya kwanza**: Hadith hizi ziko kinyume na Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na ni kinyume na walivyokongamana maimamu wote wa kizazi kitakatifu.[120] Na Qur'ani na hiki kizazi ni vizito viwili vya Mtume (s.a.w.w) ambavyo haviwezi kuepukana abadani, na umma hauwezi kupotea maadamu umeshikamana navyo (hivyo vizito viwili). Basi na chochote kinachokwenda tofauti na hivyo vizito viwili kipigwe na ukuta (hakina maana).
Inakutosha katika kupinga kuosha na kuonyesha udhaifu wa Hadith zake, ile Hadith iliyopokewa kutoka kwa mjuzi wa huu umma na mfasiri wa Qur'ani na Hadith naye ni Abdallah Ibn Abbas alipokuwa akitoa hoja juu ya kupaka kwa kusema:[121] "Mwenyezi Mungu amefaradhia kuosha mara

118 Ameipokea Bukhari

119 Ameipokea Muslim.

120 Wote (a.s) wameafikiana juu ya ulazima wa kupaka, na nususi (dalili) zao ni hizo katika (kitabu) *Wasail Shia ila Ahkamus Sharia* na katika vitabu vingine vya fiqhi yao na Hadith zao.

121 Kama ilivyo katika uk. 103 Juz. 5 ya *Kanzul U'mal* nayo ni Hadith ya 2213

mbili na kupaka mara mbili, je wewe huoni kuwa yeye ametaja tayamum, na akafanya mahali pawili katika udhu ni pa kupaka (katika tayamum) na akaacha mahala pawili panapopakwa katika udhu." Na alikuwa akisema (Ibn Abbas):[122] "Udhu ni kuosha mara mbili na kupaka mara mbili."[123]

Na alipofikiwa na habari kuwa Al-Rabi'i bint Mu'wadh ibn A'frai Al-Answariya (mwanamke wa kianswar) kwamba anadai kuwa Mtume (s.a.w.w) alitawadha nyumbani kwake na akaosha miguu miwiwli, alikwenda (Ibn Abbas) kumuuliza kuhusu habari hiyo, na alipomhadithia hivyo akasema (Ibn Abbas) - bila kusadiki bali alimkaripia na kumtolea hoja - "Hakika watu wamekataa isipokuwa ni kuosha na mimi sipati katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu isipokuwa ni kupaka.[124]

**Ya pili**: Hadith hizi lau zingekuwa ni kweli, basi zingekuja kwa wingi kufikia daraja ya *tawatur* kwa sababu haja ya kujua twahara ya miguu katika udhu ni haja ya watu wote wa umma; wanaume na wanawake wake, waungwana na watumwa wake, na ni haja yao kubwa sana katika kila mchana na usiku. Lau kungekuwa na lingine ambalo si kupaka kulikojulishwa na hukumu ya aya, basi watu wote wenye kutekeleza wangekijua katika zama za Mtume na hata baada yake, na lingekuwa ni jambo linalojulikana sana kwao, na Hadith zake zingepokewa kwa wingi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) katika kila zama na kila sehemu, wala kusingebakia nafasi ya kulipinga wala kulititilia shaka. Lakini maadamu jambo lenyewe halikuwa hivyo, basi inatudhihirikia udhaifu wenye kuziangusha hizo Hadith kutoka katika daraja ya kuzingatiwa.

122 Kama ilivyo katika uk. 103 Juz. 5 ya *Kanzul U'mal* nayo ni Hadith ya 2211.

123 Imam Sharif Bahrul Uluum amechukua kutoka katika Hadith hii katika kitabu cha mashairi ya kifiqhi (*Durat Al-Najaf*) aliposema: udhu kwetu sisi ni majosho mawili, na kupaka mara mbili na kitabu kiko pamoja na sisi, na kuosha ni uso na mikono, na kupaka ni kichwa na miguu.

124 Ameipokea ibn Majah katika Hadith zilizoeleza kuosha miguu katika *Sunan* yake na wengine wengi miongoni mwa wapokezi wa Hadith.

**Ya tatu**: Hadith zinazoeleza namna ya kutwaharisha miguu zinagongana. Baadhi yake zinajulisha kuosha, kama Hadith mbili za Hamran na ibn A’swim na umezisikia. Na zingine zinajulisha kupaka, kama Hadith iliyopokewa na Bukhari katika *Sahihi* yake. Zikapokewa na Ahmad, Ibn Abii Shaibah, Ibn Abii Umar, Al-Baghawi, Twabrani na Al-Mawardi wote wamepokea kutoka njia moja ambayo wapokezi wake wote ni wakweli,[125] kutoka kwa Abil-Aswad kutoka kwa U’bad ibn Tamim kutoka kwa baba yake amesema: “Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akitawadha na akipaka maji miguu yake.” Na ni kama Hadith iliyopokewa na Sheikhe katika Sahihi kutoka kwa Zurarah na Bakiir wote ni watoto wa A’yun kutoka kwa Al-Baqir (a.s) kwamba yeye alitoa hikaya ya udhu wa Mtume (s.a.w.w) na akapaka maji kichwa chake na miguu yake mpaka kwenye fundo mbili kwa mabaki ya maji yaliyobaki katika viganja vya mikono na wala hakuchukua maji mapya.

Na kutoka kwa Ibn Abbas kwamba yeye alitoa hikaya ya udhu wa Mtume (s.a.w.w) (Mtume) akapaka maji - kama ilivyo katika *Majma’al Bayaan* - katika miguu yake. Maadamu Hadith zinagongana, basi marejeo yetu ni kitabu cha Mwenyezi Mungu wala hatuwezi kukiacha na kutafuta kitu kingine.

## UCHUNGUZI JUU YA KUTOA KWAO HOJA HAPA KWA *ISTIHSANI*

Huenda Jamhuri (Ahlul sunna) wametoa hoja juu ya kuosha miguu kwa sababu wao wameliona ndiyo linalonasibiana sana na miguu miwili kuliko kupaka maji. Kama ilivyo kupaka kunanasibiana zaidi na kichwa kuliko kuosha, kwani kwa kawaida miguu haitakasiki kutokana na uchafu wake isipokuwa ni kwa kuosha, kinyume na kichwa ambacho mara nyingi hutakasika kwa kupangusa tu kwa maji.

125 Ibn Hajar amewasifu wote kuwa ni wakweli, alipoleta Hadith hii katika kumweleza Tamimi ibn Zaid katika sehemu ya kwanza ya *Al-Iswaba* kwa kunukuu kutoka kwa hawa tuliowataja miongoni mwa wapokezi wa Hadith.

Na wamesema kwamba; Masilahi yenye kukubalika kiakili hayazuiliki kuwa ndio sababu ya ibada zilizofaradhiwa, kiasi ambacho anakuwa mwenye kuweka sharia amechunga maana mbili: Maana ya kimasilahi na ya kiibada, na wanakusudia maana ya kimasilahi yale mambo yenye kuonekana faida zake kwa hisia, na maana ya kiibada yale mambo yenye faida katika kutakasa nafsi.

**Ninasema:** sisi tunaamini kwamba mwenye sharia Mtukufu (Mwenyezi Mungu) amewachunga waja wake katika kila takilifu za hukumu za kisharia. Kwani yeye hakuwaamrisha isipokuwa ni kufanya yale yenye masilahi kwao. Wala hakuwakataza jambo isipokuwa ni kutokana na uovu wake kwao. Lakini pamoja na hayo hakuzijaalia rai za waja wake kujulisha kwamba hukumu fulani imefungamanishwa na masilahi fulani au uovu fulani. Bali Yeye (Mwenyezi Mungu) amewalazimisha wao kufanya ibada kwa dalili zenye nguvu alizowawekea, wala hakuwaachia nafasi ya kuliacha hilo na kuliendea jambo lingine. Na dalili za kwanza kabisa zenye kuhukumu ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtakatifu, naye (katika kitabu chake) amehukumu kupaka maji vichwa na miguu katika udhu, wala hakuna nafasi ya kutupa hukumu yake. Ama kutakasa miguu kutokana na najisi hilo halina budi lipatikane kabla ya kupaka maji katika miguu, hivyo ni kutekeleza dalili mahasusi zilizojulisha, kwani ni sharti kutwaharisha viungo vya udhu kabla ya kuingia katika udhu.[126] Na huenda Mtume (s.a.w.w) aliosha miguu yake - kama ilivyodaiwa katika Hadith za kuosha - si kwa jambo lingine isipokuwa ni kwa mlango huu, na huenda ilikuwa ni kwa sababu ya kujiburudisha au ni kwa sababu ya kujisafisha sana kwake, baada ya kumaliza kutawadha. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye mjuzi zaidi.

126 Kwa sababu hiyo utawaona wenye miguu mitupu miongoni mwa Mashia na wenye kufanya kazi kama wakulima na mfano wao miongoni mwa wale watu ambao huwa hawajali utwahara wa miguu yao katika nyakati ambazo siyo za ibada ambayo haikushurutishwa twahara, wanapotaka kutawadha wanaosha miguu yao, kisha wanatawadha kwa kupaka maji juu ya miguu yao iliyokuwa safi na mikavu.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 88



## UZINDUSHI

Amepokea Ibn Maja miongoni mwa Hadith zilizokuja kuhusu kuosha miguu katika *Sunan* yake kwa njia ya Abu Is-haq kutoka kwa Abu Hayyah, amesema: “Nilimuona Ali (a.s) akitawadha na akaosha miguu yake mpaka kwenye fundo mbili, kisha akasema nimetaka kuwaonyesha nyinyi twahara ya Mtume wenu (s.a.w.w).

Al-Sindi alipofika katika Hadith hii katika sherehe yake juu ya *Sunan Ibn Maja* alisema: “Haya ni majibu makali kwa Shia ambao wanasema miguu hupakwa maji kwani kuosha kumepokewa kwa riwaya ya Ali (a.s).” Akasema: “Kwa sababu hiyo mtunzi (Ibn Majah) ameitaja Hadith hii kwa mapokezi ya Ali na akaanza Mlango kwa Hadith hiyo. Mtunzi amefanya vizuri sana kwa kuleta Hadith ya Ali katika Mlango huu, Mwenyezi Mungu atamlipa malipo ya kheri.” Akasema: “Na dhahiri ya Qur’ani inajulisha kupaka maji kama ilivyokuja kutoka kwa Ibn Abbas, kwa hiyo ni lazima kuitafsiri kwa kuosha.”[127] Haya ndiyo maneno yake kwa kumnukuu. Mwenyezi Mungu amsamehe yeye, Imam Ibn Majah na wengine miongoni mwa wanazuoni wa Jamhuri, kwa sababu wao wanajua kuanguka kwa Hadith hii kwa sababu ya kuanguka sanadi yake kwa namna nyingi:

**Ya kwanza**: Huyu Abu Hayyah aliyepokea Hadith hii ni miongoni mwa wasiojulikana sana, kwani Al-Dhahabi amemtaja katika *Alkuna* ya *Mizani* yake na akasema wazi kuwa hajulikani. Kisha imenukuliwa kutoka kwa Ibn Al-Madini na Abulwalid Alfardhi maneno yaliyo wazi kuwa ni *majhuli* (hajulikani). Kisha akasema: “Na amesema Abu Zar-ah: Hajulikani.”

**Nasema:** nimemtafiti sana huyu Abu Hayyah na utafiti wangu haukunipa faida isipokuwa ni kuzidisha kutokumjua tu. Huenda wala si jambo lingine huyu mtu ametengenezwa na wale waliozua Hadith hii. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiyo Mjuzi zaidi.

127 Kwa kulinganisha Qur’ani na madhehebi yake badala ya kutoa madhehebi (yake) kutoka katika Qur’ani.

**Ya pili**: Hakika Hadith hii imepokewa na Abu Is-haq[128] peke yake na alikuwa amekuwa mzee sana, mwenye kusahau na kuchanganyikiwa na mambo, na watu wakamuacha,[129] na hawakupokea kutoka kwake isipokuwa ni huyu Abu Al-Ahwas na Zuhair ibn Mua’wiyah Al-Ja’fi[130] na watu wakawaona wamefanya aibu kwa kufanya hivyo.[131] Wala si ajabu kwamba mwenye kupokea Hadith akichanganyikiwa na mambo, Hadith zake ambazo hazijulikani kuwa alizipokea kabla ya kuchanganyikiwa zinaanguka (hazikubaliki). Sawa sawa ziwe zinajulikana kuwa alizipokea baada ya kuchanganyikiwa kama Hadith hii, au ikawa haijulikani tarehe ya kupokewa kwake. Kwa sababu *elmu ijmali fi shubuhatil almahasura* (istilahi ya usul) husababisha ikawa ni lazima kuepuka sehemu zote, kama ilivyoelezwa katika elimu ya *usulul Fiqih*.

**Ya tatu:** Hadith hii inapingana na Hadith zilizothubutu kutoka kwa Amiril Muuminin Ali na kutoka kwa watoto wake walio Maimamu ambao ni watu wa nyumba ya Utume, mahala pa risala, mashukio ya malaika, na wahyi na uteremko (wa Kitabu). Pia Hadith hii inapingana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi Hadith hii ipigwe na ukuta.

127. Kama alivyosema wazi Al-Dhahabi alipomzungumza Abu Hayyah katika *Alkuna* ya mizani yake akasema: “Abu Is-haq ni yeye peke yake aliyepokea habari ya Ali kuwa alipaka maji kichwa na akaosha miguu mpaka katika fundo mbili mara tatu tatu.

129. Kama ilivyotajwa katika hali zake - na jina lake ni Umar ibn Abdallah Al-Sabi’i - katika vitabu vya kueleza sera za wapokezi kama *Miizanil-Itidaali* na vitabu vingine.

130. Kama alivyosema wazi Al-Dhahabi alipomtaja Abu Hayyah na hii Hadith yake katika *Mizanil-itidaal*.

131. Mpaka Imam Ahmad amesema alipomtaja Zuheir ibn Mua’wiyah: yeye anadhibiti yale anayoyapokea kutoka kwa mashekhe. Akasema: na Hadith zake kutoka kwa Abu Is-haq zina upungufu kwa sababu amezisikia kwake mwisho wa maisha yake. Mwisho. Na amesema Abuzar-a: Zuheir ibn Mua’wiyah ni mkweli isipokuwa yeye amepokea kutoka kwa Abu Is-haq baada ya kuchanganyikiwa kwake. Mwisho. Na Al-Dhahabi amesema - baada ya kunukuu kutoka kwa Ahmad na Abu Zar-a uliyoyasikia: **Nasema:** Riwaya zake kutoka kwa Abu Is-haq hazina nguvu na (udhaifu) ni kutoka kwa Abu Is-haq wala sio kutoka kwake.

# MPAKA KATIKA FUNDO MBILI

Fundo mbili katika aya ya udhu ni miungano miwili kati ya miundi miwili na nyayo mbili,[132] haya ni kwa hukumu sahihi. Imepokewa kutoka kwa Zurarah na Bakiir ambao ni watoto wawili wa A'yun pindi walipomuuliza Imam Al-Baqir kuhusu hizo fundo mbili,[133] na ndiyo iliyo wazi katika Hadith aliyoipokea Swaduq pia kutoka kwake.[134] Pia maimamu wa lugha wameeleza wazi kuwa kila makutano ya mifupa ni *ka'bi* (fundo).[135]

Na Jamhuri wamekwenda (wamesema) kwamba *ka'bain* (fundo mbili) hapa si lingine isipokuwa ni mifupa miwili iliyoota pembezoni mwa kila muundi. Na wametoa hoja kwamba lau *ka'bi* ingekuwa ni maungano ya muundi na unyayo, basi kungekuwa katika kila muundi kuna *ka'bi* moja tu. Na hii ilikuwa inatakikana aseme (Mwenyezi Mungu): Na miguu yenu mpaka kwenye fundo (nyingi), kama ilivyo kwamba, kulipokuwa kwenye mkono kuna *mirfaq* (kiko) kimoja, alisema (Mwenyezi Mungu) na mikono yenu mpaka katika viko (kwa wingi).

**Nasema:** Lau (Mwenyezi Mungu) hapa angesema: mpaka katika viko viwili ingefaa bila shaka, na maana yawe: "Osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka katika viwiko viwili vya kila mmoja wenu na mpake maji

132 Kuna kauli kuwa ni mifupa ya nyayo, na kauli ya kwanza ndiyo ya ihtiyatwi na yenye nguvu.

133 Katika Hadith iliyopokewa na Sheikh Tusii kwa sanadi sahihi kutoka kwao, na walimwambia Imam: ziko wapi ka'bi (fundo) mbili? Akasema (a.s) ni "hapa" yaani maungano yaliyo chini ya muundi.

134As-Swaduq amepokea kutoka kwa Al-Baqir alipotoa hikaya ya udhu wa Mtume (s.a.w.w) akasema: "Na akapaka maji mbele ya kichwa chake na juu ya nyayo zake bila ya kupaka mifupa ya miundi yake.[134] Kamusi za lugha zinatangaza hivyo hivyo, zirudie.

135. Kamusi za lugha zinatangaza hivyo hivyo, zirudie.

vichwa vyenu na miguu yenu mpaka katika *ka'bi* (maungano) mbili za kila mmoja wenu." Kwa hiyo uwili wa haya maneno mawili (*mirfaq na ka'bi*) na wingi wake katika hii aya ni sawa sawa katika usahihi. Vile vile (ni sawa sawa) wingi wa moja wapo na uwili wa lingine, huenda kuwa ni uhodari wa upangaji wa lugha ulisababisha hivyo.

Hii ni ikiwa katika kila mguu kuna *ka'bi* moja, ama katika kila mguu kukiwa kuna *ka'bi* mbili basi maneno yao hayatokuwa na nafasi. Na wataalamu wote wa upasuaji wamesema kuwa, chini ya muundi kuna mifupa ya mviringo kama mifupa ya mviringo ya ng'ombe na mbuzi pale ambapo kuna kiungio kati ya muundi na unyayo. Pia huitwa *ka'bi* (fundo).**136** Kwa hiyo kupaka maji kila miguu kunaishia katika *ka'bi* mbili nazo ni kiungio chenyewe na mfupa wa mviringo ulio ndani ya hicho kiungio. Na kutaja uwili wa *ka'bi* katika aya na bila kutaja uwili katika *mirfaq* (kiko), hii inaonyesha kuwa kuna jambo muhimu sana na ni ishara ya kuonyesha kuwa kuna mambo yasiyojulikana isipokuwa ni kwa wataalamu wa upasuaji tu. Utakatifu wote ni wa Muumba aliye Mjuzi sana na Mwenye hekima nyingi.

---

136 Muhamad ibn Hasan Al-Shaibani na Al-Asmay'i wamesema kuwa ka'bi (fundo) katika aya ya udhu, si lingine isipokuwa ni huu mfupa ulioko chini ya muundi. Huyu Al-Asmay'i alikuwa akisema: "Hii mifupa miwili iliyoota pembeni mwa muundi inaitwa alminjamain" Ar-Razi alidhania kuwa haya ndiyo madhehebi ya Imamiya hapo ndiyo akawajibu wao kwa kuwaambia kwamba: "Mfupa wa mviringo ulioko chini ya muundi ni kitu kilichofichikana wala hawakijui isipokuwa wapasuaji, kinyume na mifupa miwili iliyoota pembeni mwa kila muundi kwani hiyo ni kitu kinachoonekana." Akasema: "Na mategemezi ya takilifi zote (za Mwenyezi Mungu) ni lazima ziwe ni mambo ya wazi sio yaliofichikana.

**Jawabu lake:** ni kwamba, Ar-Razi alipoona Imamiya wanapaka maji mpaka kwenye kiungo cha muundi, alidhani kuwa wao wanasema kama anavyosema Al-Shaibani na Al-Asmay'i, na wala hakujua kuwa ka'bi kwao ni kiungo chenyewe ambacho ni chenye kuhisiwa na kinajulikana kwa kila mtu.

## KUPAKA MAJI JUU YA KHOFU NA SOKSI

Wanafiqhi wa Kiislamu wamehitalifiana hitilafu kubwa sana katika kupaka maji ya juu khofu na soksi kiasi kwamba haiwezekani kuyaeleza yote kwa haraka. Kwa ujumla uchunguzi kuhusu jambo hili unafungamana na maangalizi juu ya; kujuzu (kupaka maji) na kutokujuzu, kuweka mpaka wa kupaka, mahali pake, sifa ya mahali pake, wakati wake, sharti zake na vitanguzi vyake.

Ama kujuzu kwake, hapa kuna kauli tatu: **Ya kwanza**: Kujuzu kwa hali yoyote; safarini au mjini. **Ya pili**: Kujuzu safarini na kutokujuzu mjini. **Ya tatu**: Kutokujuzu kwa namna yoyote ile, kwa sababu jambo hilo halikuthubutu katika Dini. Kauli hizi tatu zimepokewa kutoka katika zama za mwanzo na kutoka kwa Imam Maalik.[137]

Ama kuweka mpaka wa mahali pake; pia wametofautiana kati ya wenye kusema kwamba wajibu ni kupaka juu ya khofu, na kupaka chini yake ni suna tu.[138] Wenye kusema kwamba wajibu ni kupaka juu yake na chini yake.[139] Msemaji wa tatu anasema kwamba wajibu ni kupaka juu bila kupaka chini kwani kupaka chini siyo wajibu wala suna.[140] Na huenda kuna anayesema kwamba kuna hiyari kati ya kupaka chini na kupaka juu, popote atakapopaka kutakuwa ndiyo wajibu.[141]

137 Haya ameyasema wazi Imam Mwanafiqhi, Mwanausul, Mwanafalsafa Ibn Rushd katika uk. 14 Juz. 1 ya kitabu chake *Bidayatul Mujtahid wa Nihayatul Muqtasid*.

138 Hii ni rai ya Imam Shaafi.

139 Hii ni rai ya Ibn Naafii.

140 Haya ni madhehebi ya Abu Hanifa, Daud, Sufiyan na wengine wengi.

141 Hii ni rai ya Ash-hab.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 93



Ama mahali pa kupaka; wale wenye kusema inajuzu kupaka juu ya khofu wametofautiana katika kupaka juu ya soksi, baadhi yao wamejawazisha na wengine wamezuia.[142]

Ama sifa za khofu zenye kupakwa, wamehitalifiana katika kupaka khofu zilizopasuka. Baadhi yao wamesema inafaa kuzipaka bora tu zinaitwa khofu hata kama zimepasuka mpasuko mbaya.[143] Baadhi yao wamezuia kuweko mpasuko mbele ya khofu unaoonyesha unyayo hata kama ni mpasuko mdogo.[144] Na wengine wamejawazisha kuzipaka, kwa sharti mpasuko uwe mdogo.[145]

Na kuhusu wakati wa kupaka pia wametofautiana: Baadhi yao wamesema hakuna wakati maalumu, na kwamba mwenye kuvaa khofu atakuwa akipaka (khofu) maadamu hajazivua au hajapatwa na janaba.[146] Na wengine wamesema kuwa hilo limewekewa wakati maalumu kwa mtu aliye mjini na wakati mwingine maalumu kwa aliye safarini.[147] Hapa pia kuna hitilafu juu ya sifa ya hii safari na kuna hitilafu juu ya umbali wa safari.

Ama sharti za kupaka juu khofu: miguu iwe twahara tena twahara ya udhu wakati wa kuzivaa. Hii ni sharti iliyosemwa na wengi wao, lakini imepokewa kutoka kwa Maalik kutoshurutisha sharti hii.[148] Na wametofautiana katika mlango huu: kuhusu mwenye kuosha miguu yake, akavaa khofu zake kisha akakamilisha udhu wake. Je kule kuosha kabla ya kuzi-

142. Aliyejawazisha ni Sufyani Thauri, Abu Yusuf na Muhammad ibn Al-Hasan Al-Shaibani, na waliozuia ni Abu Hanifa, Shaafi na wengine.

143 Haya yamepokewa kutoka kwa Sufyan.

144 Hii ni moja ya kauli mbili za Shaafi katika mas-ala haya.

145 Hii imepokewa kutoka kwa Maalik na wafuasi (as-hab) wake. Na Abu Hanifa ameweka mpaka wa mpasuko kwamba uwe chini ya vidole vitatu.

146 Hii imepokewa kutoka kwa Maalik.

147 Haya ndio madhehebi ya Abu Hanifa na Shaafi.

148 Haya ameyataja Ibn Lubanah katika *Al-Muntakhab*. Na pia imepokewa kutoka kwa Ibn Al-Qasim kutoka kwa Maalik.

vaa kunatosheleza au hakuna budi ya kuzipaka maji tena? Hapa kuna kauli mbili.[149]

Ama vitanguzi ambavyo wametofautina: Miongoni mwa vitanguzi ni kuvua khofu, wengine wamesema twahara itabaki khofu zikivuliwa mpaka apate hadathi yenye kutangua udhu na siyo lazima kwake kuosha miguu yake.[150] Wengine wamesema: Twahara itatanguka kwa kuvua tu khofu,[151] na wengine wamesema twahara yake itabaki akiosha miguu yake baada ya kizivua, na akiswali bila ya kuosha miguu yake basi atarudia kuswali baada ya kuiosha.[152] Na nyingine sizizokuwa hizi miongoni mwa kauli zao walizotofautiana na madhehebi tofauti juu ya kupaka maji katika khofu mbili, na sasa hivi hatuko katika kuzieleza kwa urefu.

Ama walilonalo Imamiya wa zamani na waliofuatia - kwa kufuata Maimamu wa kizazi kitakatifu - ni kwamba haijuzu kupaka juu khofu mbili. Sawa sawa akiwa mjini au safarini. Na inatutosha kuwa ni hoja katika haya, neno la Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema: **“Na mpake (maji) vichwa vyenu na miguu yenu mpaka katika fundo mbili.” (5:6).** Kwa sababu aya hii inajulisha kupaka maji miguu yenyewe, sasa kupaka juu ya khofu kumetoka wapi? Je, aya hii imefutwa? Au ni katika zile ambazo ni *mutashabihaat*’ (haziko wazi maana yake)? La, bali hiyo - kwa *ijmaa* ya kauli moja - ni katika zile ambazo ni *muhkamaat* (zilizo wazi) ambazo ndio mama wa Kitabu, na kuna *ijmaa* ya wenye kutafsiri[153]

149 Miongoni mwa waliosema kuwa inatosheleza ni Abu Hanifah, na miongoni mwa waliosema kuwa haitoshelezi ni Shaafi.

150 Miongoni mwa waliosema kauli hii ni Daud na Ibn Abii Laila.

151 Hii ni rai ya Al-Hasan ibn Hay.

152 Miongoni mwa waliosema hivyo ni Shaafi, na katika kila kauli katika hizi kauli tatu kuna kundi la wanafiqihi wa Tabiina waliolisema.

153 Ijmaa hii ameinukuu Fakhrud Dini Ar-Razi uk. 371 Juz. 3 katika tafsiri yake Al-Kabir.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 95



(Qur'ani) kwamba katika *Surat Al-Maidah*, ambayo aya hii ya udhu iko, hakuna aya iliyofutwa isipokuwa aya: **"Enyi mlioamini msivunje alama za Mwenyezi Mungu…" (5:2).** Kwani baadhi yao wamesema kuwa aya hii peke yake ndiyo iliyofutwa na zisizokuwa hii katika aya za sura hii tukufu hazikufutwa.

Ama kuhusu Hadith zilizojulisha kuruhusiwa kupaka juu ya khofu, hata moja katika hizo haikuthubutu kwa sharti zetu, na kuongozea hilo kuna mambo yanayojulisha udhaifu wa Hadith hizo, nayo ni:
**La kwanza**: Hadith hizo zimekuja hali ya kuwa zimekikhalifu Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu na zile athari zilizopokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) kwani alisema: "Pindi mkiletewa kutoka kwangu Hadith yoyote, basi ilinganisheni na Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Ikiafikiana nacho basi ikubalini, na kama siyo hivyo basi irudisheni."[154]

**La pili:** Hizo Hadith zinagongana zenyewe kwa zenyewe na kwa sababu hiyo ndiyo kukapatikana khitilafu kubwa baina ya wale wenye kuziona kuwa ni sahihi na kuzitegemea kama ulivyojua katika yale tuliyoyaashiria hivi karibuni. Kwa sababu, si jambo lingine wao wamegongana katika kauli zao kufuatana na mgongano wa Hadith hizo. Kwa sababu hizo Hadith ndiyo mategemezi yao katika kauli hizo.[155]

154 Hadith hii utaipata uk. 371, Juz. 3 katika tafsiri ya Ar-Razi.

155 Kama alivyokiri Ibn Rushd mwanzo wa uk 15 Juz. 1 ya *Bidaya* yake alipotaja khilafu zao katika mpaka wa mahali pa kupaka. Akasema: "Na sababu ya tofauti zao ni kugongana kwa Hadith katika jambo hilo." Pia amekiri katika uk. 16 alipotaja tofauti zao kuhusu wakati wa kupaka aliposema: "Na sababu ya tofauti zao ni kutofautiana Hadith katika jambo hilo." Akasema: "Na sababu yake ni kwamba kumepokewa Hadith tatu kuhusu jambo hilo" kisha akazitaja kwa nasi zake na ikawa ile ya kwanza iko wazi kuonyesha kuwa wakati wake ni siku tatu usiku na mchana wake kwa msafiri, na siku moja na usiku wake kwa aliye mjini. Na ya pili iko wazi kuonyesha kuwa yafaa kupaka juu ya khofi kwa muda anaoutaka mwenyewe kukalifiwa na sharia bila kuweka muda maalumu. Si kwa aliye mjini wala aliye safarini. Na nassi ya tatu inapingana kabisa na zile zilizotangulia..., na mwenye kutaka kujua kwa upana tofauti ya Maimamu wanne katika mas-ala haya basi ni arudie kitabu *Al-Fiqihi A'lal Madhahibi Al-Arba'a* (fiqih ya madhehebi manne) kilicho tolewa na wizara ya wakfu ya Misri kwa kuhakikiwa na mapendekezo ya Mfalme Fuad wa kwanza.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 96



**La tatu**: Ni *ijmaa* ya Maimamu wa kizazi kitakatifu (Ali na watoto wake waliousiwa) kwamba haijuzu kupaka juu kila kitu ambacho ni kizuizi cha maji, sawa sawa kitu hicho kiwe ni khofu au soksi au viatu au kitu chochote cha aina yoyote.[156] Na Hadith zao ziko wazi kupingana na Hadith za Jamhuri[157] zenye kujulisha kufaa kupaka. Na kaida (kanuni) inayokubalika katika Hadith zinazogongana ni kutanguliza zinazoafikiana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Na hii ni pindi zikilingana daraja kwa *sanad* na *dilala*. Lakini ziko mbali sana kulinganishwa na kizito cha Mtume (s.a.w.w), wenza wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na safina ya uokovu wa umma, mlango wa mategemezi yao na ndiyo salama ya kutofautiana kwao.

**La nne:** Hadith hizi lau zingekuwa kweli zingekuwa ni *mutawatir* (zingepokewa kwa wingi) katika kila zama na kila sehemu, kwa sababu haja ya kujua twahara ya miguu katika udhu ni haja - kama tulivyosema kwanza - ya wanaume wote wa umma na wanawake wake, na ni haja yao muhimu sana mchana na usiku, wakati wakiwa mjini kwao na wakiwa kwenye safari zao. Lau kungekuwa na kitu kingine kisichokuwa kupaka maji kulikojulishwa na aya (ya udhu), basi *mukallafuna* wa zama za Utume na waliobaada yake wangekijua, na kingekuwa ni kitu kinachokubalika kwao kwa kila kizazi hususan kwa kuwa ni kitu ambacho ni ibada tupu wala si

156 Ijmai yao (a.s) imepokewa na wanazuoni kadhaa wa Imamiya. Mmoja wao ni Imam Sayyid Ali Twabatabai katika kitabu chake *Al-Burhan Alqati'i.* Na wanazuoni wa Imamiya wanamwabudu Mwenyezi Mungu kwa kujikurubisha kwake kwa kufanya amali kulingana na yanayoelezwa na madhehebi ya Maimamu wa Ahlul-Bayt katika matawi na misingi tangu zama zao (a.s) mpaka siku hii ya leo, kwani wao ndio wajuzi sana wa fiqhi yao, Hadith zao na kwa ndani na nje kuliko watu wengine.

157 Hadith zao zinazogongana na Hadith za Jamhuri ni nyingi sana mpaka akasema Imam Twabatabai katika *Al-Burhan Alqati'i* alipozitaja: “Wala haziko mbali na kuwa mutawatir.

kitu cha kuangaliwa kimaana kwa akili,[158] na ni kigeni katika mlango wa ibada ambacho kinahitaji kuwa mashuhuri kwa ugeni wake. Na lilipokuwa jambo si hivyo, imedhihirika kuanguka (Hadith hizo) kutoka katika mazingatio.

**La tano**: Hadith hizi lau zingejaliwa kuwa ni sahihi, basi ingelazimu ziwe zimefutwa na aya ya surat Al-Maidah, kwa sababu sura hiyo ndio sura ya mwisho iliyoshuka, kwani kwa sura hiyo Mwenyezi Mungu amekamilisha Dini, ametimiza neema zake na ameridhika kuwa Uislamu ndiyo dini. Wajibu wa sura hiyo ni wajibu mpaka siku ya kiyama, na haramu yake ni haramu mpaka siku ya kiyama, kama alivyosema wazi mama wa waumini A'isha aliposema kumwambia Jubeir ibn Nafir - alipohiji na akamtembelea: Ewe Jubeir, je unasoma Al-Maidah? Akasema: ndiyo. Akasema (A'isha): Hiyo ndiyo sura ya mwisho iliyoshuka, mnacho kipata katika sura hiyo miongoni mwa halali basi kifanyeni ni halali, na mnachokipata katika sura hiyo miongoni mwa haramu basi kiharamisheni.[159]

Lakini Jamhuri wameng'ang'ania kubakia hukumu ya kupaka maji juu ya khofu hata baada ya kushuka kwake (hiyo sura) kwa kutegemea Hadith ya Jarir: Alipokojoa, akatawadha, akapaka juu ya khofu zake, akaulizwa, unafanya hivyo? Akajibu: ndiyo, nimemuona Mtume wa Mwenyezi Mungu alikojoa, kisha akatawadha, na akapaka juu ya khofu zake. Hadith hii ameipokea Muslim, na amepokea kwamba Hadith hii ilikuwa inawapendeza na sababu yake ni kwamba kusilimu kwa Jarir kulikuwa

158 Lakini Imamu Abu Hanifah anaona kuwa udhu ni katika wajibu za tawassuli hazihitajii nia ndiyo zisihi, kama vile kuosha nguo iliyonajisika, na hii rai inahusika tu na kupaka juu ya khofu mbili kama unavyoona.

159. Al-Hakim ameipokea Hadith hii katika mwanzo wa tafsiri Surat Al-Maidah uk. 311 Juz. 2 ya *Al-Mustadarak*, kisha akapokea kama hii kutoka kwa Abdallah ibn A'mru ibn Al-a'sw, na akasema baada ya kupokea kila moja katika hizi Hadith mbili: Hadith hii ni sahihi kwa sharti za masheikhe wawili na hawakuipokea. Na Al-Dhahabi ameitaja katika Al-Talkhisw yake kwa kuonyesha kuwa ni sahihi kwa masharti ya masheikhe wawili (Bukhari na Muslim).

baada ya kushuka surat Al-Maidah.[160]

**Nasema:** Bali alisilimu kabla ya kushuka Al-Maidah kwa hoja kwamba alihudhuria *Hijat Alwidai* (Hija ya kuaga) pamoja na Mtume (s.a.w.w). Siku hiyo alimwamrisha - kama alivyoelezwa katika *Al-Iswabah* kwa kunukuu kutoka kwa *Sahih* mbili - awanyamazishe watu. Kwa hiyo uislamu wake ni lazima uwe kabla ya hija hiyo, na Suratul Maidah kwa yakini haikuweko kabla ya hapo.[161]

Vile vile Twabrani amepokea kutoka kwa Jarir - kama ilivyo katika kuelezwa kwake katika *Al-Iswabah* - amesema: Amesema Mtume (s.a.w.w): Hakika ndugu yenu An-Najashi amefariki. Na kufa kwa An-Najashi kulikuwa kabla ya kushuka Surat Al-Maidah, kwa vile hakuna shaka kuwa alikufa kabla ya mwaka wa kumi.

Na Qastwalani hapa alileta mambo mengine mageni kabisa aliposema - kuhusu kupaka juu ya khofu - "Huku kupaka hakukufutwa kwa kuweko Hadith ya Al-Mughira ambayo inasema wazi kwamba Mtume alipaka juu ya khofu zake katika vita vya Tabuk navyo ndiyo vita vyake vya mwisho, na Al-Maidah ilishuka kabla yake katika vita vya Almuraisi" mpaka mwisho wa maneno yake.

160 An-Nawawi amesema katika kuelezea maneno haya: "maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema katika surat Almaidah: Basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka kwenye viko na mpake maji vichwa vyenu na miguu yenu mpaka katika fundo mbili. Lau uislamu wa Jarir ungekuwa umetangulia kabla ya kushuka Almaidah, ingechukilika kuwa Hadith yake kuhusu kupaka khofu kuwa imefutwa na aya ya Almaidah, na ilipokuwa uislamu wake ni baada yake (Almaidah), tumejua kuwa Hadith yake inatumika". Mpaka mwisho wa maneno yake. Nasema: Ni nini kinacho tujulisha kuwa Hadith yake ilikuja baadaye. Na hakika sisi tumebainisha katika asili (ya kitabu) kwamba Almaidah ilikuja baada yake.

161 Inakutosha Hadith alioipokea Bukhari kuhusu kushuka baadhi ya aya zake kwa Mtume (s.a.w.w) siku ya A'rafa na hali Mtume yuko juu ya kipando chake *katika Hijat Alwida'i.*

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 99



**Ninasema:** vita vya Almuraisi ndivyo vita vya Bani Mustalaq na vilikuwa baada ya kupita mikesha miwili ya Shaaban mwaka wa tano na kuna kauli kuwa ni mwaka wa nne kama ilivyo katika Bukhari kwa kunukuu kutoka Ibn U'qbah. Na hivi ndivyo alivyoenda An-Nawawi katika *Raudhah* na kuna kauli kuwa ulikuwa ni mwaka wa sita baada ya Hijra, hakika Almaidah ilishuka baada yake na sura zingine nyingi. Wala si jambo lingine, iliyoshuka hapo ni aya ya kutayamamu nayo ni neno lake Mwenyezi Mungu katika Surat Nisai:

﴿ وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰٓ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ ٱلْغَآئِطِ أَوْ لَـٰمَسْتُمُ
ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوا۟ مَآءً فَتَيَمَّمُوا۟ صَعِيدًا طَيِّبًا فَٱمْسَحُوا۟ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُم مِّنْهُ ﴿٦﴾ ﴾

**"Na mkiwa wagonjwa au safarini au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake na hamkupata maji, basi tayamamuni kwa udongo safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu, "(5:6).**

Na riwaya katika jambo hilo imethubutu kutoka kwa A'isha, Ameitoa Alwaahidi katika kitabu chake *Asbaabi Nuzuul*, kirudie ili uwe na yakini kuwa Qastwalani alidanganyikiwa kati ya aya ya udhu na aya ya kutayamamu. Pia Al-Mughira na Jarir ni katika watu ambao haiwezekani wakawa ni hoja, na hivi karibuni utasimama na kilichotufanya tukamtia shaka huyu Al-Mughirah, na huyu Jarir ana historia pamoja na Alwasii (Imam Ali) ambayo imetufanya pia atutie shaka.

**La sita**: Hakika Mama wa waumini A'isha alikuwa - pamoja na ujuzi wake wa kuzijua Hadith, akili yake na kuwa kwake ni mashukio ya wahyi na sharia - akipinga kupaka juu ya khofu kwa ukali sana. Na Ibn Abbas - ambae ni mjuzi wa umma, mfasiri wa Qur'ani na Hadith asiyekanushika - pia alikuwa ni miongoni mwa wenye kupinga sana. Hawa wawili walifika mbali sana kupinga kiasi cha kutoa hata nafsi zao kwa ajili ya kulitetea

jambo hili. Je, huzigatii pamoja na mimi katika neno lake (A'isha):[162] "Hakika kukatwa nyayo zangu ni bora kuliko kupaka maji juu ya khofu mbili," na (Ibn Abbas) aliposema: "Hakika kupaka juu ya ngozi ya punda ni bora kwangu kuliko kupaka juu ya khofu."

Je, wewe unaona kupinga kwa namna hii kunaweza kuwa pamoja na kuzikubali zile Hadith? Sivyo hivyo, bali haviwi vivyo pamoja na tukimheshimu. Na yakiwa haya ni maneno ya waliozungumza naye ambao wanamjua unene wake na wembamba wake, ni vipi sisi tutazitegemea (hizo Hadith) pamoja na umbali wetu mkubwa nazo kwa makarne na mari-ka?

Na mwenye kuzingatia kwa mawazo huru, huku kupinga kwa watu waliokuwa pamoja na Mtume (s.a.w.w) kama mke wake, na mtoto wa ami yake, na wengine waongofu na viongozi miongoni mwa kizazi chake, ata-lazimika kuzitia shaka zile Hadith.

Mpaka hapa utajua, kusema kuwa Hadith hizo ni *mutawatir*, ni kwenda mno na kukisia kwa mafungu. Je, inawezekana zifikie kiwango cha *tawatur* na wasizijue hawa wachamungu watukufu?! Au walijifanya kuwa hawazijui?! Utakatifu ni Wako ewe Mwenyezi Mungu. Huu ni upotevu mkubwa sana. Bali lau zingekuwa ni *mutawatir* basi asingezipinga Abdallah ibn Umar,[163] na Imam Maalik katika moja ya riwaya mbili kuto-ka kwake,[164] wala hakuna wasiokuwa hawa miongoni mwa watu wema waliotangulia aliyewasuluhisha waumini.

162 Neno lake hili tutalipata mwanzo wa uk. 371 Juz. 3 ya tafsiri ya Ar-Razi, na huko kuna maneno ya Ibn Abbas.

163 A'twau amesema kama ilivyo katika uk. 372 Juz. 3 ya tafsiri ya Ar-Razi: Ibn Umar alikuwa akiwahalifu watu katika kupaka juu ya khofu, lakini yeye hakufa mpaka akawaafiki. **Nasema:** upinzani wake kumpinga Sa'd alipomuona akipaka juu ya khofu umethubutu katika *Sahihi Bukhari*.

164 Hizi riwaya mbili utazipata uk. 372 Juz. 3 ya tafsiri ya Ar-Razi na mahali pake katika vitabu vya fiqhi.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 101



Na wamemaliza kukokota wale waliosema: "Naogopa ukafiri kwa mtu asiyekubali kupaka juu ya khofu mbili."[165] Yeye anaona (anajua) kuwa kupaka juu ya khofu si katika *usuli dini* (misingi ya dini) wala si katika mambo yaliyodharura katika dini miongoni mwa *furui dini* (matawi ya dini), wala si katika mambo yaliyofaradhiwa na Kitabu (Qur'ani), wala si katika - kwa *ijmaa* ya umma - mambo yaliyolazimishwa na Hadith, isipokuwa ni mambo yaliyoruhusiwa tu tena kwa baadhi ya Waislamu bila baadhi nyingine, sasa kuna kosa gani kuacha (kupaka juu khofu) kwa kufuata yale yaliyofaradhiwa na aya ya udhu? Na hakika wamekongamana watu wote wa kibla (waislamu wote) kusema kuwa inasihi amali iliyofanywa kulingana na aya, na wameshikana kwa kuafikiana kukubalika swala iliyoswaliwa hivyo, kinyume na kupaka juu ya khofu mbili. Kwani kukubalika udhu pamoja na hilo (kupaka juu ya khofu), kuondosha hadathi kwa hilo na kukubalika swala kwa hilo, ni mambo yenye khitilafu kati ya Waislamu. Je, huogopewa ukafiri mtu aliyefanya *ihtiyat* (aliyefanya lenye uhakika na kuacha lenye shaka)?!

Enyi Waislamu mna rai gani nyinyi juu ya A'isha, Ali, ibn Abbas na baki ya watu wa nyumbani kwa Mtume (s.a.w.w.), kwani wao hawakukubali kupaka juu ya khofu!

## KUPAKA MAJI JUU YA KILEMBA

Wanazuoni wetu wamesema kuwa haijuzu kupaka maji juu ya kilemba. Na haya ndiyo madhehebi ya Shaafi, Abu Hanifah na Maalik. Na wamekhalifu wakina Imam Ahmad ibn Hambal, Abu Thaur, Al-Qasim ibn Salaam, Al-Auzayi na Thauri.[166] Pia khilafu hii imenukuliwa kutoka kwa wengine

165 Miongoni mwa watu waliosema hivyo ni Al-Karkhi kama alivyonukuu Qastwalani kutoka kwake uk. 4 Juz. 2 ya *Irshad Saari*.

166 Khilafu hii ameinukuu Ibn Rushd katika *Bidaya* yake kutoka kwa Ahmad, Abu Thaur na Alqasim. na Ar-Razi katika tafsiri yake ameinukuu kutoka kwa Al-Auzayi, Thauri na Ahmad.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 102



wasiokuwa hawa, wakasema kuwa inajuzu kwa kutumia *kiyasi* (kufananisha) na khofu. Na pia kwa kulingana na Hadith ya Mughira ibn Shu'bah kwamba Mtume (s.a.w.w) alipaka kwenye utosi wake na kwenye kilemba, na katika baadhi ya njia (za Hadith hii) kwamba alipaka juu ya kilemba bila ya kutaja utosi.

Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu kinatutosha kwa maneno yake: **"Na pakeni vichwa vyenu,"** na kwa Hadith za Mtume Wake kuwa yeye alipaka utosi wake, na hili linakubalika wala halihitajii ubainifu. Pia imenukuliwa *ijmaa mankul* na *muhaswal* (hizi ni istilahi mbili za elimu ya Usuul) katika jambo hili. *Walhamdu lillahi rabil a'lamin*.

Wala wao hawana hoja kwa kutumia *kiyasi* ya khofu, kwani Dini ya Mwenyezi Mungu haichukuliwi kwa *kiyasi*. Pia kupaka maji juu ya khofu ni kitu kisichokubalika kama ulivyojua.

Ama Hadith hiyo ya Mughira ni batili hata kama imepokewa na Muslim, kwani Abu Umar ibn Abdulbar amesema kuhusu hii Hadith kwamba ni hadith *maalul*.[167]

**Nasema:** huenda Abu Hanifah, Shaafi na Maalik hawakuitilia nguvu Hadith hii kwa sababu pia kwao ni *maalul*.

Na huyu Mughira ana sera ya vitimbi, kuhadaa, kugeukageuka, hilahila, kushikana na mambo ya madhambi, kuzama katika matamanio, kuvunja ahadi na kuvunja mipaka (sheria) katika mambo anayoyapenda na anayoyachukia hususan pamoja na wale anaowatawalisha ambao ni maadui wa watu wa nyumba ya Muhammad (s.a.w.w), na pamoja na wale anaowachukia miongoni mwa mawalii wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.

166 Amenukuu kutoka kwake Ibn Rushd uk. 10 Juz. 1 wa *Bidaya* yake

Aliingia katika Uislamu ili kuitetea damu yake (asiuwawe) kutoka kwa Bani Maalik. Kwani yeye alikwenda safari pamoja na watu watukufu (katika Bani Maalik) kwenda kwa Almaquqis aliyekuwa Iskandaria. Bani Maalik walifaulu kwa kupewa zawadi na mfalme (huyo), isipokuwa yeye hakufaulu. Kwa sababu hiyo, tamaa ikamchukua mpaka akavunja ahadi yao (pamoja na Bani Maalik), akawapa pombe, nao wakalikubali kwani walikuwa pamoja katika safari, akazidi kuwanywesha mpaka ulevi ukazichukua hisia zao na akawafanyia uadui kwa kuwaua wote na akachukua mali yao yote. Hapo akaona kuwa hakuna mtu wa kumkinga kuuwawa na ndugu zao isipokuwa ni kujiunga na Uislamu, akafunga safari ya kwenda kwa Mtume (s.a.w.w) naye alikuwa Madina, akaingia kwa Mtume na huku akisema: Nashuhudilia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na hakika Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. (Mtume) akakubali Uislamu wake kwa kufuata sunna yake iliyokuwepo katika jambo hilo pamoja na wenye imani sawa sawa au pamoja na wanafiki.

Na alipomwonyesha zile mali za Bani Maalik alijiepusha nazo, na ilikuwa azichukue kwani zilikuwa ni mali za wenye kumpiga vita na wenye kuhalalisha aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu. Lakini kwa kuwa yeye (Mughiira) alizichukua kwa kuvamia, nafsi Yake (Mtume) Tukufu ilikataa kuzichukua na akamwachia mwenyewe.**[168]** Huu ndiyo uislamu wake ambao unakupa sura ya misingi yake na kukosa kwake msimamo. Na Abu Bakarah - katika maswahaba wakubwa - na maswahibu wake walitoa ushahidi dhidi yake kwa jambo lenye kulazimu kupigwa hadi katika kad-

168 Kadhia hii ameitoa Ibn Sa'di katika kumweleza huyu Al-Mughira uk. 25 Juz. 4 ya kitabu *Twabaqaat* kwa sanadi yake mpaka kwa Al-Mughira mwenyewe amesema: Sisi tulikuwa ni kaumu ya kiarabu iliyoshikana na dini yetu na sisi ndiyo wasimamizi wa Al-lata. Waonaje lau ningewaona watu wangu wote wamesilimu singewafuata, lakini kundi la Bani Maalik lilipanga kusafiri kwenda kwa Almaquqis nikapanga kwenda pamoja nao. Mpaka mwisho wa Hadith. Na umekwisha kuisikia madhumuni yake.

hia mashuhuri miongoni mwa matukio ya mwaka wa 17 baada ya hijra,[169] sasa ni vipi tutaikataa Qur'ani tukufu kwa Hadith ya mtu huyu, enyi wenye akili?!

## JE KUPAKA KICHWA KUNA MPAKA?

Wanazuoni wetu wamesema kuwa hakuna mpaka wa kupaka maji kichwa - si kwa chenye kutumiwa kupaka wala kwa chenye kupakwa - bali kwao inatosha chochote chenye kuitwa kupaka, japo kuwa ni kitu kidogo ambacho kwa kawaida kinakubalika kuitwa kuwa ni kupaka.[170] Na haya pia ndio madhehebi ya Shaafi. Wamesema maimamu wawili; Maalik na Ahmad na wengine kwamba lililolazima ni kupaka kichwa kizima. Na Imam Abu Hanifah amesema kuwa lililolazima ni kupaka robo ya kichwa kwa kutumia vidole vitatu, na kwamba kupaka chini ya hapo kwake haitoshelezi.

Hoja yetu katika jambo hili ni kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema: **"Na pakeni vichwa vyenu,"** kwani kinachotakikana ni kupaka kichwa kwa namna yoyote ile, na hili kama linavyopatikana kwa kupaka kichwa kizima na robo yake, vile vile linapatakana kwa kiasi kinachoitwa kupaka, japo ni kwa sehemu ya kidole na kupitisha juu ya sehemu ya kichwa. Wala hakuna hoja (dalili) ya haya waliyoyasema peke yake. Lau angetaka kueneza kichwa kizima; Mwenyezi Mungu Mtakatifu angesema:

169 Utakipata kwa urefu wake katika kumweleza Yazid ibn Ziyad Al-Hamiri katika kitabu *Wafayaatil A'yaan* ya Ibn Khalqan na pia wamemwashiria wenye kueleza historia za watu walipomweleza Al-Mughira na mashahidi dhidi yake nao: Abu Bakarah, Shiblu ibn Ma'bad (hawa wawili ni maswahaba), Nafi'i ibn Al-Haarith ibn Kildah na Ziyad ibn Abihi. Na kisa ambacho hakikosekani katika kila kitabu kilichoeleza matukio ya mwaka wa 17 baada ya hijra.

170 Kwani alipokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu akipaka sehemu ya mbele ya kichwa chake pia wao walipaka sehemu hiyo hiyo ili wapate kupaka sehemu ambayo wanayakini kuwa ndiyo inayotakikana.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 105



"*Wamsahu ruusakum*" (bila kutia *bi* katika *ruusikum*) kama ilivyo katika "*faghsilu wujuhakum*." Lau kama linalotakikana ni kadiri maalumu angebainisha kama alivyofanya katika kuosha mikono miwili, kwani alisema: **"mpaka katika viwiko viwili,"** na katika kupaka miguu miwili aliposema: **"mpaka katika fundo mbili."**

## KHILAFU KATIKA MAS'ALA SITA
## 1. KUPAKA MAJI MASIKIO

Imamiya wameafikiana - kwa kufuata Maimamu wa kizazi kitakatifu - kwamba kupaka maji masikio si chochote katika udhu, kwani hakuna dalili ya kujulisha hilo si katika Kitabu (Qur'ani) au Sunna (Hadith) au *Ijmaa*, bali uwazi wa Qur'ani kwamba udhu ni maosho mawili - uso na mikono - na mapako mawili - kichwa na miguu.

Madhehebi ya Hambal wamesema: ni lazima kupaka maji masikio pamoja na ndewe zake, Ibn Rushd ameinukuu kauli hii kutoka kwa Abu Hanifah na wafuasi wake.[171] Shaafi na Maalik wamesema: Kuyapaka ni sunna, lakini wametofautiana katika kutumia maji mapya na kutokutumia maji mapya. Na miongoni mwao wamekhalifu wakasema kwamba huoshwa pamoja na kichwa. Na wengine wamesema: Ndani yake hupakwa maji pamoja na kichwa na nje yake huoshwa pamoja na uso. Na Shaafi anasema kuwa ni sunna kukariri kama ilivyo sunna kukariri kupaka maji katika kichwa.

Wao wametoa hoja kwa Hadith zisizozingatiwa ambazo hakuna hata moja iliyothubutu kwetu. Na masheikhe wawili Bukhari na Muslim hawakuzingatia hata moja katika hizo, isipokuwa waliozizingatia walizizingatia pamoja na kuwa kwao Hadith hizo ni dhaifu kwa kuzitia nguvu kwa kuwa ni mashuhuri kufanya hivyo (kupaka maji masikio) kwao.

171. Rudia katika kitabu Bidayatul Mujtahid uk. 11 Juz. 1 utampata anayanukuu haya kutoka kwa Abu Hanifa na wafuasi wake.

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 106



Lakini Maimamu wa uongofu ambao ni miongoni mwa vizito vya Mtume (s.a.w.w) hawakuzizingatia na ilhali wao ndio watu wa nyumba ya utume, na watu wa nyumbani ndiyo wanaojua zaidi kilichomo ndani ya nyumba. Na sisi tunatosheka kwa vizito viwili.

## 2. JE, INAJUZU KUOSHA KICHWA BADALA YA KUKIPAKA?

Watu wa madhehebi manne wote wameafikiana kwamba kuosha kichwa katika udhu inatosheleza badala ya kupaka, isipokuwa wametofautiana kuwa hivyo ni karaha au sio karaha. Madhehebi ya Hanafi na Maalik wamesema kuwa ni karaha kwa hoja kuwa ni kinyume na alivyoamrisha Mwenyezi Mungu. Madhehebi ya Shaafi wamesema kuwa siyo karaha lakini ni kukhalifu lililobora. Na madhehebi ya Hanafi wamesema: Hapa kuosha kunatosheleza badala ya kupaka kwa sharti ya kupitisha mkono juu ya kichwa.

Ama Imamiya, wao wameafikiana kuwa haitoshelezi, kwani ni kinyume na kile alichokiamrisha Mwenyezi Mungu, na ni kinyume na yale yaliyothubutu kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) kuwa yeye alipaka utosi Wake Mtukufu na wala hakuuosha. Huko ni kuweka sharia katika ibada na hilo lenyewe ni batili na ni lenye kubatilisha. Na hakika umekwishajua hivi karibuni kuwa kuosha na kupaka ni hakika ya mambo mawili tofauti, kila moja kati yao haliwi badala ya lingine.

## 3. MPANGILIO WA UDHU

Wamejumuika Imamiya - kwa kufuata Maimamu wa kizazi kitakatifu - kwamba ni sharti kufuata mpangilio katika vitendo vya udhu kama ilivyopangwa katika aya yake tukufu (ya udhu). [172]

172 Na wameshurutisha kufuata mpangilio katika viungo venyewe, wamesema ni lazima kuosha juu kabla ya chini kwa kufuata maimamu wao na kulingana na nususi zao (a.s).

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 107



Madhehebi ya Maalik, Hanafi na Sufiyan Thauri na Daud wote hawa hawakulishurutisha wala si lazima kwao hilo, bali wamelizingatia hilo kuwa ni sunna na kulikhalifu halibatilishi udhu. Na wamesema kuwa unaswihi udhu wa mwenye kutawadha pindi akianza kwa kuosha mguu wake wa kushoto na akamalizia udhu kwa kuosha uso, yaani kinyume na aya katika vitendo vyote vya udhu.

Hoja yetu ni Kitabu (Qur'ani) na Hadith; ama Kitabu ni ule mpango unaofahamika katika Qur'ani japo kuwa *atufi* iliyoko ni kwa *al-wau* siyo kwa *thumma* wala *al-fau* kwani *al-wau* mara nyingi huatufia kwa mpangilio, wala siyo *majazi* kufanya hivyo. Haya yamethubutu kwa kufuatilia maneno ya kiarabu ambayo hayana shaka kwa yeyote, kwa sababu hiyo Al-Kufiyuun (wananahau wa Kufa) ambao ni miongoni mwa wananahau wamesema kwamba *wau* ni *hakika* katika mpangilio hususan katika *nasaq* japo kuwa *thumma* na *al-fau* ziko dhahiri sana katika kujulisha hilo.

Ama (hoja yetu) kwa Hadith ni kulingana na udhu wa Mtume (s.a.w.w) kwani yeye alikuwa akijilazimisha kufuata mpangilio huu, sawa sawa uwe udhu wake ni kwa ajili ya swala za faradhi tano au ni kwa ajili ya kitu kingine miongoni mwa faradhi au sunna. Na alikuwa (Mtume) kwa muda wa uhai wake wote katika twahara (ya udhu) akitawadha kila udhu unapotanguka na akitawadha udhu juu ya udhu pia. Na huenda alisema: "Udhu ni nuru juu ya nuru." Na wamejumuika umma wote kuwa Yeye (s.a.w.w) hakutawadha kabisa isipokuwa ni kwa mpangilio. Lau si kushurutisha kufuata mpangilio na kuufanya kuwa ni faradhi katika udhu angekhalifu japo mara moja, au angesema wazi kuwa inajuzu kuukhalifu kwa kubainisha hukumu kama ilivyo sunna yake. Kwa kuwa hakukhalifu mpangilio wake wala hakusema wazi kwamba inajuzu kuukhalifu basi tunajua kwamba haijuzu, kwa sababu asili ya kitendo hapa inajulisha kufanya kitu ambacho kuna shaka katika usharti wake, na kufanya *istishabi* ya kitendo ni kitu chenye kufanyika kukiwa hakuna uhakika wake.

## 4. KUTUNGAMANISHA KATIKA UDHU

Wanazuoni wetu wamesema - kwa kufuata Maimamu wao (a.s) - kwamba kutungamanisha vitendo vya udhu ni sharti ya kuswihi kwake. Na namna yake, ni kutokukauka kiungo kilicho tangulia - katika wakati wa kawaida na mahali pa kawaida na kulingana na tabia ya mtu mwenyewe - kabla ya kumaliza kiungo kinachooshwa.

Madhehebi ya Shaafi na ya Hanafi wamesema kwamba kutungamanisha siyo faradhi wala si sharti wala si lazima, isipokuwa ni sunna. Kwa sababu hiyo kwao ni karaha kutokutungamanisha kati ya viungo ikiwa ni bila udhuru. Ama kama ni kwa udhuru hapana karaha. Kwa mfano akiwa amesahau au akamaliza maji aliyoyaandaa kutawadhia na akaenda kuleta maji mengine ili apate kukamilisha udhu wake. Madhehebi ya Maalik yamesema ni faradhi kutungamanisha akikumbuka, na akiwa na uwezo na siyo faradhi kwa kusahau na akiwa hawezi.

Hoja zetu ni vitendo vya Mtume (s.a.w.w), kwani alikuwa akitungamanisha katika udhu Wake kama alivyokuwa akiupanga. Hakukupokewa kabisa kutoka Kwake kutokutungamanisha vitendo vya udhu, kama vile ambavyo hakukupokewa kutoka Kwake kutofuata mpangilio wa (udhu). Na lau siyo sharti kutungamanisha basi angeacha japo mara moja, au angesema wazi kuwa inajuzu kuacha (kutungamanisha) ili abainishe hukumu ya sharia kwa kufuata sunna yake katika kuweka sharia zinazotoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, maadamu hakufanya hivyo tunajua kuwa haijuzu.

Pamoja na hayo, hakuna khitilafu kuswihi udhu uliokusanya sharti hizi, ama ukiwa haukukusanya sharti hizi huwa kuna khitilafu kuswihi kwake. Maimamu wa Ahlul Bayt (a.s) hawauoni (udhu huo) kuwa unaondosha hadathi au unahalalisha swala, kwa hiyo fanya *ihtiyat* (toka katika shaka) katika dini yako, na *ihtiyat* hapa ni kitu kisicho na budi, kwani kitendo kwa

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 109



asili hujulisha kufanya kitu chenye shaka katika usharti wake, na kufanya *istisw-habi* ya hadathi ni kitu chenye kufanyika ikiwa hakuna uhakika wake kama tulivyotangulia kusema.

## 5. KUTIA NIA

Wamejumuika Imamiya - kwa kufuata Maimamu na vizito viwili - kwamba kutia nia ni sharti ya kuswihi udhu na kuoga, kwani hizo ni miongoni mwa ibada ambazo Mwenyezi Mungu ameziamrisha **"Wala hawakuamrishwa ila wamwabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Yeye dini." (98:5).** Na haya ndiyo madhehebi ya Shaafi, Maalik, Ahmad, Daud, Abu Thaur na wengine wengi miongoni mwa maimamu wa jamhuri.

Na madhehebi ya Hanafi wamesema kuwa wajibu wa udhu na kuoga ni iwe kwa maji ya kawaida, wala si jambo lingine isipokuwa ni *tawasulia* (kufika) kwenye twahara ambayo hupatikana kwa kuchurizisha tu maji kwenye kiungo, iwe pamoja na nia au isiwe pamoja na nia; bali hata bila hiari kama kuosha nguo iliyonajisika, kwani maji kwa asili yake ni kitu chenye kutwahirisha. Na wamesema: Mtu akianguka kwenye maji bila ya hiari yake, au akaingia kwenye maji kwa nia ya kucheza au kujiburudisha au kujisafisha au akawa anaonyesha mfano wa kitendo cha mtu mwingine au (akafanya hivyo) kwa ria na maji yakaenea katika viungo vyake vya udhu basi inaswihi yeye kuswali kwa udhu huu, hata kama alipoingia kwenye maji alikuwa kafiri na akasilimu wakati wa kutoka kwake, kwa sababu wao hawakushurutisha uislamu katika kuswihi udhu.

Ndiyo, wao wameshurutisha nia katika kuswihi tayamumi kwa sababu *swai'd* (ardhi ya kutayamumia) kwa asili yake siyo kitu chenye kutwaharisha, isipokuwa kutwaharisha kwake ni kwa *taabudia* (kufatana na amri ya sharia) kwa hiyo katika tayamumi hapana budi kutia nia. Vile vile kutawadha na kuoga kwa kutumia *nabidhi* (togwa; kinywaji kinacho tengenezwa kwa tende au zabibu au shairi n.k) la tende au mabaki ya maji ya punda au nyumbu kwani utwaharishi wa nabidhi na mabaki hayo ni kama *swai'd*.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 110



Kwa ujumla, wamepambanua kutawadha na kuoga kati ya kutumia togwa la tende au mabaki ya punda na nyumbu na kati ya kutawadha na kuoga kwa kutumia maji ya kawaida. La kwanza wamelizingatia kuwa ni ibada *ghairu ma'kulatil ma'na*' (maana yake haikubaliki kiakili) na wakawajibisha kutia nia kama katika tayamumi. Na la pili wamelizingatia ni katika wajibu za *tawasulia* (wajibu zisizohitaji nia) ili kufika katika usafi wenye kuonekana kwa hisia kama kujitwahirisha kutokana na najisi.

Wala sijui ni nini kilichowajulisha kwamba malengo ya Mwenye kuweka sharia (Mwenyezi Mungu) kwa kuweka udhu na kuoga si kitu kingine isipokuwa ni twahara yenye kuonekana kwa hisia ambayo hupatikana kwa nafsi ya kuchuruzisha maji tu?!

Kwa hakika kila Mwislamu, wa kike na wakiume, anajua kuwa kutawadha na kuoga si jambo lingine isipokuwa ni kuondosha athari za hadathi ili kupata uhalali wa kuswali na mambo mengine yasiyoswihi mpaka kwa sharti ya kuondolewa hadath. Na haya si mambo ya kuhisiwa wala kufahamika lau si kuabudu kwa kutekeleza maamrisho matukufu kutoka kwa Mwenye hekma asiye na mwisho kwa kila hakika na kila undani wenye kufichikana kwa binadamu, majini, malaika na viumbe wengine. Ndio, tunaamini kuwa kutawadha ni kwa ajili ya kuondosha athari za hadath ndogo, na kuoga ni kwa ajili ya kuondosha hadath kubwa, na yote ni kwa kuabudu, kama tunavyoamini katika faradhi za swala, saumu, zaka na haji kwa namna zao, kiasi chao na wakati wao.

Kiasi cha kujisafisha kama inavyoonekana kwa hisia katika udhu na kuoga katika nyakati nyingi hakuwafanyi wao kufika katika twahara hizo, kama ilivyokuwa kumpa kitu cha kuweza kuishi mwenye kustahiki kupewa zaka hakuwezi kuitoa zaka katika ibada na kuifanya ni *tawasulia*, yaani muhimu ni kumwezesha kuishi tu. Na ni hivi hivi katika khumsi, kafara, swadaka zingine na ibada zingine za kimali. Lau lengo la kutawadha na kuoga lingekuwa ni kiasi cha kupatikana twahara ya kuonekana kwa hisia tu, basi isingekuwa ni lazima kwa mwenye hadath kutawadha akiwa ni nadhifu

sana na hana uchafu wowote. Na haya yamevunja *ijmaa* ya waislamu na yamekhalifu lile lililothubutu kutoka kwa Bwana wa Mitume aliposema (s.a.w.w): “Mwenyezi Mungu hakubali swala ya mwenye hadath mpaka atawadhe” na amesema: “Mwenyezi Mungu hakubali swala bila twahara, wala swadaka ya mwenye kukhini.”

Na hapa kunaweza kutolewa hoja juu ya usharti wa nia kwa Qur’ani na Hadith, na kuongeza yale yanayojulishwa na *aslul a’mali* (asili ya kitendo) kuwa ni lazima kuhakikisha sharti yenye shaka juu ya usharti wake, pia kufanya *istisw-hab* (kujaalia lililokuweko) kubakia hadath wakati wa kutawadha bila kutia nia.

Ama Kitabu (Qur’ani) ni aya mbili kwa pamoja za Surat Al-Maida na Al-Bayyina, kwani aya ya Al-Maida, nayo: **“Pindi mkisimama kwenda kuswali basi osheni nyuso zenu...” (5:6)** mpaka mwisho wake, inajulisha *sughra* katika *shakli* ya *kiyasi* (istilahi za kimantiki) nayo ni kwamba kutawadha na kuoga ni miongoni mwa mambo tuliyoamrishwa. Na aya ya Surat Al-Bayyina nayo: **“Wala hawakuamrishwa ila wamwabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Yeye dini” (98:5).** Hii inathibitisha *kubra* ya *shakli* nayo ni kwamba kila tulichoamrishwa ni lazima kukitakasia Mwenyezi Mungu, lakini katika hoja hii kuna uchunguzi bali kuna mushkili.

Ama Hadith, ni kauli Yake (s.a.w.w) katika Hadith mashuhuri: “Hakika si jambo lingine amali ni kwa nia,” kwa kukadiria hivi “hakika si jambo lingine kuswihi kwa amali kunapatikana katika nia.” Lakini madhehebi ya Hanafi wanaweza kusema: Hukadiriwa hivi “Hakika si jambo lingine kukamilika amali ni kwa nia.” Kwa hiyo haiwezi kuwa ni hoja (dalili) ya haya tunayoyasema. Na wanaweza kujibiwa kwamba, kukadiria kwa kwanza ni bora kwa sababu kuswihi ni jambo linalolazimu sana uhakika wa jambo kuliko ukamilifu, sasa kuchukulia hivyo ni bora kwa sababu kitu ambacho ni chenye kulazimu katika kitu kingine huwa ni karibu sana kuwa ni muhimu katika akili wakati wa kutamkwa tamko lake, mwisho. Pamoja

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 112



na hivyo katika hoja hii kuna uchunguzi.

Na sisi Imamiya katika mambo tunayomwabudu Mwenyezi Mungu kwa kuwafuata Maimamu wa kizazi kitakatifu na madhehebi yao kwa nafsi yake ni hoja kwetu. Kwani wao ndio washirika wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu, (wao ndiyo) chombo cha sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu, ndiyo safina la kuokoa umma, atasalamika mwenye kulipanda na ataghariki mwenye kubaki nyuma, (wao) ndiyo mlango wa ngome na atakaosalimika mwenye kuiingia, ndiyo kamba yenye nguvu isiokatika, ndiyo amani ya umma kutokana na kukhitalifiana, na ni amani kutokana na adhabu, (wao) ndio yai la Mtume wa Mwenyezi Mungu lililopasuka kutoka kwake, ndiyo watawalishi wake, ndiyo mawaswii wake, ndiyo warithi wa elimu yake na hekma zake, ndiyo wabora wa watu kwake, na kwa sharia kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama ilivyotolewa buruhani (dalili) katika mahali pake katika *Al-Murajaa't* yetu ya *Azharia* na mahali pengine.

## 6. KUTAWADHA KWA KUTUMIA NABIDH (*TOGWA*)

Wamejumuika Imamiya - kwa kufuata Maimamu miongoni mwa kizazi cha Muhammad (s.a.w.w) - kwamba ni sharti maji ya kutawadhia na kuogea yawe ni maji ya kawaida, sawa sawa (mtu) awe mjini kwake au awe safarini. Pia wameafikiana kwamba ikiwa ni udhuru kutumia maji basi italazimika kwa mukalafi atayamamu kwa kutumia *sai'd* (ardhi) twahara bila ya kuwa na nafasi ya kutumia kitu kingine. Na haya ndio madhehebi ya Shaafi, Maalik, Ahmad na wengine.

Na Imamu Abu Hanifa na Sufiyani Thauri wamekwenda kujawazisha kutawadha na kuoga kwa kutumia togwa la tende[173] kwa aliye safarini akikosa maji.[174] Hasan Al-Busri na Abul-A'liya Rafi'i ibn Mahran wameona ni karaha. Na A'twaa ibn Abii Rabaha amesema: Kwangu kutayama-

173 Nabidh (togwa) ni maji yanayotokana na kitu kama tende na zabibu, hutolewa utamu wake kwa kulowekwa kwenye maji. Nayo iko aina mbili; yenye kulewesha na isiolewesha. Na mahali penye ugomvi hapa ni lile lisiloleweshа. Ama lenye kulewesha hakuna khilafu kuwa halijuzu kutawadhia sawa sawa liwe nabidh au kitu kingine (chenye kulewesha).

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 113



mu ni bora kuliko kutawadha kwa kutumia maziwa na mtindi,[175] na Al-Auzai amejawazisha kutawadha na kuoga kwa kutumia *nabidh* (togwa) lolote (hata kama siyo la tende)[176] bali kwa kutumia kitu chochote cha majimaji ambacho ni twahara.[177]

Hoja ya Imamiya na kila mwenye rai kama yao katika mas-ala haya - pamoja na kuongezea *Al-aslul al-a'mali* (asili ya kitendo) - ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, Sunna za Mtume wake (s.a.w.w) na *ijmaa* ya umma.

Ama Kitabu (Qur'ani) ni kauli Yake Mwenyezi Mungu: **"Na kama hamkupata maji basi tayamumini (kwa kutumia) sai'd (ardhi) iliyo safi (twahara) na mpake nyuso zenu na mikono yenu"(4:43),** pindi alipotamka amri ya kutayamamu kwa kukosekana maji wala hakujaalia kitu kingine katikati baina ya maji na *sai'd* (ardhi).

---

174 Kauli hii ni mutawatir kwa Abu Hanifa. Ibn Rushd amenukuu kutoka kwake katika *Bidayat Almujtahid*, na Imam Ar-Razi alipozungumzia aya ya tayamumi uk. 375 Juz. 3 ya tafsiri yake Al-Kabir na ametia Al-Sindi katika Mlango wa kutawadha kwa kutumia nabidh katika maelezo yake kuieleza *Sunan ibn Maja* kwa kunukuu kutoka kwa Abu Hanifa na Al-Thauri.

175 Bukhari amenukuu katika *Sahih* yake kutoka kwa kila mmoja kati ya Al-Hasan Al-Busri, Abul-A'liya na A'twaa katika mwanzo wa Mlango wa 'Kutokujuzu Kutawadha kwa Kutumia Nabidh Wala Chenye Kulewesha' kama tulivyokunukulia kutoka kwao katika asili ya kitabu hiki, rudia.

176 Kama alivyosema wazi Qastwalani katika uk. 43 Juz. 2 ya *Irshad Al-Sari*.

177 Kama Imam Ar-Razi alivyonukuu kutoka kwake katika uk. 375 Juz. 3 ya tafsiri yake aliposema: Al-Auzai na Al-Aswam wamekwenda kusema kuwa inajuzu kutawadha na kuoga kwa kutumia kitu chochote cha majimaji ambacho ni twahara.

Ama Sunna (Hadith) linatutosha neno la Mtume (s.a.w.w): “Ardhi safi ni udhu wa mwislamu kama amekosa maji...” Mpaka mwisho wa Hadith hii, na Hadith hii ni kama aya iliyotangulia katika kutaja (vyenye kufaa kutawadhia) bila kutaja kitu kingine.

Ama *Ijmaa* ni kwamba watu wote wa kibla (waislamu wote) katika masala haya wako katika rai moja, na aliyekhalifu, huyo amekiuka na amevunja *ijmaa* ya waislamu, wala kukiuka kwake hakuzingatiwi, kwa mfano yule aliyesema kuwa haijuzu kutawadha kwa kutumia maji ya bahari.[178]

Abu Hanifa na Thauri na wenye rai kama yao wametoa hoja kwa Hadith iliyopokewa kutoka kwa Ibn Mas’ud kwa njia mbili:

**Ya kwanza**: kutoka kwa Abbas ibn Al-Walid ibn Swabih Al-Khalal Aldemeshqi kutoka kwa Marwan ibn Muhammad Al-Twatwari Al-Demishqi kutoka kwa Abdallah ibn Lahia’h kutoka kwa Qais ibn Al-Hajaj kutoka kwa Hansh Al-Swanai’ kutoka kwa Abdallah ibn Abbas kutoka kwa Ibn Mas’ud kwamba Mtume (s.a.w.w) katika usiku wa Aljin alimuuliza: Una maji? akasema: Sina isipokuwa nina *nabidh* katika *sat-hiya*[179] (chombo), Mtume (s.a.w.w) akasema: Hizo ni tende nzuri na maji twahara, nipe, akasema: Nikampa na akatawadhia.

Hadith hii kwa njia hii ameitoa Muhammad ibn Yazid ibn Majah Al-Kazweni katika Mlango wa ‘Kutawadha kwa Nabidh’ katika *Sunan* yake. Wala hakuna hata mtu mmoja katika waandishi wa *Sunan* (vitabu vya Hadith) aliyeipokea Hadith hii kwa njia hii isipokuwa ni yeye tu, kama ninavyojua,

178 Abdallah ibn A’mru ibn Al-A’sw alikuwa akikataza kutawadha kwa kutumia maji ya bahari kama ilivyomashuhuri kutoka kwake, Ar-Razi ameyanukuu haya kutoka kwake alipokuwa akizungumzia aya ya udhu katika Surat Al-Maida.

179 Sat-hiya ni chombo cha maji kinacho tengenezwa kwa ngozi mbili zikawa zaelekeana, na sehemu ya juu inaweza ikawa ndogo na inaweza ikawa kubwa.

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 115



na hilo ni kwa sababu ya giza lililomo kwenye Hadith hii baada ya giza. Kwani huyu Abbas ibn Al-Walid hakuwa mtu mkweli wala mwenye kuaminiwa. Wanazuoni wa kuchambua wapokezi wa Hadith walimuacha mpaka Abu Daud aliulizwa kuhusu mtu huyu - katika (kitabu) *Mizan Al-i'tidal* - akasema: Alikuwa ni mjuzi wa wapokezi na Hadith lakini sipokei kutoka kwake.

Na wewe unajua kuwa wao si jambo lingine walimuacha kwa sababu ya udhaifu wake. Na ama sheikhe wake Marwan ibn Muhammad Al-Twatwari alikuwa ni miongoni mwa wapotevu wa madhehebi ya Murjia, na Al-u'qaili amemtaja katika Kitabu *Al-Dhuafaa* (kitabu cha watu dhaifu). Pia amesema wazi juu ya udhaifu wake ibn Hazmi. Haya yote utayajua katika maelezo yake katika *Mizan Al-I'tidal*. Ukiongeza kwamba sheikhe wake Abdalllah ibn Lahia'h ni miongoni mwa wale waliofanywa na wanazuoni wa wapokezi wa Hadith kuwa ni watu dhaifu. Rudia maneno yao katika kumzungumzia mtu huyu katika vitabu vyao, kama; *Mizan Al-I'tidal* na vingine, utampata kuwa ameshuhudiwa udhaifu wake na Ibn Mui'n, ibn Sai'd na wengine. Na huko kuna matatizo mengine kuhusu wasiokuwa hawa watatu miongoni mwa wapokezi wa njia hii, wala hatuna haja ya kuyabainisha.

**Ama njia ya pili** katika njia mbili za Hadith hii inaishia kwa Abu Zaid ambaye alikuwa ni mtumwa wa A'mar ibn Hariith kutoka kwa Abdallah Ibn Mas'ud: Kwamba Mtume (s.a.w.w) alimuuliza katika usiku wa Aljin: Una maji yenye kutwaharisha? Akasema: Sina, isipokuwa kitu kidogo cha *nabidh* katika vyombo. Akasema (s.a.w.w): (hizo) Ni tende nzuri na maji yenye kutwaharisha, na akatawadha kwa kutumia hiyo.

Hadith hii imepokewa na ibn Majah, Tirmidhi na Abu Daud. Na katika mapokezi ya Abu Daud hakuna: Na akatawadha kwa kutumia hilo. Na Hadith hii kwa njia hii pia ni batili kama ilivyobatilika katika njia ya kwan-za. Na inakutosha kubatilika kwake kuwa imepita kwa Abu Zaid ambaye ni mtumwa wa A'mur ibn Hariith, naye ni mtu asiyejulikana kwa

wanazuoni wa Hadith kama alivyosema dhahiri Tirmidhi na wengine. Na Dhahabi amemtaja katika *Alkuna* katika *Mizani* yake na akasema wazi kwamba yeye hajulikani na amepokea kutoka kwa Ibn Mas'ud na Hadith yake haiswihi. Na Bukhari naye amemtaja katika watu dhaifu. Na matni ya Hadith yake ni: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alitawadha kwa *nabidh*," na Al-Hakim amesema kuwa yeye ni mtu asiyejulikana na yeye hana Hadith isipokuwa ni hii ambayo ni batili.

Kwa ujumla wanazuoni waliotangulia, kundi baada ya kundi, wameifanya Hadith hii ni dhaifu[180] kwa kila njia zake mbili. Pia Hadith hii inagongana na Hadith iliyopokewa na Tirmidhi katika *Sahihi* yake. Abu Daud katika Mlango wa Udhu katika *Sunan* yake, na maimamu wote wameifanya ni *sahihi*, (imepokewa) kutoka kwa A'lqama kwamba yeye alimuuliza Ibn Mas'ud akasema: Ni nani miongoni mwenu alikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) katika usiku wa Aljin? Akajibu: hakuna hata mmoja katika sisi alikuwa pamoja naye.

Lau tutajaalia kuwa Hadith hii imeswihi na wala haikugongana, basi aya ya tayamumi itakuwa ni yenye kuifuta, kwa sababu usiku wa Aljin ulikuwa Makka kabla ya hijra na aya ya tayamumi ni ya Madina bila ya khilafu yoyote.[181]

Pia inafaa kuichukulia Hadith hii - lau tutaijaalia imeswihi - kwamba kwenye vile vyombo vya maji kulikuwa na tende kavu kidogo, ambazo hazikuyabadilisha maji na wala kuharibu sifa zake.

---

180 Kama alivyosema wazi hayo Qastwalani na Sheikhe Zakaria Al-Answari katika sherehe zao za *Sahihi Bukhari*, rudia mlango wa kutokujuzu kutawadha kwa kutumia nabidh wala chenye kulewesha uk. 43 na uliyo baada yake katika Juz. 2 ya sherehe mbili zilizopigwa chapa pamoja.

181 Kabla ya hapo udhu ulikuwa ni sunna, wala tayamumi ilikuwa haijawekewa sharia mpaka aya yake iliposhuka baada ya hijra.

Al-Auzayi, Al-Aswam na mwenye rai kama yao wametoa hoja ya kujuzu kutawadha na kuoga kwa kutumia vitu vingine vya majimaji vilivyo twahara; na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu si jambo lingine ameamrisha kuosha na kupaka maji, na mambo hayo mawili kama yanavyopatikana kwa kutumia maji ya kawaida pia yanapatikana kwa kutumia kitu kingine cha majimaji kilicho twahara.

**Jawabu lake**: Mwenyezi Mungu Mtukufu ameifanya tayamumi kuwa ni wajibu wakati wa kukosekana maji, na kujawazisha kutawadha kwa kutumia kitu kingine kunabatilisha haya, na hiki ni kitu kinachofanya kuwa kuosha kulikoamrishwa katika aya hii kumeshurutishwa ni kwa maji peke yake kama ilivyowazi. Na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufahamu hivi.

Huenda Madhehebi ya Hanafi wamejawazisha kutawadha kwa kutumia maziwa yaliyochanganywa na maji kama ilivyotolewa hikaya kutoka kwao,[182] kwa kutegemea kile walichokitegemea Al-Auzayi na Al-Aswam Hatim ibn A’nwan Al-Balkhi.

Haya ndiyo ambayo Mwenyezi Mungu amemfanyia wepesi mja Wake na mtoto wa waja Wake wawili; Abdul-Husein ibn Sharif Yusuf ibn Al-Jawad ibn Ismail ibn Mohamed ibn Muhammad ibn Sharafud Diin Ibrahim ibn Zain Al-A’bidin ibn Ali Nurud-Din ibn Nurud-Diin Ali ibn Al-Husein A`l Abi-Hasan Al-Musawi Al-A’mili.

Na kila sifa njema zote ni Zake Mwenyezi Mungu Bwana wa viumbe vyote.

182 Miongoni mwa hikaya alizozitoa Imam Qastwalani kutoka kwao (madhehebi ya Hanafi) katika mlango wa kutokujuzu kutawadha kwa kutumia nabidh wala chenye kulewesha uk. 44 Juz. 2 ya *Irshad Saari*, na hapa ninakunukulia kwa tamko lake: “Ama maziwa safi hayajuzu kutawadhia kwa ijmaa, na yakichanganyikana na maji basi yanajuzu katika madhehebi ya Hanafi.”

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 118



# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja’a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali

87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 122



114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?

Mas'ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd 7/2/2011 11:25 AM Page 123



140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Tatu
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Elimu ya Ghaibu
152. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.1
153. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.2
154. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.3
155. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza

Mas’ala ya Kifiqhi-Mpya.qxd  7/2/2011  11:25 AM  Page 124



# BACK COVER

Kitabu hiki huelezea hitilafu zilizopo baina ya Shia na Sunni kuhusu masiala (mas'ala) ya kifikihi na matendo mengine ya kiibada. Wafuasi wa madhehebu hizi wamekuwa wakishutumiana na kila upande ukiona upande wa mwenzake kuwa umepotoka. Sheria zote za Kislamu ziwe za matendo ya kiibada au za kimaisha chimbuko lake ni kutoka kwenye Qur'ani na Sunna, na madhehebu zote za Kiislamu zinakubaliana na kaida hii.

Hivyo, mwanachuoni huyu mkubwa wa Kiislamu anajaribu kuyachambua masiala haya ya kifikihi (kifqhi) ambayo madhehebu hizi hutofautiana kwa kutoa dalili na hoja kutoka kwenye Qur'ani na Sunna na pia matukio ya kihistoria kwa kutumia hoja za kielimu na ujuzi alionao.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info